Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Ujumbe – Sehemu ya Nne

Author(s):

Sheikh Jafar Subhani [3]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The Message, kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, Ujumbe. Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Nne.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Translator(s):

Maalim Dhikiri U.M. Kiondo [5]

Category:

General [6]

Topic Tags:

Historia [7]
Vita [8]
Jeshi [9]

Hadith [10]

Person Tags:

Mtume Muhammad (s.a.w) [11]
Imam Ali (as) [12]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, The *Message,* kilichoandikwa na Sheikh Ja'far Subhani. Sisi tumekiita, *Ujumbe.* Kwa vile kitabu hiki ni kikubwa, tumekigawa katika juzuu nne ili kuwarahisishia wasomaji wetu kukisoma kwa makini katika kila sehemu. Hii uliyonayo mkononi ni Juzuu ya Nne.

Kitabu hiki kilichoandikwa na mwanachuoni mkubwa Sheikh Ja'far Subhani kimekuwa ni miongoni mwa vitabu bora vilivyofanya utafiti wa kina kuhusu historia ya Uislamu na Waislamu.

Haya ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na mwanachuoni mwandishi wa kitabu hiki juu ya maudhui haya yaliyotaja hapo juu.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni mambo ambayo hayana nafasi tena katika akili za watu. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imea- mua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Maalim Dhikiri Kiondo (Allah *'Azza wa Jalla* amkubalie amali zake na amweke karibu na Maasumina 14 [a.s.] - Amin) kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam
Tanzania.

Utangulizi

Kwa Jina La Allah, Mwingi Wa Rehema, Rahimu.

Tangu zamani za kale, mwanadamu amekuwa akiitafuta elimu kupitia milango yake ya fahamu. Hivyo basi, kwa kuvitambua vitu, hujaribu kulitatua tatizo lake. Katika mchakato huu, amekuwa akifanya majaribio, na hatimaye kwa kubahatisha alifikie kwenye ufumbuzi uwezekanao wa matatizo yake. Ikiwa imetegemea juu ya dhana na utendaji huu, sayansi ilistawi kwa ukubwa mno kwenye maeneo na nyanja mbali mbali za matu- mizi yake.

Kwenye zama hizi mpya za sayansi, mamia na maelfu ya maabara ya utafiti yanavutia nadharia ya wanasayansi ambao hufanya ugunduzi na ubunifu mkubwa mno wa kiwango cha kutoaminika cha usahihi wa ala na zana. Vivyo, kitu pekee ambacho hadi sasa sayansi imeshindwa kukikamata ni tatizo la kijamii. Ni dhahiri kwamba matatizo ya kijamii ni matatizo ya wanadamu. Na matatizo ya wanadamu ni ya hali ambayo haiwezi kuingizwa kwenye neli ya majaribio /testityubu (test-tube). Ili kuisadiki habari hii, mtu yuatambua vizuri mno kwa mfano, ya kwamba bado sayansi hai- jatoa jibu la kutoafikiana na chuki iliyomo miongoni mwa watu au tofauti za kimatabaka zinazokithiri kwenye matabaka ya jamii za wanaadamu.

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu, zilizochakaa. Hakuna shaka kwamba sayansi inagundua habari za maisha kwa njia ya ufukuaji wa mashimo yanayodhaniwa kuwa na vitu vya kale kwa ajili ya uchunguzi, na kwa kujifunza masalio ya vitu visivyo na uhai (relics) na (vikisukuku) vile vyenye uhai vilivyogeuka kuwa mawe (fossilis), vilivyogandamana na miamba ya ardhi. Lakini tukiyaachilia mbali yote hayo, hakuna matokeo ya dhahiri yaliyopatikana kuhusiana na matatizo mengi ya wanaadamu.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikara zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema: “Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao, kwa juhudu nyingi niliyapitia matendo yao, nilizifikiria fikara na matendo yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu; na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika, historia imeandika habari zote, zile zenye kupendeza na zenye kuchukiza, lakini lile lisikitishalo ni kwamba hakuna yeyote aliyejali kuzama ndani ya kina cha sababu za habari hizo. Ama kuhusu ufumbuzi halisi wa tatizo, liwe kubwa au dogo, hakuna juhudi katika upande wa mwanaadamu uonekanao kwenye historia. Ni yale mambo yasiyo muhimu ndiyo yaliyoshughulikiwa kwa maelezo

marefu yaogofyayo.

Kwa kuwa historia ni masimulizi ya matukio ya kale yaliyoandikwa, yana– pata kuwepo kwake kutoka kwa mwandishi wake. Watu walioiandika historia hawakuwa huru kutokana na kiburi cha ubinafsi, rangi au sehemu atokayo mtu, na hivyo basi, lengo lake hasa laonekana kushindwa. Mbele ya tafsiri mbaya na uzushi wa habari za kihistoria, msomaji wa kawaida wa historia yumo kwenye hasara ya kuuelewa ukweli wa jambo hilo. Ni kama daktari ambaye, kama hana taarifa sahihi kuhusu maradhi ya mgonjwa wake anayemwuguza, hataweza kuchunguza maradhi halisi ya mgonjwa wake huyo.

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taar– ifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda histo– ria kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).
Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote, wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kujifunza maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.), mkuu zaidi miongoni mwa wanaadamu wote, kunachukuliwa kuwa ni kwenye kuleta hofu na kujierevusha. Nyororo ya matukio ya kabla na ya baada ya kuzaliwa kwa huyu mtu mkuu kunatoa mawazo kwa ajili ya kila mtu aliye na japo punje ndogo tu ya akili na hisia za ulinganifu.

Kuzaliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) akiwa yu mtoto aliyezaliwa baada ya baba yake kufariki dunia, na kifo cha mama yake, Bibi Amina (a.s.), alipokuwa na umri wa miaka sita tu, na kulelewa kwake, kwanza na babu yake na kisha na ami yake ni mambo yasiyo kifani.

Baada ya kuyapitisha maisha yenye mambo mengi, kujitenga kwake kwenye Pango la Mlima Hira na Ufunuo wa Allah uliofuatia, kuwaitia watu kwenye dini ya Allah, upinzani wa makafiri na wenye kuabudu masanamu, maonevu na mateso yao, umadhubuti wake uliodumu katika kuimarisha ujumbe wa Allah kwenye kipindi cha miaka kumi na mitatu ya mwanzo ya Utume wake mjini Makkahh hadi kwenye muda wa kuhamia kwake Madinah, ni matukio yasiyo kifani kwenye historia.

Miaka kumi ya mwisho ya maisha yake mjini Madina, kuimarisha kwake juhudi za ujumbe wake kwa ajili ya uenezaji wa Uislamu, kushiriki kwake kwenye vita nyingi dhidi ya makafiri na hatimaye kutekwa kwa Makkahh bado ni matukio makuu yenye kuonekana kuwa si ya kuaminika, lakini yameandikwa kwenye historia kuwa ni mafanikio ya kimiujiza.

Mamia ya vitabu yameandika kuhusiana na maisha na ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) lakini vitabu hivi haviwezi kuchukuliwa kuwa ni wasifu kamili juu ya sifa na mafanikio yake. Hasa yale maandishi ya mustashrik yameingiliwa na chuki, makosa na tafsiri potofu.

Kitabu hiki sio tu kwamba kinatoa mambo yenye kuongoza, bali vile vile kimezitegemeza taarifa zake kwenye maandiko ya kihistoria yaliyo ukweli. Moja ya sifa zake zijidhihirishazo mno ni kwamba mwandishi amechukua hadhari kubwa katika kuyasimulia matukio ya kihistoria, na wakati huohuo amejitahidi, akiwa yu mwanachuoni mtafiti, kuyaendea matukio hayo kwa fikara zenye kuchanganua mambo pia.

Sifa nyingine, ya kitabu hiki yenye kuvutia ni kuwa kiko huru kabisa kutokana na uzushi na hadithi zilizobuniwa zilizozushwa na faida zilizofichwa. Kwa maneno mengine ni kwamba, kiko kabisa kwenye hali ya kusalia kwenye kiwango kihitajikacho cha ukweli wa kihistoria. Kwa kifupi ni kwamba, kinapelekwa kwa Waislamu kwa ujumla, bila ya upendeleo na kiburi.

Tunategemea ya kwamba kitabu hiki kitalifikia lengo lake la kukiongoza kizazi kichanga chenye shauku kuu ya kujipatia taarifa za kweli na zenye kutegemewa juu ya huyu Mtume Mkuu wa Uislamu (s.a.w.), na tunaamini ya kwamba vijana wetu wa kiislamu watajipatia mwongozo kutokana na kitabu hiki katika kuyatengeneza maisha yao kwa mujibu wa maamrisho ya Allah pamoja na sifa tukufu za Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Dhuria wake Wateule (a.s.).

Kuhusiana Nasi

(Inawahusu watoaji wa toleo la Kiingereza ambalo kitabu hiki ni tafsiri yake)

Leo hii, akili iliyo macho huyaona mabadiliko kwenye maisha ya kiakili ya mwanaadamu. Sayansi na teknolojia, vikiwa kwenye ustawi wake wa juu zaidi, vyaelekea kukifikia kipeo chake cha mwisho. Mahitaji ya kimwili pamoja na tamaa ya mamlaka na tawala vimemwongoza mwanaadamu kwenye ufisadi wa dhahiri wa maadili yake. Katika hali hii ya kukatisha tamaa, mtu alazimika kutulia na kuitathmini hatari iliyojificha na inay– owatishia wanaadamu wote kwa ujumla. Mwanaadamu, tayari kaisha mkodolea macho tena Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu, kwa kuwa, sasa kaishatambua ya kwamba ufumbuzi wa matatizo yake na wokovu wake umo kwenye kuzifuata Amri za Allah.
Mgeuko huu, wa kutoka kwenye fikara za kimwili na kuja kwenye fikara za kiroho unaafikiana kabisa na malengo na shabaha za hii Seminari ya kiislamu. Mafundisho ya dini yanakwenda sambamba na maendeleo ya huu wakati wetu, yakitoa kimbilio lihitajiwalo mno na akili yenye kusumbuka na mashaka.

Haya ni matokeo ya mtanabahisho, ya kwamba sasa inatambulikana ya kwamba siri ya kuishi maisha ya kiuchamungu kwenye ulimwengu huu huongoza kwenye baraka ya milele ya maisha ya Ahera. Huu ndio ujumbe wa UISLAMU kwa ulimwengu mzima.

Hii Seminari ya kiislamu inadhamiria kuinua juu kurunzi ya mwongozo wa kiroho na kusaidia kwa juhudi zote katika kuukuza urithi wa mwanaadamu. Inaionyesha njia ya maisha ifundishwayo na Qur’ani katika

utukufu wake wa asili. Inayaonyesha yale yenye nguvu na yaliyo ya kweli tu. Vitabu vyake vimekusudiwa kufaa katika kuyafikia mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi. Vitatumika kama kijito kitiririkacho maji daima, kwa wale walio na kiu ya elimu.

Hii Seminari ya kiislamu ni taasisi ya ulimwengu mzima yenye kujitahidi katika kudumisha udugu wa kiislamu. Inafurahia mchango wa akili zilizo bora zaidi, zaidi ya kuwa na msaada wa kimataifa kwa ajili ya kuyafikia malengo yake makuu. Inavyo vituo Canada, na Mashariki ya Mbali.

Orodha ya anwani iko kwenye kurasa za mwisho za kitabu hiki. Msomaji (wa Kiingereza) anaweza kukiandikia barua chochote miongoni mwa vituo hivi ili kuvipata vitabu vyetu.

Islamic Seminary Publications

Kwa Ndugu Msomaji

Asalaam Alaykum

Kitabu hiki kinatolewa na Seminari ya kiislamu (S.L.B. 5425, Karachi, Pakistan). Vitabu vyake vimelengwa kuyatimiza mahitaji ya kiroho ya zama zetu hizi, na msisitizo maalum juu ya kuzisafisha akili na fikara. Juhudi nyingi zimefanywa na Seminari hii kuweka kwenye vitabu vyake yale yaliyo na nguvu na yaliyo ukweli halisi kwenye Uislamu.

Unaombwa kukisoma kitabu hiki katika hali iliyodhamiriwa. Vilevile unaombwa kuwasiliana nasi, kuhusu maoni yaliyo huru kuhusu vitabu vyetu, jambo tutakalolipenda mno.

Kuubalighisha ujumbe wa Uislamu ni jukumu lihitajilo ushirikiano wa watu wote. Seminari hii inakukaribisha ushiriki kwenye jukumu hili ukiuitika mwito wa aya ya Qur'ani Tukufu isemayo:

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۖ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مَثْنَىٰ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۚ{46}

"...Sema: Mimi ninakuahidini jambo moja tu, ya kwamba msimame kwa ajili ya Allah, wawili-wawili na mmoja-mmoja..." **(*As-Saba, 34:46*).** ***Allah na Akubariki. Nduguyo katika Uislamu, Katibu wa Uchapishaji.***

Sura Ya 49: Vita Vya Hunayn

Ilikuwa ni desturi ya Mtume (s.a.w.w.) kwamba kila alipoliteka eneo fulani, yeye mwenyewe alikuwa akiyaangalia matatizo yale ya kisaiasa na mambo ya kidini ya wakazi wake kwa kadiri akaavyo kwenye eneo lile, na anapoondoka kwenye eneo hilo aliwateua watu waliofaa kuzishika nafasi mbalimbali.

Sababu yake ilikuwa kwamba, watu wa eneo lile walioizoea mipango ya kale na iliyozongwa zongwa hawakuwa na ujuzi wa mpango mpya na ulioichukua nafasi ya ile ya kale.

Uislamu ni mpango wa kijamii, kimaadili, kisiasa na kidini. Sheria zake zinatokana na ufunuo, na kunawajuvya watu sheria hizi na utelekezaji wake miongoni mwao kunahitaji watu wanaotambulika waliokomaa kiakili na wenye elimu, watakaowafunza misingi sahihi ya Uislamu kwa hekima, na vilevile kusimamia utekelezaji wa mfumo wa Kiislamu miongoni mwao.

Mtume (s.a.w.w.) alipoamua kuondoka mjini Makka na kuiendea nchi ya makabila ya Hawaazin na Saqif, alimteua Mu'aaz bin Jabal kuwa kiongozi ili awaelimishe na kuwaelekeza watu, na akaiweka serikali na utawala wa mji ule na vile vile uimamu (wa Sala) mle msikitini mikononi mwa 'Atab bin Usayd, mtu aliyekuwa na uwezo. Baada ya kukaa mjini Makka kwa muda wa siku kumi na tano Mtume (s.a.w.w.) alikwenda kwenye nchi ya kabila la Hawaazin.1

Jeshi Lisilo Na Kifani

Katika siku ile Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na askari elfu kumi na mbili wenye silaha waliokuwa chini ya bendera yake. Miongoni mwao askari elfu kumi walikuwa wale waliofuatana naye kutoka Madina, na walishiriki katika kutekwa kwa mji wa Makkah, na wale elfu mbili wangine waliotoka miongoni mwa Waquraishi waliosilimu karibuni tu. Ukamanda wa kundi hili ulikuwa mikononi mwa Abu Sufyani.

Katika siku zile jeshi kubwa kiasi kile halikuweza kuonekana mahali popote pale, na nguvu yao hii ya wingi ikawa ndio sababu ya kushindwa kwao. Ilikuwa kwa sababu, kinyume na siku za nyuma, walijifaharisha kutokana na idadi kubwa ya askari wao na wakazitupilia mbali mbinu za kijeshi na kanuni za kivita. Macho ya Abu Bakr yalipoiangukia ile idadi kubwa ya askari alisema: "Katu sisi hatuwezi kushindwa hata kidogo, kwa kuwa idadi ya askari wetu imezidi sana ile ya adui."2 Hata hivyo, yeye hakuzingatia ukweli kwamba ukubwa wa idadi sio sababu pekee iletayo ushindi, na kwa kweli sababu hii ni ya umuhimu mdogo tu.

Qur'ani Tukufu yenyewe inautaja ukweli huu na inasema:

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ ۙ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ ۙ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ

عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُمْ مُدْبِرِينَ {25}

“Hakika Allah amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayn ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu. Na ardhi ikawa finyu kwenu juu ya upana wake. Kisha mkageuka mkarudi nyuma.” (*Sura al-Tawbah*, 9:25).

Upatikanaji Wa Taarifa

Baada ya kutekwa kwa mji wa Makka msisimko na shauku kubwa viliweza kuonekana kwenye maeneo yaliyokaliwa na makabila ya Hawaazin na Saqif. Mawasiliano maalum yalikuwapo baina yao. Kiunganisho baina yao kilikuwa ni mtu wa kupenda vita aliyeitwa Malik bin Awf Nasri. Matokeo ya mawasiliano yao yalikuwa kwamba kabla ya lile jeshi la Kiislamu kuonyesha kuwajali, wao wenyewe walijitokeza kupambana nalo ili kwamba kabla ya Waislamu kutoka, wao wenyewe wawashambulie vikali mno kwa mbinu za kijeshi. Vile vile walimchagua kutoka miongoni mwao mtu mwenye umri wa miaka thelathini aliyekuwa shujaa na shupavu ili awe kamanda wao.

Zaidi ya hayo makabila mawili tuliyoyataja, makabila ya Bani Hilal, Bani Nasr na Bani Jasham nayo yalishiriki vilevile kwenye vita hivi na wote walitoka kama jeshi moja lenye kushambulia.

Kama ilivyoamrishwa na yule kamanda wao mkuu, wale wote walioshiriki kwenye vita hivi waliwaweka wanawake wao na wale wawategemeao nyuma ya kikosi cha mwisho cha jeshi lile.

Alipoulizwa sababu ya uamuzi ule, alijibu akisema: “Wanaume hawa watasalia thabiti katika mapigano yao ili kuwahami wanawake na mali zao na kamwe hawatafikiria kukimbia au kurudi nyuma.”3

Pale Durayd bin Sammah, mzee na shujaa mzoefu alipovisikia vilio vya wanawake na watoto aligombana na Malik na akakichukulia kitendo chake hiki kuwa ni kosa kwa mtazamo wa kanuni za kivita, alimwambia: “Matokeo ya kitendo hiki yatakuwa kwamba kama mkishindwa mtakuwa mmewatoa wanawake na mali zenu zote kwa jeshi la Waislamu bila ya sababu.” Malik hakuyasikiliza maneno ya askari huyu mzoefu, nae akamjibu akisema: “Wewe umeshazeeka na umeshapoteza hekima na ujuzi wako wa mbinu za kivita.” Hata hivyo, matokeo ya baadae yalidhihirisha kwamba yule mzee alikuwa sahihi na kuwako kwa wanawake na watoto kwenye eneo la shughuli za kijeshi ambamo mtu anapaswa kupiga na kukimbia kulithibitisha kuwa hakuna faida yoyote, ila tu kwamba wale askari walijitia kwenye matatizo na mishughuliko yao ilitatizwa.

Mtume (s.a.w.w.) alimtuma Abdullah Aslami bila ya kutambulika ili akakusanye taarifa juu ya zana, malengo na utaratibu wa safari ya adui. Alitangatanga miongoni mwa jeshi zima la adui, akakusanya taarifa muhimu na kumletea Mtume (s.a.w.w.). Malik naye aliwatuma majasusi watatu kwa Waislamu kwa njia maalum ili wamletee tarifa zihitajikazo. Hata hivyo, wao walirejea kwa Malik wakiwa na nyoyo zilizojawa na hofu na woga.

Kamanda wa lile jeshi la adui akaamua kufanya mabadiliko yatakayofaa kwa ule uduni wa idadi na udhaifu wa nyoyo wa askari wake kwa njia ya hila za kijeshi, yaani kufanya mashambulizi ya kushitukiza, kusababisha mchafuko miongoni mwa jeshi la Waislamu ili kwamba nidhamu ya vikosi vyao ivurugike na mpango wa uongozi wao mkuu uharibike.

Ili kulifikia lengo hili, alipiga kambi mwishoni mwa njia ya kuingilia kwenye eneo la Hunain. Kisha aliwaamrisha askari wote kujificha nyuma ya mawe, majabali na vipenyo vya milima na kwenye sehemu za miinuko ziizungukazo njia ile, na mara tu jeshi la Uislamu liwasilipo kwenye njia hii ndefu na yenye kina kirefu, wote watoke kwenye maficho yao na kuvishambulia vikozi vya Uislamu kwa mishale na mawe. Baada ya hapo, kikundi maalum kishuke kutoka kule milimani kwa utaratibu mzuri na kuwauwa Waislamu kwa msaada wa kukingwa na wapiga mishale wao.

Zana Za Waislamu

Mtume (s.a.w.w.) aliitambua nguvu na ukaidi wa adui yule. Hivyo basi, kabla ya kutoka Makka alimwita SafwAn bin Umayyah na kuazima deraya mia moja kutoka kwake na akamhakikishia kuzirejesha kwake. Yeye mwenyewe alivaa deraya mbili, akavaa kofia ya chuma, akampanda yule nyumbu mweupe aliyewasilishwa kwake, na akatembea nyuma ya jeshi la Uislamu.

Wakati wa usiku jeshi la Uislamu lilipumzika kwenye mlango wa kuingilia wa njia ile, na ilikuwa bado hakujakucha vizuri pale kabila la Bani Salim lilipowasili kwenye ile njia ya Hunayn likiwa chini ya uamiri jeshi wa Khalid bin Walid. Wakati sehemu kubwa ya jeshi la Uislamu ilipokuwa bado imo kwenye njia ile, kelele za ghafla za mvumo ya mishale na mingurumo ya askari waliokuwa wakiotea nyuma ya majabali zilisikika na zikaleta hofu isiyo kifani na woga miongoni mwa Waislamu. Mishale ilikuwa ikimiminwa juu yao na kikundi cha maadui kikaanza kuwashambulia kikilindwa na wapiga mishale.

Hili shambulio la ghafla liliwaogofya mno Waislamu kiasi kwamba walianza kukimbia na wao wenyewe walisababisha mvurugiko wa safu za jeshi lao zaidi ya vile walivyofanya wae adui. Matokeo haya yalikuwa chanzo cha furaha kubwa mno kwa wanafiki waliomo kwenye jeshi la Waislamu, kiasi kwamba Abu Sufyani akasema: “Waislamu watakimbia hadi kwenye ufuko wa bahari.” Mnafiki mwingine akasema: “Uchawi umebatilishwa.” Mtu wa tatu miongoni mwao alidhamiria kuulia mbali Uislamu kwenye ile hali ya machafuko ya mambo kwa kumuua Mtume (s.a.w.w.) na hivyo kuiangamiza itikadi ya Upweke wa Allah na Utume wa Uislamu, vyote jumla.

Uimara Wa Mtume (S.A.W.W.) Na Kikundi Cha Watu Wenye Kujitoa Mhanga

Mtume (s.a.w.w.) aliingiwa na wasiwasi sana kutokana na kukimbia kwa marafiki zake ambapo kulikuwa ndio sababu kuu ya mshituko na mvurugiko, na alijihisi kwamba kama mambo yakiruhusiwa kwenda kama yalivyo, japo kwa kitambo kidogo tu zaidi ya hapo, basi mhimili wa historia utakuwa tofauti,

binadamu wataubadili mwelekeo wake na nguvu za ushirikina zitaliangusha jeshi la itikadi ya Upweke wa Allah. Hivyo basi, akiwa amempanda ngamia wake, alisema kwa sauti kuu: “Enyi Wasaidizi wa Allah na Mtume Wake! Mimi ni mja wa Allah na Mtume Wake.”

Aliitamka sentensi hii na kisha akamgeuzia yule nyumbu wake kwenye uwanja wa vita uliokuwa ukikaliwa na askari wa Malik, ambao tayari waliishawauwa baadhi ya Waislamu na walikuwa wakiendelea kuwauwa wengine. Kikundi cha watu waliojitoa mhanga, kama vile Sayyidna Ali Amirul–Mu’minin (a.s.), Abbas, Fadhl bin Abbas, Usamah na Abi Sufyan bin Harith, ambao walikuwa hawakumwacha Mtume (s.a.w.w.) akiwa peke yake na bila ya ulinzi tangu mwanzoni mwa vita vilipoanza, vile vile walisonga mbele pamoja naye.4

Mtume (s.a.w.w.) alimwomba ami yake Abbas, aliyekuwa na sauti kuu mno, kuwaita Waislamu warudi kwa namna hii: “Enyi Ansar, mliomsaidia Mtume! Enyi mliokula kiapo cha utii kwa Mtume chini ya mti wa Peponi! Mnakwenda wapi? Mtume yuko hapa!” Maneno haya ya Abbas yaliyafikia masikio ya Waislamu na kuamsha moyo wa dini na nguvu. Mara moja wote wakaitika kwa kusema: *“Labbayk! Labbayk”* na wakarudi vitani kishujaa, wakimrudia Mtume (s.a.w.w.).

Mwito wa Abbas uliorudiwa rudiwa, uliobashiria usalama wa Mtume (s.a.w), uliwafanya wale watu wanaokimbia wamrudie Mtume (s.a.w.w.) kwa masikitiko yasiyo kifani na majuto na ukawafanya wazisimamishe safu zao upya. Kwa kuitika maamrisho ya Mtume (s.a.w.w.) na vile vile kulifuta lile doa lenye kuabisha la kuukimbia uwanja wa vita, Waislamu walifanya mashambulizi ya pamoja na kwa muda mfupi tu wakawalazimisha maadui kurudi nyuma au kukimbia. Ili kuwatia moyo Waislamu, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akisema: “Mimi ni Mtume wa Allah nami kamwe sisemi uwongo na Allah ameniahidi ushindi.”

Mbinu hii ya kivita iliwafanya wapiganaji wa Hawaazin na Saqif kukimbilia kwenye eneo la Autas na Nakhlah na kwenye ngome za Taaif na kuwaacha wanawake wao na watu walioandamana nao na idadi kadhaa ya wale waliouawa katika vita hivyo.

Ngawira Za Vita

Katika vita hivi wale waliouawa katika upande wa Waislamu walikuwa wengi, lakini waandishi wa wasifu hawakuitaja idadi ya wale waliouawa. Hata hivyo, Waislamu waliweza kupata ushindi na maadui wakakimbia wakiacha nyuma yao mateka elfu sita, ngamia elfu ishirini na nne, kondoo elfu arobaini na Waqih5 elfu nne za fedha. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba watu na mali zote vipelekwe Ji’raanah. Vile vile aliwateuwa watu fulani kuziangalia ngawira zile. Wale mateka waliwekwa kwenye nyumba maalum na Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba ngawira zote zibakie hapo zilipo hadi atakaporejea kutoka Taaif.

---

1. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk. 137.

2. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk. 150

3. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 897.

4. Kwenye Maghaazil, Juz. 3, uk. 602, Waaqidi ameyataja baadhi ya matendo ya kijasiri ya Amirul–Mu'minin (a.s.) kwenye hali ile ngumu sana.

5. Waqih moja ni karibuni sawa na gramu 213.

Sura Ya 50: Vita Vya Ta'if

Ta'if ni moja ya miji ya nchi ya Hijaz yenye ardhi yenye rutuba. Mji huu uko upande wa Kusini Mashariki mwa Makka yapata umbali wa ligi 12 (Kilomita 58). Mji huu uko meta elfu moja juu ya usawa wa bahari. Kutokana na hali ya hewa nzuri ya Ta'if, bustani na mashamba ya mitende, mji wa Taa'if ulikuwa ni kituo cha kundi moja la watu walioishi maisha ya raha mustarehe!

Mji huu ulikaliwa na kabila la Saqif lililokuwa moja ya makabila ya Kiarabu yenye nguvu na umaarufu. Waarabu wa kabila la Saqif walikuwa miongoni mwa watu wale waliopigana dhidi ya Uislamu kweye Vita vya Hunayn. Baada ya kushindwa vibaya walikimbilia kwenye mji wao wenye ngome madhubuti na zilizoinuka juu.

Ili kuukamilisha ushindi wa Hunayn, Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha ya kwamba wale watoro wa Vita vya Hunayn wafuatiliwe. Abu 'Aamar Ash'ari na Abu Musa Ash'ari walipelekwa pamoja na kikosi cha askari wa Uislamu ili kuwafuatilia baadhi ya watoro waliokimbilia Awtaas. Yule kamanda wa kwanza (Abu Aamr Ash'ari) alipoteza uhai wake kwenye mapambano lakini yule wa pili (Abu Musa Ash'ari) alipata ushindi kamili na kuwatawanya maadui.1

Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alikwenda Taa'if akifuatana na jeshi lililosalia2 na alipokuwa njiani aliivunja ngome ya Malik, (ambaye alivichochea vita vya Hunayn). Kwa kweli ubomoaji wa ngome ya Malik haukuchua mwelekeo wowote wa kulipiza kisasi. Bali alichokitaka Mtume (s.a.w.w.) kilikuwa kwamba asiiache sehemu inayoweza kutumika kama kimbilio la maadui.

Makundi ya jeshi la Uislamu yalisonga mbele, moja baada ya jingine na kuzifanya pande zote za mji kuwa sehemu za kupigia kambi zao. Ngome ya Taa'if ilikuwa kwenye sehemu ya mwinuko nayo ilikuwa na kuta madhubuti sana, na minara yake ya doria ililitawala eneo lote la nje. Jeshi la Uislamu lilikwenda kuizingira ngome ile, lakini ilikuwa bado haijazingirwa vya kutosha wakati maadui walipowazuia wasiendelee kwa mvua ya mishale na kuwauwa baadhi yao hapo hapo, mwanzoni kabisa.3

Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha lile jeshi lirudi nyuma na kuihamishia kambi yake kwenye sehemu isiyoweza kufikiwa na mishale ya maadui.4 Salmaan Muhammadi, ambaye mipango yake ya kijeshi iliwanufaisha Waislamu wakati wa Vita vya Handak, alimshauri Mtume (s.a.w.w.) kwamba ile ngome ya adui ipigwe mawe kwa kutumia mateo. Kwenye vita za siku zile teo ilifanya kazi inayofanywa na mizinga

kwenye vita za siku zetu hizi. Maafisa wa Uislamu walitengeneza teo chini ya uongozi wa Salmaan na wakairujumu minara na sehemu za ndani za ngome ile kwa karibuni siku ishirini. Hata hivyo, maadui nao waliendelea kupiga mishale na hivyo wakawatia majeraha wale askari wa Uislamu.

Sasa hebu tuone jinsi Waislamu walivyotengeneza teo katika hali ile. Baadhi ya watu wanasema kwamba Salmaan yeye mwenyewe aliitengeneza na akawafunza askari wa Uislamu jinsi ya kuitumia, wengine wanaamini kwamba Waislamu waliipata silaha hii ya kijeshi wakati wa kutekwa Khaybar na wakaja nayo pale Taa'if.5 Si jambo lisilowezekana kwamba Salmaan yeye mwenyewe alitengeneza ile teo na akawafunza Waislamu jinsi ya kuijenga na kuitumia. Historia inatueleza kwamba hii haikuwa teo pekee waliyokuwa nayo Waislamu, kwa sababu sambamba na vita za Hunayn na Taa'if, Mtume (s.a.w.w.) alimpeleka Tufayl bin Amr Duwsi kuyabomoa mahekalu ya masanamu ya kabila la Duws. Alirejea baada ya kufaulu kuitimiza kazi aliyopewa na Mtume (s.a.w.w.) na akamjia Mtume (s.a.w.w.) huko Taa'if pamoja na askari mia nne, wote wakiwa ni wa kabila lake, pamoja na teo na gari la kijeshi. Na kwenye vita hivi zana hizi za kijeshi alizokuwa amezipata Tufayl bin Amr Duwsi zikiwa ni ngawira za vita, nazo zikatumika.6

Kubomoa Ukuta Wa Ngome Kwa Kutumia Magari Ya Kijeshi

Ili kumfanya adui asalimu amri, ilikuwa muhimu kuishambulia ngome ile kutoka pande zote. Hivyo basi, iliamuliwa kwamba sambamba na usimikaji wa teo na kutupa mawe, magari ya kijeshi yatumike ili kuupasua ukuta wa ngome ile, ili lile jeshi la Uislamu liweze kuiingia. Hata hivyo, makundi ya askari wa Uislamu yalikabiliwa na ugumu mkubwa katika kuitimiza kazi hii, mishale ilitupwa vichwani mwao kutoka kwenye minara na kwenye sehemu nyingine za ngome ile, na hakuna yeyote aliyeweza kuukaribia ukuta ule.

Njia iliyokuwa bora zaidi ya kulifikia lengo hili ilikuwa ni ile ya kulitumia magari ya kijeshi yalilokuwa yakipatikana pamoja na majeshi yenye mipango mizuri ya zama zile katika maumbo ya kutokamilika.

Gari la kijeshi lilitengenezwa kutokana na mbao na lilifunikwa na ngozi nene nzito. Askari wenye nguvu walikaa humo na wakalisukuma kuelekea kwenye ngome ile na wakaanza kutoboa matundu kwenye ukuta, wakikingwa na gari hili. Kwa kutumia zana hii ya kijeshi askari wa Uislamu wakajishughulisha kishujaa katika kuuangusha ule ukuta. Hata hivyo, maadui walimwaga chuma na nyaya zilizoyeyushwa kwenye lile gari na kukichoma kile kifuniko chake na kuwajeruhi wale askari. Hivyo basi, mbinu hii ya kijeshi ilithibitika kwamba si yenye kufaulu kutokana na mipango ya adui, na Waislamu walishindwa kupata ushindi. Hivyo basi, wakati idadi fulani ya Waislamu ikiwa imejeruhiwa na kuuwawa, waliliacha jaribio lao hili.7

Pigo La Kiuchumi Na Kihamasa

Kupata ushindi hakutegemei zana za kijeshi za kimaada tu. Kamanda stadi anaweza kuimaliza nguvu ya adui kwa kupiga pigo la kiuchumi na kihamasa na kwa njia hii anaweza kumfanya asalimu amri. Mara

kwa mara sana mapigo ya kiuchumi na kihamasa yanathubutu kuifanya kazi vizuri kuliko majeraha ya mwili ambayo mara kwa mara askari wa adui huyapata. Taa'if ilikuwa eneo la mitende na mizabibu na ulikuwa mji maarufu nchini Hijaz mwote kwa rutuba yake. Kwa kuwa wakazi wa mji huu walikuwa wamefanya kazi kubwa katika kuyaendeleza mashamba ya mitende na mizabibu, walikuwa makini mno katika usalama wao.

Ili kuwaogofya wale waliojifungia ndani ya ngome ile, Mtume (s.a.w.w.) alitangaza kwamba, kama wakiendelea kufanya upinzani bustani zao zitatekwa ngawira. Hata hivyo wale maadui hawakuisikiliza kauli ile ya kutishia, kwa sababu hawakufikiria kwamba yule Mtume (s.a.w.w.) aliye mpole na mwenye huruma angaliweza kufanya vile. Hata hivyo, kama walivyoona, kwa ghafla tu kwamba utekelezaji wa amri ya Mtume (s.a.w.w.), ya kuzikata zile bustani na kuangushwa mitende na zile zabibu ilikuwa tayari imeshaanza. Watu wa Taa'if wakaanza kulia na kupiga makelele na wakamwomba Mtume (s.a.w.w.) asifanye vile, ikiwa ni ishara ya heshima kwa ukaribu na uhusiano uliokuwako baina yao.

Licha ya ukweli kwamba wale waliokimbilia kwenye ngome ile walikuwa ni watu wale wale waliohusika na Vita vya Hunayn na Taa'if, na vita hivi viwili vimetokea kutia hasara kubwa, lakini Mtume (s.a.w.w.) alionyesha tena ukarimu na upole kwenye uwanja wa vita, mahali ambapo kwa kawaida ni uwanja wa maonyesho ya ghadhabu na kulipiza kisasi. Aliwaamrisha masahaba zake kuacha kuikata ile miti.

Ingawa alikuwa kapoteza maafisa na askari wengi kwenye vita hizi mbili (ambazo zilisababishwa na makri za watu wa kabila la Saqif walioendesha mashambulizi ya usiku dhidi ya jeshi la Uislamu na sasa wamekimbilia kwenye pango lao kama mbweha), na ingekuwako haki ya kuyaangamiza mashamba na bustani zao ikiwa ni hatua ya kulipiza kisasi, lakini upole na huruma zake viliishinda ghadhabu yake na akawaomba marafiki zake wajiepushe na vitendo vya kuadhibu.

Kutokana na tabia za Mtume (s.a.w.w.) na jinsi ambayo daima alikuwa akiwatendea maadui zake, tunaweza kusema kwamba amri alizozitoa za kukata ile miti zilikuwa tishio tu na kama silaha hii isingelifaa, bila shaka angelijizuia kuitumia.

Mkakati Wa Mwisho Katika Kuiteka Ile Ngome Ya Taa'if

Watu wa kabila la Saqif walikuwa matajiri na wakwasi nao walimiliki idadi kubwa ya watumwa na wajakazi. Ili kupata taarifa juu ya hali ya mambo ndani ya ile ngome na kuweza kuitathimini nguvu ya adui pamoja na kujenga mfarakano miongoni mwa kundi lile lililokuwa na utaratibu mwema, Mtume (s.a.w.w.) alituma itangazwe kwamba wale watumwa wa adui watakaotoka mle ngomeni na wakakimbilia kwenye jeshi la Uislamu watakuwa waungwana huru. Mbinu hii ilifanya kazi kwa kiasi fulani, na kiasi cha watumwa ishirini walitoroka kwenye ile ngome kwa ustadi mkubwa na kujiunga na Waislamu. Walipoulizwa, ilifahamika kwamba wale waliokuwamo kwenye ile ngome hawakuwa tayari kusalimu amri kwa vyovyote vile, japo kule kuzingirwa kwa ngome ile kungeliendelea kwa mwaka mzima wasingekabiliwa na upungufu wa chakula hata kidogo.

Jeshi La Uislamu Larejea Madina

Mtume (s.a.w.w.) alizitumia mbinu zote za kimwili na za kiakili za kivita katika vita hivi, lakini uzoefu alioupata hapo ulithibitisha kwamba kuiteka ngome ile kulihitaji matendo ya ziada na subira, ambapo hali iliyokuwapo wakati ule, kurefuka kwa vita na nguvu za jeshi la Uislamu, havikuruhusu kuendelea kukaa pale Taa'if, kwa sababu, kwanza kabisa kwenye kipindi cha uzingiraji huu watu kumi na watatu waliuawa, miongoni mwao watu saba walitoka miongoni mwa Waquraishi, wanne walikuwa Ansar na wawili walikuwa wa makabila mengine. Aidha, baadhi ya watu ambao kwa bahati mbaya idadi na majina yao havikurekodiwa vitabuni, waliuawa nao pia kutokana na mashambulizi ya hila ya adui kule kwenye bonde la Hunayn, na matokeo yake yakawa kwamba kulitokea utovu wa nidhamu na kukosa moyo wa kuendelea na vita kwenye jeshi la Waislamu.

Pili, mwezi wa Shawwal ulikuwa unamalizika na mwezi wa Dhil-Qaad (ambao kupigana vita humo kumeharimishwa miongoni mwa Waarabu na baadaye Uislamu nao uliithibitisha desturi hii) ulikuwa ukija mbiombio.8

Ili kuihami desturi hii, ilikuwa muhimu kwamba kule kuzingira kukome mapema iwezekanavyo ili kwamba, lile kabila la Kiarabu la Bani Saqif liseweze kumlaumu Mtume (s.a.w.w.) kwa kosa la kuivunja desturi ile iliyo njema.

Aidha, majira ya Hija yalikaribia, na ukaguzi wa ibada za Hija ulikuwa ni jukumu la Waislamu, kwa sababu kabla ya hapa ibada zote za Hija zilikuwa zikiendeshwa chini ya uongozi wa washirikina wa Makka. Idadi kubwa sana ya watu walikuja Makka kutoka kwenye sehemu zote za Uarabuni kuja kushiriki kwenye ibada ya Hija na huu ulikuwa wakati muafaka zaidi kuuhubiri Uislamu na kuwazoeza watu ukweli wa hii dini ya Allah.

Ilikuwa muhimu kwamba Mtume (s.a.w.w.) aitumie kikamilifu nafasi hii aliyoipata kwa mara ya kwanza, na ayafikirie mambo yaliyo muhimu zaidi yalinganishwapo na kule kutekwa kwa ngome ile. Kwa kuyazingatia mambo yote hayo, Mtume (s.a.w.w.) aliukomesha yale mzingiro wa Taa'if na akaenda Jiraanah pamoja na askari wake.

Matukio Ya Baada Ya Vita

Vita vya Hunayn na Taa'if viliahirishwa na bila ya kupata matokeo ya mwisho, Mtume (s.a.w.w.) akaenda Ji'raanah kwenda kuzigawa ngawira za Vita vya Hunayn.

Ngawira walizozipata Waislamu kwenye vita ya Hunayn zilikuwa nyingi kuliko ngawira walizopata Waislamu mwenye Vita vyovyote vile vingine, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alipofika Ji'raanah alikuwa na wafungwa

6000, ngamia 24,000 zaidi ya kondoo 40,000 na fedha gramu 852 za fedha,9 na kwenye siku zile

sehemu ya gharama za jeshi la Uislamu vilevile zilipatikana kutokana na chanzo hiki cha mapato.

Mtume (s.a.w.w.) alikaa pale Ji'raanah kwa muda wa siku kumi na tatu. Kwenye kipindi hiki alijishughulisha na ugawaji wa ngawira za vita kwa njia maalum akiwaachilia baadhi ya wafugwa na kuwarejesha kwa ndugu zao; akitengeneza mpango kwa ajili ya kusalimu amri na kusilimu kwa Malik ibn Awf (yule mtu ambaye aliwajibika moja kwa moja na vita vya Hunayn na Taa'if); akionyesha moyo wa kuridhika na kushukuru kwa huduma zilizotolewa na watu mbalimbali; akizivutia, kwa sera zake za hekima, nyoyo za maadui wa Uislam kwenye dini hii ya haki; na kumaliza, kwa njia ya hotuba ya kuvutia, mgogoro ambao ulikuwa umezuka baina yake na kikundi cha Ansari.

Haya hapa ni maelezo ya masuala yaliyotajwa hapo juu:

1. Moja ya sifa zilizojitokeza zaidi za Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa kwamba katu hakuzibeua huduma walizozitoa watu au haki zao, japo ziwe ndogo kiasi gani. Na kama mtu yeyote yule akimpatia huduma alimfidia kwa ajili ya huduma ile kwa kiasi kilichosawa nayo. Mtume ameutumia muda wa utotoni mwake miongoni mwa kabila la Bani Sa'ad lililokuwa tawi la Khawaazin, na Bibi Halima Sa'adiyah alimnyonyesha na amemlea kwenye kabila lake kwa kipindi cha miaka mitano.

Kabila la Bani Sa'ad ambalo lilishiriki katika vita vya Hunayn dhidi ya Uislamu, idadi fulani ya wanawake na watoto wao pamoja na mali zao viliangukia mikononi mwa Waislamu, sasa walikuwa wakijuta kwa kile walichokitenda. Hata hivyo, walikuwa wakifikiria akilini mwao kwamba Muhammad amekulia kwenye kabila lao na amelelewa na wanawake wao, na kwa kuwa yu mpole, mwema na mtu mwenye shukrani, bila shaka atawaachia wafungwa wao kama atakumbushwa kuhusu utotoni mwake. Hivyo basi, machifu kumi na wanne wa kabila lile ambao wote walikuwa wamesilimu, walimjia Mtume (s.a.w.w.). Waliongozwa na watu wawili, mmoja wao alikuwa ni Zuhayr bin Sard na mwingine alikuwa ni mjomba wa kunyonyeshwa wa Mtume (s.a.w.w.) na walisema hivi:

"Miongoni mwa hawa wafungwa wamo mama zako wa kunyonyesha, na dada zako wa kunyonyeshwa pamoja na wale waliokuhudumia wakati wa utoto wako, na upole na huba huhitaji kwamba kuzingatia haki walizonazo baadhi yao juu yako, huna budi kuwaachia mateka wetu wote, ikiwa ni pamoja na wanawake, wanaume na watoto. Na kama tungeliyapeleka maombi haya kwa Nu'waan bin Munzir au Harith bin Abi Shamir, mtawala wa Iraq na Shamu, tungelitegemea kukubaliwa kwa maombi haya na viongozi hawa, achilia mbali wewe uliye kigezo cha upole na huba."

Akijibu ombi hili, Mtume (s.a.w.w.) aliwauliza: "Je, ni kitu gani mnachokithamini zaidi, wanawake na watoto wenu, au mali zenu?" Walimjibu wakisema: "Hatutawabadilisha wanawake wetu na watoto wetu kwa kitu chochote." Mtume akasema: "Niko tayari kusamehe fungu langu pamoja na lile la dhuria wa Abdul Muttalib, lakini mafungu ya Muhajiriin, Ansar na Waislamu wengine yanawahusu wao wenyewe na ni muhimu kwamba wao wenyewe wazisamehe haki zao. Nitakapomaliza kusali sala ya Adhuhuri msimame baina ya safu za Waislamu na mseme nao hivi: "Tunamfanya Mtume kuwa mwombezi wetu mbele ya Waislamu na kuwafanya Waislamu kuwa waamuzi wetu mbele ya Mtume ili tuweze

kurudishiwa wanawake na watoto wetu.” Wakati huo huo, mimi nitasimama na kukurudishieni fungu langu pamoja na lile fungu la dhuria wa Abdul Muttalib na vilevile nitawashauri wengine kufanya vivyo hivyo.”

Wale wajumbe wa Haazin walizungumza na Waislamu baada ya sala ya Adhuhuri kama walivyoshauriwa na Mtume (s.a.w.w.) na Mtume (s.a.w.w.) aliwapa zawadi lile fungu lake pamoja na lile la dhuria wa Abdul Muttalib. Wakimfuatisha Mtume (s.a.w.w.), Muhajiriin na Ansar nao walikubali kuyasamehe mafungu yao. Hata hivyo, ni watu wachache tu kama vile Aqra’ bin Haabis na ‘Uyainah bin Hisn Fazaari waliokataa kutoa mafungu yao. Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia hao: “Kama mkiwatoa wafungwa wenu nitakupeni wafungwa sita kwa kila mfungwa mmoja mumtoaye, kutokana na wafungwa watakaoangukia mikononi mwangu katika vita ya kwanza vitakayopiganwa baada ya hapa.”10

Hatua za kivitendo alizozichukua Mtume (s.a.w.w.) na maneno yake ya kuvutia yalifikisha kwenye kuachiliwa kwa wafungwa wote wa kabila la Bani Hawaazin ila ajuza mmoja ambaye ‘Uyainah alikataa kumwachilia. Hivyo basi, kitendo chema na cha uchamungu ambacho msingi wake ulijengwa na Bibi Halimah Sa’adiyah miaka sitini iliyopita kwenye kabila la Bani Sa’ad, kilizaa matunda baada ya miaka mingi kama matokeo yake, wafungwa wote wa kabila la Bani HawAzin waliachiwa huru. Kisha Mtume (s.a.w.w.) alimwita Shaymah, Dada yake wa kunyonya na baada ya kulitandaza joho lake chini, alimfanya akae juu yake na akamwuliza kuhusu hali ya ustawi wake pamoja na wa familia yake.11 Kwa kuwaachilia wafungwa wao, Mtume aliwafanya watu wa kabila la Bani Hawaazin wauelekee Uislamu. Hivyo basi, wote walisilimu kwa moyo mmoja na matokeo yake yakawa kwamba, Taa’if nayo vilevile ikampoteza mshiriki wake wa mwisho.

Malik Bin ‘Awf Asilimu

2. Wakati uleule Mtume (s.a.w.w.) alipata nafasi ya kutatua suala la Malik, kupitia kwa wajumbe wa Bani Sa’ad, yule chifu mwenye kichwa kigumu wa kabila la Nasr aliyevichochea vita vya Hunayn, na hatimaye akamvutia kwenye Uislamu. Kuhusiana na jambo hili, aliulizia kuhusu hali ya mambo yake na alielezwa kwamba, yeye (Malik) amekimbilia Taa’if na kwamba alikuwa akishirikiana na Bani Saqif. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mfikishieni salamu zangu kwamba kama akisilimu na kujiunga na sisi, nitawaachia watu wake na vilevile nitampa ngamia mia moja.” Wale wajumbe wa Bani Hawaazin walimfikishia Malik ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.). Malik alitambua kwamba nguvu ya Bani Saqif imedhoofika na vilevile alitambua kuongezeka kwa nguvu za Uislamu kunakoendelea kila uchao. Hivyo basi, aliamua kuondoka Taa’if na kwenda kujiunga na Waislamu.

Hata hivyo, alikuwa akichelea kwamba kama Bani Saqif watautambua uamuzi wake ule, watamzuia mle mwenye ngome yao. Hivyo basi aliunda mpango fulani. Aliagiza kwamba awekewe kitundu cha kupakia mtu juu ya ngamia kwenye sehemu iliyokuwa mbali na Taa’if. Baada ya kuifikia sehe- mu ile alimpanda ngamia wake na akaenda upesi sana hadi pale Ji’raanah na akasilimu. Mtume (s.a.w.w.) akamtendea kama alivyokwisha kuahidi na baadae alimteua kuwa kiongozi wa Waislamu wa makabila ya Bani Nasr,

Bani Thamaalah na Bani Salimah. Kutokana na heshima na hadhi yake aliyoipata kutoka kwenye upande wa Uislamu, aliyafanya maisha kuwa mabaya kwa watu wa kabila la Bani Saqif na akawatia katika dhiki ya kiuchumi.
Malik aliona haya kutokana na ule upole aliotendewa na Mtume (s.a.w.w.) na akazisoma beti fulani fulani za mashairi akiusifu utukufu wake: “Mimi sijapata kuona au kusikia miongoni mwa wanadamu wote, mtu yeyote awezaye kuwa kama Muhammad!”12

Kugawanywa Kwa Ngawira Za Vita

3. Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) walishikilia ya kwamba zile ngawira za vita zigawanywe mapema iwezekanavyo. Ili Mtume (s.a.w.w.) kuthibitisha kutokuwa kwake na mvuto na jambo lile, alisimama ubavuni mwa ngamia, akachukua kiasi fulani cha sufu kutoka kwenye nundu yake na akiwa ameibana katikati ya vidole vyake, aliwageukia watu na kusema: “Mimi sina haki yoyote kwenye ngawira zenu, hata kwenye sufu hii, ila hiyo ‘Khums’ niliyo na haki nayo. Hivyo kila mmoja wenu naarudishe kila aina ya ngawira, japo iwe ni sindano na uzi, ili kwamba igawanywe miongoni mwenu kwa usawa.”

Mtume (s.a.w) aliigawa mali yote iliyokuwamo kwenye hazina miongoni mwa Waislamu na pia aliigawa ‘Khums’ yake iliyokuwa fungu lake miongoni mwa machifu wa Waquraishi waliosilimu karibuni tu. Alimpa kila mmoja wao ngamia mia moja, ikiwa ni pamoja na Abu Sufyan, mwanawe Muawiyah, Hakim bin Hizaam, Harith bin Harith, Harith bin Hisham, Suhayl bin ‘Amr, Huwaytab bin Abdul ‘Uzzaa, Alaa bin Jaariyah na wengineo, wote wakiwa machifu wa kufuru, ushirikina na maadui wakuu wa Uislamu hadi kwenye siku chache tu zilizopita.

Kwa watu wa kundi jingine ambao cheo chao kilikuwa chini ya kile cha wale tuliowataja hapo awali, kila mtu alipata ngamia hamsini. Kutokana na zawadi hizi kubwa kubwa na mafungu maalum, watu hawa walianza kuwa na hisia za huba na upendo kwa Mtume (s.a.w.w.), lakini pia walivutika na Uislamu. Katika sheria za Kiislamu, watu wa aina hii huitwa *‘Mu’allafatul Qulubi’* (Wale ambao yahitajika kuwatia moyo) na moja ya malengo ambayo ‘Zaka’ yaweza kutumiwa ni matumizi juu yao.13

Ibn Sa’ad anasema: “Zawadi zote hizi zilitolewa kutokana na khums iliyokuwa mali ya Mtume (s.a.w.w.) na haikuwapo japo dinari moja iliy- otumiwa kutokana na mafungu ya watu wengine kwa ajili ya kuwatia moyo watu wa kundi hili.”14

Zawadi na matumizi haya aliyoyaruhusu Mtume (s.a.w.w.) zilikasirikiwa mno na baadhi ya Waislamu na hasa baadhi ya Ansar.

Wale ambao kwamba hawakuweza kuyatambua maslahi makubwa aliyoyazingatia Mtume (s.a.w.w.) katika kuzitoa zawadi hizi, walifikiria kwamba mahusiano ya udugu yamemsukuma kuigawa ile Khums ya ngawira ile miongoni mwa ndugu zake. Mtu mmoja aliyeitwa Zul Khuwaysirah wa kabila la Bani Tamim alionyesha ufidhuli mwingi mno kiasi kwamba alimwambia Mtume (s.a.w.w.): “Leo nimeyachunguza matendo yako kwa makini sana, na nimeona kwamba hukuwa mwadilifu katika

kuzigawa ngawira.” Mtume (s.a.w.w.) alichukizwa alipoyasikia maneno yake.

Dalili za hasira zilijitokeza usoni mwake, na akasema: “Ole wako! Kama mimi sifanyi uadilifu na haki, basi ni nani mwingine awezaye kufanya hivyo?” Khalifa wa pili alimwomba Mtume amruhusu amwue mtu yule, lakini Mtume (s.a.w.w.) alisema: “Mwache. Hapo baadae atakuwa kiongozi wa kikundi kitaka-choutoka Uislamu kwa jinsi ile ile ambayo mshale huutoka upinde.”15

Kama alivyotabiri Mtume (s.a.w.w.), mtu huyu alikuwa kiongozi wa Khawarij (wenye kuritadi) wakati wa utawala wa Sayyidna Ali (a.s.) na akautwaa uongozi wa kikundi kile hatari. Hata hivyo, kwa vile ni kinyume na misingi ya Uislamu kwamba adhabu itolewe kabla ya kutendeka kosa, Mtume (s.a.w.w.) hakuchukua hatua yoyote dhidi yake.

Akiwawakilisha Ansar, Sa’ad bin Ubaadah alizifikisha huzuni zao kwa Mtume (s.a.w.w.), ambapo Mtume (s.a.w.w.) alimwambia: “Wakusanye wote mahali pamoja ili niwaeleze jambo hili.” Mtume (s.a.w.w.) aliwasili kwenye ule mkutano wa Ansar kwa heshima kubwa na aliwahutubia akisema: “Mlikuwa kundi la watu waliopotoka, nanyi mmepata mwongozo kupitia kwangu mimi. Mlikuwa maskini nanyi mkawa matajiri. Mlikuwa maadui nanyi mkawa marafiki.” Wote wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Yote hayo ni sawa.”

Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Mnaweza kunijibu kwa njia nyingine vile vile na kinyume na huduma zangu na mnaweza kutaja haki mlizonazo juu yangu na mnaweza kusema: “Ewe Mtume wa Allah! Waquraishi walipokukataa, sisi tulikutambua. Hawakukusaidia, nasi tumekusaidia. Walikufanya usiyekuwa na hifadhi yoyote, nasi tulikupa kimbilio, ulikuwapo wakati ambapo wewe hukuwa na hata senti moja, nasi tukakusaidia.”

Enyi kundi la Ansar! Kwa nini mlihuzunika kwa sababu nimewapa Waquraishi mali kidogo ili waweze kuwa imara kwenye Uislamu na nimekupeni Uislamu? Je, hamridhiki kwamba watu wengine wachukue ngamia na kondoo ambapo ninyi mumchukue Mtume pamoja nanyi? Ninaapa kwa jina la Allah! Kama watu wengine wakiifuata njia fulani, na Ansari wakaifuata njia nyingine isiyokuwa ile, mimi nitaifuata ile njia waliyoifuata Ansar.”

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) aliwaombea Ansar na watoto wao baraka za Allah. Maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yaliziibua mno hisia zao kiasi kwamba wote walianza kulia, na wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Tumetosheka na mafungu yetu (tuliyopata) nasi hatuna malalamiko japo yaliyo madogo mno juu ya jambo hili.”

---

1. Maghaazil-Waaqidi, Juz. 3, uk. 915-916.
2. Bihaarul-An’waar, Juz. 21, uk. 162.
3. Siiratu-Halabi, Juz. 3, uk. 132.
4. Tabaaqatil-Kubra, Juz. 2, uk. 158.
5. Siiratu-Halabi, Juz.3, uk. 134.

6. Tabaaqatil–Kubra, Juz. 2, uk. 157.
7. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 928.
8. Kauli hii inaungwa mkono na ukweli uliokuwapo kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitoka Makka mnamo tarehe 5, Shawwal na kipindi cha kuzingira kilikuwa ni siku 20 na siku tano za mwezi huu zilizosalia zilitumiwa kwenye Vita vya Hunayn na katika kusafiri. Ama kuhusu kile kipindi cha kuzingira, kuwa siku 20, ni kwa mujibu wa masimulizi aliyoyanukuu Ibn Hishamu. Hata hivyo, Ibn Sa'ad ameki– taja kipindi cha mzingiro kuwa ni siku 40 (Tazama Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk.
9. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk 152.
10. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 949–953.
11. Tabaaqatil–Kubra, juz. 2, uk 153–154; Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 49.
12. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 491.
13. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 3, uk. 493.
14. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 3, uk. 153.
15. Maghaazi anasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alizungumzia juu yake (yaani Zul Khuwaysirah) kuwa: "Atakuwa na marafiki ambao ibada zao zilinganishwa na sala na funga zako, basi hizo sala na funga zako vitakuwa vichache mno. Wataisoma Qur'ani, lakini usomaji wao hauyavuka mitulinga yao. Watatoka nje ya dini ya Uislamu kama vile mshale ukimbiavyo upinde." (Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 496).

Sura Ya 51: Hotuba Maarufu Ya Wasifu Ya Ka'ab Bin Zuhayr

Kijana Mdogo Awa Gavana Wa Makka

Katikati ya mwezi Dhul Qa'ad ya mwaka wa nane wa Hijiriya, Mtume (s.a.w.w.) alizitoa ngawira zote za Hunayn pale Ji'raanah. Siku za Hija zilikuwa zikikaribia upesi upesi na huu ulikuwa ni mwaka wa kwanza ambao Waarabu washirikina na Waislamu walikuwa wafanye ibada za Hija pamoja chini ya ukaguzi wa serikali ya Kiislamu ya Makka. Kushiriki kwa Mtume (s.a.w.w.) kwenye ibada hizi kutaongezea fahari na utukufu wa Hija, na ilikuwa chini ya mwongozo wake wenye hekima kwamba utangazaji wa kweli na wa msingi wa Uislamu ungelifanyika kwenye ule mkusanyiko mkubwa wa watu.

Hata hivyo vilevile ilimbidi Mtume (s.a.w.w.) azifanye kazi fulani kule makao makuu (Madina), kwa sababu baada ya miezi mitatu ya kuondoka kwake mahali pale, mambo yaliyombidi ayaangalie yeye mwenyewe binafsi yalibaki bila kushughulikiwa kabisa.

Hivyo basi baada ya kuchunguza ubaya na uzuri wote wa jambo hili, Mtume (s.a.w.w.) aliona kwamba ingelifaa kutoka Makka baada ya kufanya Umrah na afike Madina upesi iwezekanavyo.

Ilikuwa muhimu kwamba awateue baadhi ya watu wa kuyatawala mambo ya kisiasa na kidini ya lile eneo lililotekwa hivi karibuni tu, ili kwamba isitokee migogoro wakati akiwa hayupo na mambo ya eneo lile yaweze kutawaliwa vizuri. Kwa kuzingatia hili, alimteua kijana aliyekuwa mvumilivu na mwenye

hekima aliyeitwa Ataab bin Usayd, ambaye wakati ule umri wake ulikuwa bado haujazidi miaka ishirini, kuwa gavana wa Makka kwa kumlipa mshahara wa kila mwezi wa dirhamu moja.

Hivyo basi kwa kumpa ugavana kijana ambaye ndio kwamba kasilimu, na kwa kule kumpendelea kijana yule kuliko watu wazima wengi, alikiondoa kizuizi cha hofu isiyokuwa na msingi na akathibitisha kivitendo kwamba kushika ofisi za Umma hutegemea uwezo tu, na umri mdogo usimzuie mtu kukifikia cheo na ofisi ya juu kabisa ya umma. Yule gavana wa Makka aliuhutubia mkutano mkubwa na akawaambia watu: “Mtume ameweka kiwango cha mshahara wangu, basi kuhusiana na jambo hili, mimi si mhitaji wa zawadi au msaada wenu.”1

Uchaguzi mwingine mzuri aliofanya Mtume (s.a.w.w.) ni kwamba alimteua Mu’aaz bin Jabal kuwasomesha watu Qur’ani na sheria za Uislamu. Yeye alikuwa mtu maarufu miongoni mwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) kwa elimu yake ya Qur’ani, fiqhi, na maamrisho ya Uislamu. Mtume (s.a.w.w.) alipomtuma kwenda Yaman, kwenda kuwa hakimu huko, Mtume (s.a.w.w.) alimwuliza: “Utategemea nini katika kutatua kutoelewana baina ya watu?” Alimjibu akisema:

“Kitabu cha Allah, Qur’ani.” Mtume (s.a.w.w.) alimwuliza: “Je, kama hakuna uamuzi maalumu upatikanao kwenye Kitabu cha Allah kuhusiana na jambo lihusikalo, utahukumu chini ya msingi gani? “ Alijibu akisema: “Nitahukumu kwa mujibu wa hukumu za Mtume wa Allah (s.a.w.w.). Kwa kuwa mimi nimezishuhudia hukumu zako kwenye mambo mbalimbali na ninazikumbuka. Kama likitokea jambo lifananalo na lile ambalo wewe umelitolea hukumu, nitaitumia hukumu ile na kuhukumu kama ulivyohukumu wewe.”

Mtume (s.a.w.w.) akamwuliza kwa mara ya tatu: “Ni njia ipi utakayoifuata endapo litatokea tatizo ambalo hakuna hukumu ya dhahiri kwenye Kitabu cha Allah wala kwenye hukumu zangu?” Alijibu, akisema: “Katika mambo ya aina hiyo, nitatumia *Ijtihad* (njia ya kuzifasiri sheria za kiislamu) na kutoa uamuzi kwa msingi wa Qur’ani Tukufu na Ahadith zako kwa usawa na uadilifu.” Hapo Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Na ashukuriwe Allah kwamba, Amemwezesha Mtume wake kumchagua mtu wa kutawala kwa uadilifu, ambaye matendo yake yanalingana na mapenzi Yake.”2

Hadith Ya Ka’ab Bin Zuhayr Bin Abi Sulma

Zuhayr bin Abi Sulma alikuwa mmoja wa mshairi wa Zama za Ujinga aliyeandika moja ya *Mu’allaqaat* (yaani kazi za kishairi bora zaidi) saba zilizobakia zimening’inizwa kwenye kuta za Ka’abah kwa muda mrefu kabla ya kushushwa kwa Qur’ani, nazo zilikuwa chanzo cha fahari na utukufu katika fasihi ya ulimwengu wa Waarabu. Zuhayr alifariki dunia kabla ya kuanza kwa Utume wa Mtume (s.a.w.w.), na akaacha wana wawili walioitwa Buhayr na Ka’ab. Buhayr alikuwa mfuasi mwaminifu wa Mtume (s.a.w.w.), lakini Ka’ab alikuwa akifikiriwa kwamba yu mmoja wa maadui zake wakali. Kwa vile alijaaliwa kipaji chenye nguvu cha kurithi, (yaani ushairi – kutoka kwa mzazi) alimzulia na kumtusi Mtume (s.a.w.w.) kwenye mashairi yake na akawachochea watu kuamka dhidi Uislamu.

Mtume (s.a.w.w.) aliwasili Madina mnamo mwezi 24 Dhil-Qa'ad. Buhayr yule nduguye Ka'ab alikuwa amefuatana na Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kuuteka mji wa Makka na kuzingiwa kwa Taa'if vilevile pamoja na wakati wa kurejea kwake Madina.

Aliona kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliwatishia kifo washairi fulani fulani waliokuwa na kashfa kama yule ndugu yake, na waliowachochea watu kuupinga Uislamu, na ametangaza damu yao kuwa ni halali na hatimaye mmojawao aliuawa na wengine wawili walikimbilia kwenye sehemu zisizojulikana.
Buhayr alimwandikia barua nduguye Ka'ab akimwarifu hali ile na mwishoni mwa barua ile ikiwa ni dalili ya kumtakia wema, alitaja kwamba kama akiendelea kuwa adui kwa Mtume (s.a.w.w.), basi atayapoteza maisha yake, lakini kama akija kwa Mtume (s.a.w.w.) na kudhihirisha kuyajutia kwake matendo yake, atasamehewa, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na tabia za kuyakubali maombi ya msamaha na majuto ya wakosefu na hatimae kuwasamehe.
Ka'ab aliyekuwa na imani thabiti juu ya ndugu yake, alikuja Madina. Alipowasili kwenye Masjidun-Nabi, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa yu tayari kwa kusali sala ya Alfajiri. Ka'ab akasali kwa mara ya kwanza pamoja na Mtume (s.a.w.w.). Kisha alikwenda na kukaa ubavuni pake na kuuweka mkono wake mkononi mwake Mtume (s.a.w.w.), na kusema: "Ewe Mtume wa Allah! Ka'ab anaona haya mno na yu mwenye kuyajutia matendo yake na hivi sasa amekuja kusilimu. Je, utayakubali maombi yake ya msamaha kama akikujia mbele yako yeye mwenyewe?" Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: "Ndio." Baada ya hapo Ka'ab akasema: "Mimi ndimi Ka'ab bin Zuhayr mwenyewe."

Ili kuyasahihisha matusi na masengenyo ya tangu kale, Kaab alikuwa tayari kaishatunga maneno ya wasifu wa kifasaha akimsifu Mtume (s.a.w.w.).3 Aliyasoma maelezo hayo ya wasifu mle msikitini mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake. Wasifu huu mzuri sana ni kazi ya sanaa mahiri kabisa miongoni mwa hotuba za wasifu za Ka'ab. Tangu siku uliposomwa mbele ya Mtume (s.a.w.w.) Waislamu wamekuwa wakiukariri na kuueneza miongoni mwa watu wengine. Wanachuoni wa Kiislamu nao wameandika sherehe (mafafanuzi) yake. Wasifu huu uliandikwa kwa mtindo wa '*Laamiyah*' 4 nao una beti hamsini na nane.

Kama wale washairi wa zama za Ujinga waliozianza sifa zao kwa kuwataja wapenzi wao au kwa kuyataja magofu ya minara, yeye anaanza wasifu wake kwa kumkumbuka binamu na mpenzi wake Sa'ad. Alipoifikia hatua ya kutubia kwa ajili ya matendo yake ya kale yaliyokuwa mabaya, anasema: "Nimearifiwa ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amenitishia, ambapo kile kitakiwacho kutoka kwake ni msamaha na maghfira." Na kisha anasema: "Mtume yu mshumaa uwakao, ambao chini ya mwanga wake watu hupata mwongozo moja kwa moja, naye yu 'upanga uliofutwa' wa Allah ambao daima ni wenye kushinda."

Huzuni Iliyochanganyika Na Furaha

Mwishoni mwa mwaka wa 8 Hijiriya, Mtume (s.a.w.w.) alimpoteza binti yake mkubwa Zaynab.5 Zaynab alikuwa kaolewa na mwana wa mama yake mkubwa (au mama yake mdogo) aliyeitwa Abul Aas, kabla

ya kuanza kwa Utume wa Mtume (s.a.w.w.), naye alikuwa akitangaza kumwanini kwake baba yake mara tu baada ya kuanza kwa Utume. Hata hivyo, mumewe aliendelea kuwa mshirikina na akashiriki kwenye vita vya Badr dhidi ya Uislamu na akatekwa.

Mtume (s.a.w.w.) alimwachilia kwa sharti la kwamba akamlete Zaynab Madina. Abul Aas aliitimiza ahadi yake na akampeleka Zaynab Madina lakini machifu wa Waquraishi walimtuma mtu mmoja aende akamrudishe, na mtu huyo alimrudisha Zaynab alipokuwa njiani akienda Madina. Yule mtu aliyetumwa alifaulu kufika karibu na kitundu cha ngamia aliyekuwa akisafiria Zaynab mle njiani na akauchoma mkuki wake kwenye kile kitundu alimokuwamo Zaynab.

Kutokana na hofu iliyokithiri, yule binti wa Mtume (s.a.w.w.) asiyekuwa na ulinzi aliharibu mimba mle njiani. Hata hivyo hakukata tamaa kuhusu kwenda Madina, na alifika kule katika hali ya ugonjwa. Aliitumia sehemu iliyosalia ya maisha yake akiwa yu mgonjwa na akafariki dunia mwishoni mwa mwaka wa 8 Hijiriya.

Huzuni ile iligeuka kuwa furaha, kwa sababu mwishoni mwa mwaka uleule Mtume (s.a.w.w.) alijaaliwa kupata mwana kutoka na Marya [mjakazi ambaye Muqawqis, mtawala wa Misri alimpa zawadi Mtume (s.a.w.w.)], naye akamwita mwana yule Ibrahim.

Wakati mkunga (Salma) alipompasha Mtume habari njema kwamba Allah kamjaalia mwana, alimpa bibi yule zawadi zenye thamani.
Katika siku ya saba, alitoa kafara ya kondoo ili kufanya '*Aqiqah*'6 ya mtoto yule, na akamnyoa nywele mtoto yule na akatoa sadaka ya fedha iliyokuwa na uzito sawa na zile nywele za mtoto, katika njia ya Allah.

---

1. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 500.
2. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk. 147.
3. Siratu Halabi, Jz. 3, uk. 242.
4. Kila ubeti unamalizikia na herufi ya Kiarabu ya Laam (Yaani L).
5. – Hii ni kwa yule anayedhani kuwa alikuwa ni binti yake wa kuzaa. lakini kilichothibiti kwetu ni kuwa hakuwa binti wake wa kuzaa bali wa kulea. –Mhariri–
6. Kuzinyoa nywele za kichwa za mtoto.

Sura Ya 52: Matukio Ya Mwaka Wa Tisa Hijiriya

Mwaka wa nane Hijiriya, pamoja na furaha na tabu zake zote ulimalizikia, na kile kituo kikuu cha ushirikina kiliangukia mikononi mwa Waislamu. Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alirejea Madina baada ya

kupata ushindi kamili, na nguvu ya kijeshi ya Uislamu ilienea Uarabuni kote. Makabila ya Waarabu wenye kuasi ambao kabla ya hapo, kamwe hayakupata kufikiria kwamba Uislamu utapata ushindi ule, sasa yakaanza kufikiria pole pole kwamba lazima wasogee karibu na Waislamu na kufuata dini yao. Kwa mtazamo huu, wawakilishi wa makabila mbalimbali ya Kiarabu na wakati mwingine makundi yao yakiongozwa na machifu wao, walipata heshima ya kufika mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na kuidhihirisha itikadi yao katika Uislamu. Katika mwaka wa 9 Hijiria, wawakilishi wengi wa makabila walikuja Madina kiasi kwamba mwaka ule ulianza kuitwa ni mwaka wa wawakilishi.

Safari moja kikundi cha watu wa kabila la Tayyi wakiongozwa na mtu mmoja aliyeitwa Zaydul Khayl kilikuja kuonana na Mtume (s.a.w.w.). Zayd alianza kuzungumza kama chifu wa kabila lile na Mtume (s.a.w.w.) alishangazwa na upole na hekima zake. Alisema kuhusu yeye: “Nimekutana na watu maarufu wa Uarabuni lakini nimewaona kuwa ni wenye sifa duni kuliko vile nilivyopata kusikia juu yao, lakini nimemwona Zayd kuwa yu bora zaidi ya vile atambulikavyo. Ingelikuwa bora kama angeliitwa Zaydul Khayr (Zayd mwema) badala ya Zaydul Khayl (Zaydu ngamia).”1

Kuvunjwa Kwa Hekalu La Masanamu

Lilikuwa ni jukumu kubwa zaidi na la kimsingi Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kuitangaza dini ya Upweke wa Allah na kuuondoa ushirikina kabisa kabisa. Hivyo basi, ili kuitengeneza hali ya watu wale waliopotoka na waabudu masanamu, mwanzoni kabisa aliitumia njia ya kuhoji na mantiki na kujaribu, kwa hoja zenye nguvu ili kuwafanya wauelewe upuuzi wa ushirikina. Hata hivyo, kama akiona kwamba hoja zake hazina athari yoyote kwao, nao wanaendelea kuwa wenye kiburi na wakaidi, alijiona kuwa anayo haki ya kutumia nguvu dhidi ya watu hawa wenye maradhi ya kiroho ambao hawakuweza kurekebishika hadi waweze kuzitumia akili zao.

Kama katika nyakati hizi kipindupindu kikilipuka kwenye sehemu ya nchi, na baadhi ya watu wanakataa kuchanjwa kutokana na ukosefu wa kuona mbali, Idara ya Afya ya Nchi ile hufikiria yenyewe kuwa inawajibika kuwachanja watu wale kwa nguvu ili kuhakikisha usalama wao na halikadhalika ule wa watu wengine kutokana na ugonjwa huu wa kuambukiza.

Mtukufu Mtume amejifundisha kutokana na mafundisho ya mbinguni kwamba ibada ya masanamu ni kama vijidudu vya kipindupindu. Vinaharibu maadili, ubora na tabia njema, na kumvuta mtu chini kutoka kwenye daraja la juu, humfanya kuwa duni hata zaidi ya mawe, udongo na viumbe vingine vilivyo duni. Hivyo aliteuliwa na Allah kuyaondoa maradhi ya ushirikina, kuzikomesha aina zote za ibada ya masanamu, na kutumia nguvu dhidi ya wale walioamka na kumpinga katika kuubalighisha ujumbe wa Allah.

Ubora wa kijeshi wa Uislamu ulimpa nafasi Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kutuma vikundi kwenye sehemu mbalimbali za Hijaz kwenda kuyavunja mahekalu ya masanamu na kutobakisha japo sanamu moja tu, kwenye eneo hili.

Mtume (s.a.w.w.) alipata taarifa mapema kwamba lilikuwepo sanamu kubwa miongoni mwa watu wa kabila la Tayyi na baadhi ya watu bado wangali wana imani juu ya sanamu lile.
Hivyo alimtuma Sayyidna Ali (a.s.), yule afisa wake mwenye hekima na mwenye uzoefu pamoja na askari wapanda wanyama mia moja kwenda kulibomoa hekalu la sanamu lile na kulivunja lile sanamu lenyewe.

Amirul–Mu'minin (a.s.) alipata kutambua kwamba kabila lile litapinga kile kitendo cha jeshi la Uislamu na jambo hili halitamalizika bila ya vita. Hivyo basi, asubuhi na mapema alianza kuishambulia ile sehemu lilipowekwa lile sanamu na akapata ushindi kamili katika kuitimiza kazi yake. Vile vile aliwakamata baadhi ya watu wa kundi lenye kupinga na kuwaleta mjini Madina wakiwa ni sehemu ya ngawira.

Adyy bin Haatim, ambaye baadaye alijiunga na safu za wapiganaji mashujaa wa Kiislamu na akaushika uchifu wa sehemu ile baada ya babu yake aliyekuwa na fikira tukufu Haatim, anasimulia kisa cha kukimbia kwake kwa maneno haya: "Kabla ya kusilimu kwangu, nilikuwa na uadui dhidi ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) kutokana na propaganda za kinyume zilizokuwa zikiendeshwa dhidi yake. Vilevile sikukosa kuutambua ushindi mkubwa nchini Hijaz na nilikuwa na uhakika kwamba siku moja mamlaka yake itafika kwenye eneo la Tayyi' pia, ambalo mimi nilikuwa mtawala wake.

Hata hivyo, kwa kuwa mimi sikutaka kuiacha dini yangu, na vilevile sikutaka kuwa mfungwa na kuangukia mikononi mwa Waislamu, nilimwamrisha mtumwa wangu kumweka ngamia mmoja tayari tayari kwa ajili ya kusafiri ili kwamba wakati wowote ule nikabiliwapo na hatari niondoke kwenda Sham kuepuka kukamatwa na Waislamu.

Ili nisije kukamatwa bila ya kujua niliweka doria kwenye sehemu mbalimbali za njia kuu, ili waweze kuniarifu wakati wowote waonapo vumbi litimuliwalo na msongo wa jeshi la Uislamu au watakapoiona dalili ya bendera zao.

Siku moja, mmoja wa watumwa wangu alikuja kwa ghafla na akanipa tahadhari na akaniarifu kuja kwa jeshi la Waislamu. Siku ile ile, mimi nikifuatana na mke na watoto wangu, tukatoka kwenda Sham, nchi iliyokuwa kituo kikuu cha Ukristo kule Mashariki. Dada yangu, binti yake Haatim alibakia na kabila lile na alikamatwa na Waislamu.

Baada ya dada yangu kupelekwa Madina, alifungiwa kwenye nyumba karibu na Masjidun–Nabi ambamo vile vile waliwekwa wale wafungwa wengine. Yeye amekieleza kisa chake hivi: "Siku moja wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akienda kusali mle msikitini, alipata bahati ya kupita karibu na ile nyumba walimowekwa wale wafungwa.

Niliitumia nafasi ile na nikiwa nimesimama upande wa pili wake nilimwambia: "Ewe Mtume wa Allah! Baba yangu amefariki dunia na mlezi wangu ametoweka. Basi nifanyie upendeleo fulani. Allah Atakufanyia upendeleo."

Mtume akaniuliza: "Ni nani aliyekuwa mlezi wako?" Nilimjibu nikasema: "Ni kaka yangu Adyy bin

Haatim.” Mtume akasema: “Je, yeye ndiye yule mtu aliyemkimbia Allah na Mtume Wake na akaenda Shamu?” Kisha akaelekea msikitini. Siku iliyofuatia, mazungumzo yale yale yalifanyika tena baina yangu na Mtume (s.a.w.w.) lakini mazungumzo hayo hayakuzaa matokeo. Siku ya tatu nilikuwa nimeyapoteza matumaini yoyote yale ya mazungumzo kama hayo na Mtume (s.a.w.w.) yenye kuthubutu kutokuwa na uwezo wa kuzaa matunda yoyote yale.

Hata hivyo, Mtume alipokuwa akipita kutoka kwenye sehemu ile ile, nilimwona mtu akija nyuma yake. Alinifanyia ishara niamke na niseme maneno yale yale niliyokuwa nikiyasema kwenye zile siku mbili zilizopita. Ile ishara aliyofanya yule mtu iliyahuisha matumaini yangu. Hivyo, nilisimama na nikayarudia yale maelezo niliyoyataja hapo juu mbele ya Mtume, kwa mara ya tatu. Alinijibu akisema: “Usifanye haraka kwenda. Nimeamua kukurejesha makwenu na mtu aaminikaye; lakini kwa wakati huu, matayarisho ya sarafi yako bado hayajakamilika.”

Dada yangu anasema kwamba, yule mtu aliyekuwa akimfuatia Mtume kwa nyuma na aliyenifanyia ishara kuyarudia yale maneno mbele ya Mtume, alikua ni Ali mwana wa Abu Talib.
Safari moja msafara uliokuwa na baadhi ya ndugu zetu, nao pia ulikuwa ukisafiri kutoka Madina kwenda Sham. Dada yangu alimwomba Mtume amruhusu kwenda Sham na msafara ule na kwenda kujiunga na kaka yake. Mtume alilikubali ombi lake na akaandaa mahitaji yote ya safari. Huko Shamu, mimi nilikuwa nimeketi karibu na dirisha la nyumba yangu. Mara kwa ghafla nikaona kwamba ngamia kasimama nyumbani kwangu.

Baada ya kutazama kwa makini, nilimwona dada yangu akiwa ameketi kwenye kitundu cha ngamia. Nilimshusha kutoka mle kitunduni na nikamwingiza nyumbani. Alianza kunilalamikia kuhusu kumwacha kule kwenye eneo la kabila la Tayyi’ na kushindwa kuja naye Sham.

Nilimchukulia dada yangu kuwa ni mwanamke mwenye hekima na akili. Siku moja nilizungumza naye juu ya Mtume na nikamuuliza: “Nini maoni yako juu yake?” Alijibu akisema: “Nimeona maadili yaliyo bora zaidi na sifa zilizo bora zaidi kwake, nami ninaona kwamba ni jambo lifaalo mno kufanya naye mapatano ya urafiki mapema iwezekanavyo.

Ninasema hivi kwa sababu, kama yeye ni Mtume wa Allah, ubora utakuwa ni wake yule amwaminiye mapema zaidi kuliko wengine, na kama akiwa mtawala wa kawaida, katu hutapata dhara lolote kutoka kwake na utafaidika kutokana na mamlaka aliyonayo.”

Adyy Bin Haatim Aenda Madina

Adyy anasema: “Maneno ya dada yangu yalinivutia mno kiasi kwamba niliuandaa moyo wangu juu ya kuelekea Madina. Nilipofika kule, nilikwenda moja kwa moja kumuona Mtume na nilimkuta mle msikitini. Niliketi karibu naye na kujitambulisha kwake. Mtume aliponitambua aliamka kutoka pale alipokuwa ameketi na akiwa ameushika mkono wangu, alinichukua nyumbani kwake. Tulipokuwa njiani, ajuza mmoja alikuja mbele yake na akazungumza naye maneno fulani.

Nilimwona akimsikiliza ajuza yule kwa makini na kumjibu. Tabia zake njema zilimvutia na nikasema moyoni mwangu: “Bila shaka mtu huyu si mtawala wa kawaida.” Tulipofika nyumbani kwake, maisha yake ya kawaida yalinivutia. Aliniwekea mkeka uliotengenezwa kwa nyuzi za mtende uliokuwamo nyumbani mle na akaniomba nikae. Mtu wa juu zaidi nchini Hijaz, aliyekuwa akiziogofya dola zote alikaa chini ardhini. Nilistaajabu mno kuyaona ya adabu zake na nilitambua kutokana na tabia zake njema maadili ya hali ya juu na heshima alizomtendea kila mtu, kwamba hakuwa mtu wa kawaida au aina ya mtawala wa nchi ya kawaida.

Wakati huo huo Mtume aliugeuzia uso wake kwangu na akayataja maelezo halisi ya maisha yangu na akasema: “Je, wewe hukuwa mfuasi wa dini ya Rakusi?”2 Nikajibu: “Ndio.” Kisha akaniuliza: “Kwa nini ulijitwalia robo ya mapato ya taifa lako peke yako? Je dini yako ilikuruhusu kufanya hivyo?” Nikajibu: “Hapana.” Kutokana na ujuzi wake wa ghaibu nilishawishika kuamini kwamba alitumwa na Allah.

Nilipokuwa bado ninafikiria hivyo, alizungumza nami kwa mara ya tatu, na akasema: “Umaskini na ufukara wa Waislamu usikuzuie kusilimu, kwa sababu iko siku inakuja ambayo utajiri wa ulimwengu utawatiririkia na hatakuwako wa kuukusanya na kuuweka.

Na kama nguvu ya kiidadi ya maadui na udogo mno wa idadi ya Waislamu unakuzuia kuipokea dini hii, mimi ninaapa kwa jina la Allah, siku ile inakuja ambapo kutokana na kushinda kwa Uislamu, idadi kubwa ya wanawake wa Kiislamu wasio na ulinzi watakuja kutoka Qaadisia kwa ajili ya Hija ya Ka’abah na hakuna yeyote atakayewaudhi.

Na kama leo hii utaona nguvu na mamlaka viko mikononi mwa watu wengine, nakuahidi kwamba itakuja siku ambayo majeshi ya Uislamu yatayakalia makasiri yenu yote haya na yataiteka Babylon.”

Adyy anaendelea kusema: “Niliishi na nikaona kwamba chini ya usalama uliotolewa na Uislamu, wanawake wasio na ulinzi walikuja kutoka sehemu za mbali, kuja kufanya Hija kwenye Ka’abah na hakuna yeyote aliyewaingilia katika shughuli zao. Vile vile niliona kwamba, nchi ya Babylon ilitekwa na Waislamu, walikikalia kiti cha enzi cha Kisra. Ninategemea kwamba nitaliona jambo la tatu; yaani utajiri wa ulimwengu utatiririka kuelekea Madina na hakuna atakayeelekea kuukusanya na kuuhifadhi.”3

---

1. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 577.
2. Dini ya ‘Rakusi’ ni dini iliyo baina ya Ukristo na Usabiya.
3. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 988 – 989; Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 578–581; Darajaatur Rafi’ah fi Tabaqaatish Shi’ah Imamiyah, uk. 352–354.

Sura Ya 53: Vita Vya Tabuk

Ile ngome ya kifahari na imara iliyojengwa kandoni mwa chemchemu kwenye barabara itokayo Hijr kwenda Damascus kwenye eneo la mpakani mwa nchi ya Shamu, iliitwa Tabuk. Katika siku zile Shamu ilikuwa moja ya makoloni ya Dola ya Rumi Mashariki (Ugiriki). Mji mkuu wa Dola ya Urumi ya Mashariki ulikuwa ni Constantinople.

Watu wa mipakani mwake walikuwa ni wafuasi wa dini ya Ukristo na machifu wa wilaya walikuwa vibaraka wa mtawala wa Shamu ambaye yeye mwenyewe alikuwa akipokea amri moja kwa moja kutoka kwa mfalme wa Urumi.

Kupenya na kuenea upesi upesi kwa Uislamu kwenye Rasi ya Uarabuni na utekaji wa haraka haraka uliokuwa ukifanywa na Waislamu nchini Hijaz kulikuwa kukionekana kwenye maeneo ya nje ya Hijaz na kulikuwa kukiwatetemesha maadui wao na kuwafanya wafikirie njia na jinsi ya kulikomesha wimbi hili.

Kuanguka kwa Serikali ya Makka, kusilimu kwa machifu wakuu wa Hijaz, ushujaa na kujitoa mhanga kwa wapiganaji wa Kiislamu kulimfanya mtawala wa Urumi kuamua kufanya mashambulio ya kushitukiza dhidi ya Uislamu kwa msaada wa jeshi lenye silaha za kutosha, kwa sababu alihisi kwamba dola yake ilikuwa kwenye hatari kuu kutokana na ushawishi usio kifani na kutanuka kwa Uislamu. Alikuwa akihofia mno kuongezeka kwa nguvu za kijeshi na kisiasa kwa Waislamu.

Katika siku zile, Urumi ilikuwa adui pekee wa Iran na alikuwa anayo nguvu kubwa zaidi ya kisiasa na kijeshi. Ilikuwa ikijivuna sana kutokana na ushindi wa mara kwa mara iliokuwa ikiupata dhidi ya Iran na kushindwa ambako ilikusababisha katika jeshi la Iran.

Jeshi la Urumi lililokuwa na askari 4000 wapanda wanyama na watembeao kwa miguu na walikuwa na silaha za muundo mpya kabisa zilizopatikana kwenye zama zile, walipiga kambi kwenye ukanda wa mpakani mwa Shamu. Makabila yaliyokuwa yakiishi kwenye maeneo ya mpakani (kama vile makabila ya Lakham, Aamilah, Ghassan na Jazaam) nayo yalijiunga nao, na watangulizi wa jeshi lile wakaenda hadi Balqaa.1

Taarifa za kupiga kambi kwa kundi la askari wa Kirumi kwenye ukanda wa mpakani mwa Shamu zilimfikia Mtume (s.a.w.w.) kupitia misafara iliyokuwa ikisafiri baina ya Hijaz na Shamu kuhusiana na biashara. Hakupata njia yoyote nyingine ila kuwajibu washambuliaji kwa jeshi kubwa na kuihami dhidi ya shambulio la kuotea, ile dini iliyokwisha kuenea kwa gharama ya uhai wa watu wapenzi katika Uislamu, na kujitoa mhanga kwake binafsi, na sasa imeshaimarisha mizizi yake, nayo ilikuwa karibuni ienee ulimwenguni kote.

Taarifa hizi zisizopendeza zilimfikia Mtume wakati watu wa Madina walipokuwa bado hawajayavuna mavuno yao yote, na tende zilikuwa karibu kuiva, na Madina na viungani mwake kusema kweli, ilikuwa

kwenye makucha ya namna ya njaa. Hata hivyo, kwa watu wachamungu, maisha ya kiroho na ulinzi wa maadili matukufu na Jihad katika njia ya Allah yana kipaupembele zaidi kuliko kitu chochote kingine.

Kuwaita Mashujaa Na Upatikanaji Wa Gharama Za Vita

Kwa kiasi fulani Mtume (s.a.w.w.) alitambua uwezo na uzoefu wa jeshi la adui na alikuwa na uhakika kwamba ukiachilia mbali kule kuhitajia rasilimali ya kiroho (nayo ni imani juu ya Allah, na kupigana kwa ajili ya Allah) ushindi katika vita hivi pia ulitegemea kuwa na jeshi kubwa. Akilizingatia jambo hili aliwatuma watu kwenda Makka pamoja na maeneo yenye kuuzunguka mji ule wa Madina kwenda kuwaita Waislamu watoke na kupigana katika njia ya Allah na kuwaomba Waislamu wenye uwezo kugharimia gharama za vita kwa kutoa Zaka.

Mara tu baada ya tangazo la Mtume (s.a.w.w.) watu 30,000 walitangaza kuwa tayari kwao kushiriki katika vita na kujikusanya kwenye kiwanja cha kupigia kambi cha mji wa Madina (Thaniyyatul Widaa). Gharama za vita zilitolewa kwa kukusanya Zaka. Kati ya hawa watu 30,000, watu 10,000 walikuwa ni askari wapanda wanyama, na wale askari 20,000 waliobakia walikuwa askari waendao kwa miguu. Baadae Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha kwamba kila kabila lijichagulie bendera yake.2

Watu Waliokataa Kushiriki Kwenye Vita

Vita vya Tabuk vilikuwa fursa nzuri zaidi ambamo ndani yake watu wenye kujitoa mhanga na watu wadanganyifu wanaojionyesha tu na wanafiki waliweza kutambulika, kwa sababu kuondoka kwa askari wote kuliamrishwa wakati wa hali ya hewa ilipokuwa na joto sana, na jamii ya kibiashara ya mji wa Madina ilikuwa tayari kuanza kuvuna tende.

Kukataa kwa baadhi yao kushiriki kwenye vita vile kwa kutoa nyudhuru mbalimbali kunalitoa pazia kutoka kwenye nyuso zao halisi, na aya za Qur'ani Tukufu zilifunuliwa zikikilaumu kitendo chao kile. Aya zote hizi zimo kwenye *Surat al-Tawbah*. Baadhi ya watu walikataa kushiriki kwenye hii Jihad takatifu kwa sababu zifuatazo:

Mtume (s.a.w.w.) alipompendekeza Jadd bin Qays, aliyekuwa mtu mwenye mvuto kwa watu ajiunge na jeshi dhidi ya Warumi, alijibu akisema: "Mimi nina upendo wa kishabiki mkali sana kwa wanawake. Hivyo basi mimi ninachelea kwamba ninaweza nikawaona wanawake wa Kirumi na nikashindwa kujitawala." Mtume (s.a.w.w.) alipousikia udhuru wake huu wa kitoto, aliamua kumwacha na kuwasiliana na watu wengine juu ya jambo hili. Jadd alilaumiwa na Allah kwenye Aya hii:

وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ ائْذَنْ لِي وَلَا تَفْتِنِّي ۚ أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا ۗ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ {49}

“Na miongoni mwao wapo wanaosema: Niruhusu wala usinitie katika fitina. Kwa yakini wao hivyo wamekwisha tumbukia katika fitina. Na hakika Jahannamu imewazunguka.”
(***Sura al-Tawbah, 9:49***)

Wanafiki: Wale watu waliowatishia Waislamu katika kushiriki kwenye vita vile, na wakasema: “Waarabu hawana uwezo wa kupigana na Warumi na matokeo yake yatakuwa kwamba wale wote watakaoshiriki kwenye vita vile watafungwa kamba na kuuzwa masokoni.3

Kugunduliwa Kwa Kituo Cha Wapanga Makri Mjini Madina:

Yule kiongozi mkuu wa Uislamu (s.a.w.w.) alizipa umuhimu mkubwa taarifa za kijasusi, na nusu ya ushindi wake ulikuwa ni matokeo ya taarifa alizozipata kabla juu ya hali ya maadui na waeneza fitna. Kwa njia hii aliweza kuyakomesha mengi ya matendo yao ya kishetani na mipango iliyo dhidi ya Uislamu tangu mwanzoni kabisa.

Mtume (s.a.w.w.) alipokea taarifa kwamba nyumba ya Myahudi mmoja aliyeitwa Suwaylam imekuwa kituo cha matendo yaliyo kinyume na Uislamu na wanafiki wanakusanyika hapo na kupanga mipango miovu ya kuwazuia Waislamu wasishiriki kwenye hii Jihad takatifu. Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kuwatisha wale wapanga makri katika hali ambayo hawatarudia tena kuwa na fikra za kishetani hapo baadae.

Alimwamrisha Talhah bin Ubaydullah kwenda na baadhi ya masahaba shujaa na kuichoma nyumba ya Suwaylam wakati walipokuwa wakiendesha mkutano wao humo. Kama alivyoelekezwa na Mtume (s.a.ww), Talha aliichoma nyumba ile wakati wapanga makri walipokuwa wakijishughulisha na kuujadili mpango uliokuwa kinyume na Uislamu. Wote wakaikimbia miali ya moto na mmoja wao alijeruhiwa mguu wake. Kitendo hiki kilikuwa na athari mno kiasi kwamba kiliweza kutoa funzo kwa wanafiki kwa siku zijazo.4

Kikundi Cha Watu Waliolia Na Kutoa Machozi:

Baadhi ya masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) ambao walikuwa na shauku kubwa ya kushiriki kwenye hii Jihad takatifu walikuja na kumwomba Mtume (s.a.w.w.) awapatie mahitaji ya safari ile ili waweze kutoa huduma ile takatifu ya kidini. Mtume (s.a.w.w.) alipowaambia kwamba hakuwa na mnyama yoyote wa kupanda ambaye angeliweza kuwapa, walilia sana sana na machozi yalitiririka nyusoni mwao.

Kama walikuwako baadhi ya watu miongoni mwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) waliopanga makri au waliojishughulisha na vizuizi au kutunga nyudhuru, vilevile walikuwepo wengine miongoni mwao waliokuwa na shauku ya kushiriki kwenye Jihad, ambayo wakati mwingine huwa na gharama ya uhai wa mtu, na kutoshiriki ndani yake kunawafanya walie sana. Kwa mujibu wa istilahi za kihistoria watu hawa wanaitwa ‘wenye kulia’ na Qur’ani Tukufu inataja imani yao kwa maneno haya:

وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَا أَجِدُ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّوْا وَأَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلَّا يَجِدُوا مَا يُنْفِقُونَ {92}

"Wala wale waliokujia ili uwachukue ukasema: Sina kipando cha kukuchukueni. Tena wakarudi na macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kukosa cha kutoa."
(***Sura al-Tawbah, 9:92***).5

Kundi lingine lilikuwa na watu kama vile Ka'ab, Hilal, na Mararah waliokuwa na imani kamili juu ya Uislamu na vilevile walikuwa na shauku kubwa ya kushiriki katika Jihad, lakini kwa kuwa walikuwa bado hawajavuna mazao yao, waliamua kwamba baada ya kuvuna mazao yao watajiunga na mashujaa wa Uislamu. Katika istilahi ya Qur'ani Tukufu (tazama *Surat-Tawbah,* 9:118) wao ndio wale wenye kuruka mipaka watatu waliokaripiwa vikali mno na Mtume (s.a.ww) aliporejea kutoka Tabuk na lile karipio walilopata, vilevile lilikuwa mfano kwa wengine.

Sayidna Ali (A.S.) Hakushiriki Kwenye Vita Hivi

Moja ya sifa za Amirul-Mu'minin (a.s.) ni kwamba yeye alifuatana na Mtume (s.a.w.w.) na alikuwa mshika bendera wake kwenye vita vyote vya Kiislamu ila kwenye vita vya Tabuk. Yeye alibakia mjini Madina naye hakushiriki kwenye Jihad hii kwa amri ya Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe.

Mtume (s.a.w.w.) aliuchukua uamuzi huu kwa kuwa alitambua vizuri kwamba, wanafiki na baadhi ya watu kutoka miongoni mwa Waquraishi walikuwa wakiitafuta fursa ya kuleta ghasia na kuipindua ile serikali mpya ya Kiislamu pindi Mtume (s.a.w.w.) atakapokuwa hayupo. Tabuk ilikuwa sehemu ya mbali zaidi aliyoifika Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na vile vita alivyoshiriki.

Alitambua kikamilifu kwamba, ingeliwezekana kwamba wakati akiwa hayupo, vikundi vipingavyo Uislamu vingelifanya ghasia na vingeliwaita washirika wao kutoka sehemu mbalimbali na kuwaunga mkono kwa ajili ya kupata ushindi kwenye mpango wao mwovu.

Hivyo basi, ingawa alimteua Muhammad bin Maslamah kuwa mwakilishi wake mjini Madina wakati wa kuondoka kwake, vile vile alimwambia Sayyidna Ali (a.s.): "Wewe ni mlezi wa Ahlul Bayt na ndugu zangu na kundi la Muhajiriin, na hakuna yeyote mwingine afaaye kwa jukumu hili ila mimi mwenyewe na wewe."

Kubakia kwa Amirul-Mu'minin mle mjini Madina kuliwaudhi mno wale wapanga makri, kwa sababu walitambua kwamba hawataweza kuutekeleza mpango wao mbele ya Sayyidna Ali (a.s.) ambaye daima alikuwa mwangalifu.

Hivyo basi ili kuthibitisha kwamba Sayyidna Ali (a.s.) anaondoka mjini Madina, waliamua kuunda mpango mwingine na wakaeneza uvumi kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimtaka Ali ashiriki kwenye Jihad

lakini Ali alikataa kushiriki kwenye vita hivi takatifu kutokana na safari ndefu na hali ya hewa yenye joto kali.

Ili kuwapinga watu hawa, Sayyidna Ali (a.s.) alimuona Mtume (s.a.w.w.) (nje ya kidogo ya mji wa Madina ambapo Mtume alipiga kambi ili kusubiri jeshi lote likamilike) na akaliweka suala lile mbele ya Mtume (s.a.w.w.). Wakati ule Mtume (s.a.w.w.) aliitamka ile kauli yake ya kihistoria ambayo ni uthibitisho wa dhahiri wa Uimamu wa Sayyidna Ali (a.s.) na Ukhalifa wake wa mara tu baada ya kufariki dunia Mtume (s.a.w.w.).

Alisema: “Ewe Ndugu yangu! Rejea Madina, kwa kuwa hakuna afaaye zaidi kuuhifadhi utukufu na cheo cha mji wa Madina zaidi yangu mimi mwenyewe na wewe. Wewe ni mwakilishi wangu miongoni mwa Ahlul Bayt na ndugu zangu. Je, wewe hufurahi ninapokwambia kwamba uhusiano wako na mimi ni sawa na ule uliokuwepo baina ya Harun na Musa, ila tu kwamba hatakuja Mtume baada yangu? Kama vile alivyokuwa Harun kwamba alikuwa mrithi wa papo kwa papo wa Nabii Musa, wewe nawe ni mrithi na Khalifa wangu. “6

Jeshi La Uislamu Laelekea Tabuk

Desturi ya Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa kwamba anaposafiri kwenda kuwaadhibu watu waliokinza kuendelea kwa Uislamu, au waliodhamiria kuwashambulia Waislamu, au waliokuwa na mipango miovu dhidi yao, hakuidhihirisha nia na madhumuni yake kwa maafisa askari wake na alilifanya jeshi lipitie njia isiyopitiwa mara kwa mara.

Hivyo, hakuwaruhusu maadui wayatambue malengo yake na akawajia maadui wakiwa wao wenyewe hawatambui.7 Hata hivyo, ili kuwafukuzilia mbali majeshi ya kirumi yaliyokusanyika kwenye mpaka wa Shamu kwa lengo la kuzishambulia nchi za Kiislamu, alilifanya lengo lake lieleweke dhahiri kwa wale wote wahusikao, siku ileile ambayo ukusanyaji wa majeshi ulipotangazwa.

Madhumuni ya kufanya hivyo yalikuwa kwamba wale Mujahidiin (mashujaa) watambue umuhimu wa safari ile na taabu zipasazo kukabiliwa mle njiani, na ili waweze kuchukua masurufu yatoshelezayo. Aidha, ili kuliimarisha jeshi la Uislamu, Mtume (s.a.w.w.) alilazimika kuomba msaada kutoka kwa watu wa makabila ya Tamim, GhatfAn na Tayyi, hawa walikuwa wakiishi kwenye sehemu za mbali kutoka Madina. Kwa sababu hii Mtume (s.a.w.w.) aliandika barua kwa machifu wa makabila haya na vilevile alimwandikia barua ‘Ataab bin Usayd, yule Gavana kijana wa Makka, na kuyaita makabila pamoja na watu wa Makka washiriki kwenye Jihad hii takatifu.8

Kwa kuwa upanuzi wa ule mwito wa watu wote haukuweza kuwa siri. Hivyo ilikuwa muhimu kwamba, aweze kuyafanya mahitaji ya safari kabisa kwa wale machifu wa makabila ili waweze kutayarisha masurufu yatoshelezayo na wanyama wa kupanda kwa ajili ya Mujahidiin wao.

Jeshi Lafanya Gwaride Mbele Ya Mtume (S.A.W.W)

Siku ya kuondoka kwa jeshi la Waislamu ikafika. Siku ile Mtume (s.a.w.w.) alivikagua vikosi kwenye makao makuu ya jeshi ya mjini Madina. Mandhari kubwa mno ya gwaride lile lililokuwa likifanywa na watu waaminifu na wenye kujitoa mhanga ambao ili kuyafikia malengo yao, wamechagua kupata taabu na kifo badala ya starehe na faida za kidunia, kwa shauku na imani iliwavutia waliokuwapo pale.

Wakati wa kuondoka, Mtume (s.a.w.w.) aliwahutubia askari ili kuziimarisha nyoyo zao, na kuwaeleza lengo lake katika kule kuamrisha watu wote kwenda vitani, kisha askari waliendelea wakielekea kwenye njia iliyoainishwa.

Kisa Cha Malik Bin Qays

Baada ya kuondoka kwa jeshi, Maliki bin Qays alirejea Madina kutoka kwenye safari yake. Hali ya hewa ilikuwa ya joto kali mno siku ile. Aliona kwamba upweke ulitawala kila mahali mle mjini Madina na akapata kutambua kuhusu kule kuondoka kwa askari wa Uislamu. Wakati ule ule, aliwasili kwenye bustani yake na akaona kwamba mkewe mzuri amemjengea kibanda.

Aliutupia jicho uso wenye kuvutia wa mkewe na vilevile akakikodolea macho kidogo chakula na maji alichokitayarisha yule mwanamke kwa ajili yake. Baada ya hapo aliyafikiria matatizo machungu ya Mtume (s.a.w.w.) na masahaba wake waliokuwa wakienda kufanya Jihad katika njia ya Allah na kukikabili kifo katika hali ya hewa ya joto kiasi kile.

Kisha akaamua kutokutumia yale maji na kile chakula alichokitayarisha mkewe wala kile kibanda alichokijenga mkewe, bali kumpanda mnyama wake upesi sana, na kwenda kujiunga na jeshi la Uislamu upesi iwezekanavyo. Hivyo, upesi sana alimgeukia mkewe na kumwambia:

“Si sahihi hata kidogo kwamba mimi nipumzike chini ya kivuli cha kibanda hiki pamoja na mke wangu na kula chakula kitamu, na kunywa maji yaliyopoa na matamu, ambapo bwana wangu anakwenda kwenye Jihad katika joto kali kiasi hiki. Hapana jambo hili haliafikiani na uadilifu na kanuni za urafiki, na imani na uaminifu haviniruhusu kufanya hivi.”

Aliyasema maneno haya akaokota masurufu machache hivi kwa ajili ya ile safari na akaenda zake. Alipokuwa njiani alikutana na ‘Umar bin Wahab, ambaye yaonekana alikawia nyuma ya lile jeshi la Uislamu, na wote wawili wakamkuta Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa Tabuk.9

Mtu huyu hakuzipata baraka za kufuatana na Mtume (s.a.w.w.) pale mwanzoni, lakini hatimaye alizitoa huduma zake katika njia hii tukufu kwa njia ya kujitoa mhanga kwake. Kwa upande mwingine, wako watu ambao mlangoni pao bahati njema inabisha hodi, lakini wanakaa mbali nayo kwa kisingizio cha ukosefu wa kufaa na ufanisi na hatimaye wakajitupa wenyewe kwenye uadui na maangamizi. Kwa mfano, Abdullah bin Ubayy, chifu wa wanafiki, alikita hema kwenye sehemu ya kambi ya Mtume (s.a.w.w.) ili

kwamba aweze kushiriki kwenye Jihad hii akifuatana na Mtume (s.a.w.w.).

Kwa vile alikuwa adui katili wa Uislam, alibadilisha mawazo wakati jeshi lilipokuwa tayari kuondoka na akarejea Madina pamoja na watu waliokuwa wakimuunga mkono ili aweze kufanya ghasia pale wakati Mtume (s.a.w.w.) akiwa hayupo. Mtume (s.a.w.w.) hakumjali hata kidogo, kwa sababu aliutambua unafiki wake na hakudhania kushiriki kwake kwenye Jihadi ile kuwa na faida yoyote ile.

Tabu Za Njiani

Jeshi la Uislamu lilikabiliwa na matatizo makubwa lilipokuwa njiani kutoka Madina kwenda Shamu na ni kwa sababu hii kwamba lilipewa jina la *Jayshul usrah* (Jeshi la Tabu). Hata hivyo, imani na juhudi viliyashinda matatizo yote hayo nao waliyakaribisha matatizo yote yaliyo wakabili.

Lile jeshi la Uislamu lilipoifikia nchi ya Wathamud Mtume (s.a.w.w.) aliufunika uso wake kwa nguo kwa sababu ya upepo wenye joto lichomalo na uvumao sana na akaipita sehemu ile kwa haraka sana na akawaambia masahaba zake: “Utazameni mwishilizo wa uhai wa Wathamud waliopasika na ghadhabu ya Allah kutokana na ukaidi na uasi wao; na kumbukeni kwamba hakuna muumini wa kweli ambaye angelifikiria kwamba mwishilizio wa uhai wake hautakuwa kama wa watu wale. Utulivu mzito kama wa kifo wa sehemu hii, na magofu ya nyumba zilizoharibiwa ambayo yameangukiwa na kimya kizito ni funzo kwa umati nyingine.”

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha askari wale wasinywe maji ya sehemu ile au kutayarisha chakula au mkate kutokana nayo, na kwamba wasijaribu hata kufanya udhuu nayo, na kama kwa bahati mbaya walishatayarisha chakula au kukanda unga kwa maji yale basi wawape wanyama wale chakula hicho.

Kisha lile jeshi la Uislamu liliendelea na safari likiwa chini ya uongozi wa Mtume (s.a.w.w.) na ilipopita sehemu ya usiku, walikifikia kisima ambacho Ngamia wa Nabii Swaleh alinywea maji. Walipoifikia sehemu ile, Mtume (s.a.w.w.) alitoa amri ya kwamba watu wote wapige kambi pale na kupumzika.

Amri Za Tahadhari

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiitambua vizuri sumu ya upepo uvumao kwa nguvu na kimbunga kikali cha eneo lile, ambacho wakati mwingine huwazidi watu na ngamia na kuwafukia chini. Hivyo basi, aliamrisha kwamba magoti ya ngamia yafungwe na mtu yeyote yule asitoke eneo la kambi wakati wa usiku akiwa yu peke yake.

Uzoefu ulithibitisha kwamba ile amri ya tahadhari aliyoitoa Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa na faida kubwa, kwa sababu watu wawili wa kabila la Bani Saidah waliikiuka amri hii na wakalitoka eneo la kambi wakiwa peke yao wakati wa usiku, na matokeo yake yakawa kwamba ile dhoruba kali ilimkosesha hewa mmoja wao na kumvurumisha mwingine kwenye kilima. Mtume (s.a.w.w.) alipata habari za matukio haya, naye

aliwahuzunikia sana wale watu waliopoteza maisha yao kutokana na utovu wa nidhamu. Hivyo basi, aliwaomba tena wale askari kudumisha nidhamu. 10

Abbad bin Bishr, aliyekiongoza kikosi kilichohusika na usalama na ulinzi wa jeshi la Uislamu, alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kwamba askari wa Uislamu wameingia kwenye matatizo kutokana na upungufu wa maji, na hifadhi yote ya maji yaelekea kumalizika hivi karibuni. Hivyo baadhi yao waliwachinja ngamia wao wa thamani mno ili kuweza kuyatumia maji yaliyokuwamo matumboni mwao, na wengine walijiweka kwenye mapenzi ya Allah, nao walikuwa wakisubiri kwa hamu kubwa rehma za Allah.

Allah Mwenye nguvu zote ambaye amemwahidi ushindi Mtume Wake, alimsaidia tena yeye na masahaba wake waaminifu. Mvua kubwa ilinyesha na wote wakapata maji ya kunywa yenye kuwatosheleza. Zaidi ya hapo, wale walioteuliwa kuhifadhi vyakula, pamoja na jeshi zima waliweza kuhifadhi maji kiasi walichohitaji.

Habari Za Ghaibu Za Mtume (S.A.W.W)

Haukaniki ukweli uliopo kwamba, kama inavyoelezwa dhahiri kwenye Qur'ani Tukufu,11 Mtume (s.a.w.w.) aliweza kutoa taarifa juu ya mambo ya ghaibu ambayo watu wengine hawakuwa wakijua chochote. Hata hivyo, elimu ya Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa na kikomo, na ilitegemea kile alichofunzwa na Allah. Hivyo basi, iliwezekana kwamba asitambue mambo fulani fulani. Kwa mfano, aliweza kupoteza pesa au kupoteza funguo ya nyumba na akashindwa kuiona. Hata hivyo, wakati fulani aliweza kutoa taarifa za ghaifu juu ya mambo yaliyokuwa ya siri zaidi na yaliyotatanisha zaidi na kuwaacha watu wakiwa wanashangaa. Sababu ya kupanda na kushuka huku ni ile tuliyoitaja hapo juu. Yaani kila Allah alipopenda alimpa Mtume taarifa za mambo yahusianayo na ulimwengu wa ghaibu.

Wakati jeshi lilipokuwa njiani ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) alipotea na baadhi ya masahaba walikwenda kumtafuta. Wakati huo huo mmoja wa wanafiki aliamka na kusema: "Anasema kwamba yu Mtume wa Allah na anatoa taarifa juu ya mbingu, lakini inashangaza kwamba hajui aliko ngamia wake!" Mtume (s.a.w.w.) akapata kulitambua jambo hili na akaifafanua hali ile kwa njia ya kauli fasaha. Alisema: "Ninajua tu yale aniambiayo Allah. Hivi karibuni tu Allah ameniarifu aliko ngamia wangu. Yuko jangwani kwenye bonde hili na hili. Hatamu yake imejifunga kwenye mti na kumzuia kutembea. Nendeni mkamlete."

Watu fulani walikwenda upesi upesi kwenye sehemu ile na wakamwona yule ngamia akiwa kwenye hali ile aliyoieleza Mtume (s.a.w.w.).12

Taarifa Nyingine Ya Siri

Ngamia wa Abu Dharr alishindwa kutembea na hivyo Abu Dharr aliachwa nyuma na lile jeshi la Kiislamu. Alisubiri kwa muda fulani lakini hakupata matokeo yoyote. Hatimaye alimwacha yule ngamia na akakibeba chakula mgongoni mwake na akaanza kutembea ili aende akajiunge na lile jeshi la

Uislamu mapema iwezekanavyo. Wale askari wa Uislamu walikuwa wamepiga kambi mahali fulani kama walivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) nao walikuwa wakipumzika.

Mara kwa ghafla waliliona kwa mbali umbo la mtu aliyekuwa akipita njia ile na mzigo mzito mgongoni mwake. Sahaba mmoja alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) hali ile. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Huyo ni Abu Dharr. Allah amsamehe Abu Dhar! Anatembea peke yake, atakufa peke yake na atafufuliwa peke yake.”13
Matukio ya baadae yalithibitisha kwamba alivyotabiri Mtume (s.a.w.w.) vilikuwa sahihi kabisa; kwa sababu Abu Dharr alifariki katika hali ya kuhuzunisha, mbali kutoka kwenye makazi ya watu, kwenye jangwa la Rabzah akiwa peke yake na binti yake tu akiwa karibu naye.14

Jeshi La Uislamu Lawasili Kwenye Eneo La Tabuk

Jeshi la Uislamu lilifika kwenye eneo la Tabuk mwanzoni mwa mwezi wa Sha’aban, mwaka wa 9 Hijiriya. Hata hivyo, hakuna dalili ya jeshi la Kirumi iliyoweza kuonekana pale. Inaonekana kwamba wale makamanda wa jeshi la Warumi waliutambua ukubwa wa jeshi la Waislamu na ujasiri wao na kujitoa mhanga kwao kusiko na kifani, ambako mfano wake mdogo tayari wameshauona kwa karibu zaidi katika Vita vya Muuta, hivyo waliona kwamba inafaa kulirudisha tena jeshi lao katika mipaka ya nchi yao wenyewe. Kwa kufanya hivyo, walitaka kukana kivitendo kwamba walipeleka majeshi dhidi ya Waislamu, na walitaka kutoa dhana ya kwamba katu hawakupata kufikiria kuanzisha mashambulizi, na taarifa zozote za aina hiyo ni dhana tu, na kwa kufanya hivyo walitaka kuthibitisha kutopendelea kwao matukio yaliyokuwa yakitokea Uarabuni.

Katika hali hii, Mtume (s.a.w.w.) aliwakusanya maafisa wake watukufu na akiutekeleza msingi uliodumishwa wa Uislamu, ule wa kushauriana, aliwataka ushauri kama waendelee na kuingia kwenye nchi ya adui au warejee Madina. Matokeo ya ule ushauriano wa kijeshi ni kwamba, iliamuliwa kwamba lile jeshi la Uislamu lilipata taabu nyingi sana lilipokuwa likisafiri kuja pale Tabuk, hivyo lirudi Madina kwenda kuihuisha nguvu yake. Aidha, kwa kuifanya safari ile, Waislamu watakuwa wamekwisha kulifikia lengo lao kuu ambalo lilikuwa ni kulitawanya jeshi la kirumi.

Warumi walitishwa mno na kuogopa, kiasi kwamba kwa kipindi kirefu sana hawakufikiria kuwashambulia Waislamu, na hivyo basi kwenye kipindi kile usalama wa Uarabuni kutoka kwenye upande wa Kaskazini ulipatikana.

Ili kukilinda salama cheo cha Mtume (s.a.w.w.) na kudhihirisha kwamba maoni yao yangeliweza kukataliwa au kuondolewa; wanakamati wa halmashauri ya ushauriano wa kijeshi, vile vile waliongezea sentensi ifuatayo: “Kama umeamrishwa na Allah Mwenye nguvu zote kuendelea, basi tuamrishe, sisi nasi tutakufuata.”15

Mtume (s.a.w) akasema: “Hakuna amri yoyote iliyofunuliwa kutoka kwa Allah, na kama amri ingelipokelewa kutoka Kwake, nisengelikutakeni ushauri. Hivyo basi, kutokana na heshima ya

halmashauri ya ushauri, nimeamua kurejea Madina kutoka mahali hapa.”

Watawala walioyakalia maeneo ya mipakani mwa Shamu na Hijaz na ushawishi uliloungana miongoni mwa watu wao, wote walikuwa Wakristo na ulikuweko uwezekano kwamba siku moja jeshi la Warumi lingeliweza kuwatumia hawa watawala wa kienyeji na kuishambulia Hijaz kwa msaada wao. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kwa Mtume (s.a.w.w.) kufanya mikataba ya kutoshambuliana na watawala hawa ili aweze kujipatia usalama mzuri zaidi.

Yeye mwenyewe aliwasiliana na watawala hawa wa mipakani waliokuwa wakiishi kwenye maeneo ya jirani na Tabuk, na kufanya nao mikataba ya kutoshambuliana kwa masharti fulani fulani. Ama kuhusu maeneo yaliyoko mbali kutoka Tabuk alipeleka wawakilishi wake kwa watawala wahusika ili usalama ulio bora zaidi uweze kupatikana kwa ajili ya Uislamu.

Vilevile aliwasiliana na mtawala wa Aylah, Azri’aat na Jarbaa’ na mapatano ya kutoshambuliana yalifanyika baina ya vikundi hivi. Aylah ni mji wa pwani uliokuwako kwenye pwani ya Bahari ya Shamu na uko umbali fulani kutoka Shamu.
Mtawala wake aliitwa Yohana mwana wa Rawbah, alikuja kutoka kwenye mji wake mkuu hadi pale Tabuk akiwa amevaa msalaba wa dhahabu shingoni mwake. Alimpa Mtume (s.a.w.w.) zawadi ya nyumbu mweupe na akadhihirisha utii wake kwake. Mtume (s.a.w.w.) alipendezewa na ishara yake ya urafiki na vilevile yeye naye alimpa zawadi.

Yule mtawala aliamua kubakia kwenye dini ya Ukristo na kulipa *Jizayh* (kodi) ya dinari elfu tatu kila mwaka na vilevile kumpokea kila Mwislamu apitaye kwenye eneo lile la Aylah. Ulifanyika mkataba wenye masharti yafuatayo na ukasainiwa na pande zote mbili: “Huu ni mkataba wa kutoshambuliana kutoka kwenye upande wa Allah na Mtume Wake, Muhammad kwa ajili ya Yohana na wakazi wa Aylah. Kufuatana na mkataba huu njia zao zote za usafiri, iwe ni kwa bahari au kwa nchi kavu, na watu wote wa Shamu, Yaman na visiwa, yeyote yule awaye pamoja nao atakuwa kwenye hifadhi ya Allah na Mtume Wake. Hata hivyo, kama yeyote miongoni mwao atazikiuka sheria, basi utajiri wake hautamwokoa kutokana na adhabu. Njia zote za bahari na za nchi kavu zitakuwa wazi kwa ajili yao nao wanayo haki ya kuzipita.”16

Mkataba huu waonyesha kwamba kama taifa fulani lilishirikiana na Waislamu kwa njia ya amani, lilipewa njia za kulifanikisha jambo hilo, na vilevile lilithibitishiwa usalama wake.

Vile vile Mtume (s.a.w.w.) alifanya mikataba na watu wa mipakani kama vile watu wa Azri’aat, na Jarbaa’ ambao nchi zao zilikuwa na umuhimu mkubwa wa kimikakati, na hivyo kuthibitisha kuwapo kwa usalama wa nchi za Kiislamu kutoka kwenye ule upande wa Kaskazini.

Khalid Bin Walid Apelekwa Duwmatul Jandal

Ukanda wenye watu wengi na miti ya kijani, maji yatiririkayo na ngome madhubuti iliyokuwa kiasi cha ligi

50 (kilometa 240) kutoka Shamu ulikuwa ukiitwa Duwmatul Jandal.17 Katika siku zile Mkristo mmoja aliyeitwa Okaydar bin Abdil Malik Kindi alitawala hapo. Mtume (s.a.w.w.) alichelea kwamba katika hali ya jeshi la Kirumi kuanzisha tena mashambulizi, yule mtawala wa Duwmatul Jandal angeliweza kuwasaidia na hivyo kuuhatarisha usalama wa Uarabuni.

Kwa sababu hii aliona kwamba ni muhimu kupata faida kiasi iwezekanavyo kutokana na jeshi alilonalo, na kukipeleka kikosi chini ya uamiri jeshi wa Khalid bin Walid kwenda kutisha watu wa ukanda huo tulioitaja. Khalid alifika karibu na Duwmatul Jandal akifuatana na askari wapanda wanyama na akaiotea ile ngome.

Katika usiku wa mbalamwezi Okaydar alitoka nje ya ngome ile akifuatana na nduguye aliyeitwa Hassan wakienda kuwinda. Walikuwa bado hawajakwenda mbali sana kutoka kwenye ile ngome pale walipokutana uso kwa uso na wale askari wa Khalid. Katika mapambano madogo tu yaliyotokea baina ya hivyo vikundi viwili, nduguye Okaydar aliuwawa, na watu wake wakakimbilia mle ngomeni na wakalifunga lango la ile ngome, na Okaydar akakamatwa.

Khalid alimwahidi kwamba kama wale wakazi wa ile ngome wakilifungua lango lake kwa amri yake na kuzisalimisha silaha zao kwenye jeshi la Uislamu atamsamehe na atampeleka kwa Mtume (s.a.w.w.).

Okaydar alitambua kwamba Waislamu walikuwa wakweli na walizitimiza ahadi zao. Hivyo basi, aliamrisha kwamba lile lango la ngome lifunguliwe na zile silaha zisalimishwe kwa Waislamu. Silaha zilizokuwamo ngomeni mle zilikuwa ni deraya 400, panga 500 na mikuki 400. Khalid aliondoka kwenda Madina pamoja na ngawira zile na Okaydar naye alifuatana naye. Kabla ya kuwasili Madina, Khalid alimpelekea Mtume (s.a.w.w.) mharuma wa Okaydar uliotarizwa kwa zari ambao yeye Okaydar alikuwa akijitandia mabegani mwake kama wafanyavyo wafalme.
Macho ya watu wenye tamaa za kiulimwengu yalipumbazwa katika kuutazama mharuma ule, lakini Mtume (s.a.w.w.) alionyesha kutoupendelea kabisa na akasema: “Mavazi ya watu watakaokwenda Peponi yatakuwa yenye kushangaza zaidi.”

Okaydar alikutana na Mtume (s.a.w.w.). Alikataa kusilimu, lakini alikubali kuwalipa Waislamu Jizyah na ukafanyika mkataba baina yake na Mtume (s.a.w.w.). Baada ya hapo alimpa zawadi zenye thamani na akamteua Abbad bin Bashir kumrejesha Duwmatul Jandal kwa usalama.18

Tathmini Ya Safari Ya Tabuk

Kwa matokeo ya safari hii yenye kuchosha ni kwamba, Mtume (s.a.w.w.) hakukutana uso kwa uso na adui na hakuna mapigano yaliyotokea, lakini faida fulani zilipatikana.19

Kwanza kabisa, safari hii iliharakisha upatikanaji wa heshima ya jeshi la Waislamu na Mtume (s.a.w,w) aliwezeshwa kutia ukuu na nguvu zake nyoyoni mwa watu wa Hijaz na watu wa mpakani mwa Shamu. Matokeo yake ni kwamba, marafiki pamoja na maadui wa Uislamu walipata kutambua kwamba nguvu

yake ya kijeshi inakua sana kiasi cha kuweza kuzikabili nguvu na kuzitishia na zikaogopa.

Majinai na uasi vimekuwa sifa ya pili ya makabila ya Kiarabu. Hata hivyo kule kuitambua nguvu ya kijeshi la Kislamu kuliweza kutowapinga Waislamu na kuasi dhidi yao. Hivyo basi, baada ya kurejea kwa Mtume (s.a.w.w.) Madina, wawakilishi wa makabila ambayo hadi pale yalikuwa bado hayajasalimu amri yalianza kuja Madina kwa wingi sana na kutangaza kuhusu utii wao kwa serikali ya Kislamu na kusilimu, kiasi kwamba mwaka wa tisa wa Hijiriya ulianza kuitwa 'mwaka wa wawakilishi.'

Pili, kwa kufanya mapatano mbalimbali na watu wa mipakani mwa Hijaz na Shamu, Waislamu walithibitishiwa usalama wa ukanda ule, nao walitosheka kwamba machifu wa makabila haya hawatashirikiana na jeshi la kirumi.

Tatu, kwa kuifanya safari hii yenye taabu, Mtume (s.a.w.w.) aliufanya utekaji wa Shamu kuwa wa rahisi zaidi. Aliwafanya makamanda wa jeshi lile kuyazoea matatizo ya ukanda ule na aliwafunza mbinu za kivita dhidi ya madola makubwa ya siku zile.

Hivyo basi, ukanda wa kwanza kutekwa na Waislamu baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa ni nchi ya Damascus na Shamu. Zaidi ya hapo, kwa kupeleka jeshi kubwa kiasi kile, waumini wa kweli waliweza kuainishwa kutokana na wanafiki, na maelewano mema yalidumishwa miongoni mwa Waislamu.

Wanafiki Waunda Makri Dhidi Ya Mtume (S.A.W.W.)

Mtume (s.a.w.w.) alikaa Tabuk siku kumi20 na akarejea Madina baada ya kumtuma Khalid kwenda Duwmatul Jandal. Wanafiki kumi na wawili ambao nane kati yao walitoka miongoni mwa Waquraishi na wale wanne waliosalia walikuwa wakazi wa Madina, waliamua kumshitua ngamia wa Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa juu ya njia nyembamba ya juu ya mlima iliyokuwako kwenye njia baina ya Madina na Shamu ili kumfanya Mtume (s.a.w.w.) aangukie bondeni.
Jeshi la Uislamu lilipoifikia sehemu ya kwanza ya njia hii, Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Yeyote yule apendaye kulipita jangwa anaweza kupita kwa sababu jangwa ni pana sana." Hata hivyo, yeye alipanda kwenye ile njia nyembamba wakati Hudhayfah alikuwa akimwendesha ngamia wake kwa nyuma na Ammar alikuwa akizishika hatamu zake kwa mbele.

Alipokigeuzia nyuma kichwa chake aliona kwenye mwanga wa mwezi kwamba watu waliokuwa wamewapanda wanyama walikuwa wakimfuata. Ili kuhakikisha kwamba wasiweze kutambulika walikuwa wamezifunika nyuso zao na walikuwa wakizungumza kwa kunong'onezana. Mtume (s.a.w.w.) alichukia sana na akawapa changamoto na akamwamrisha Hudhayfah awageuze ngamia wao kwa fimbo yake.

Mwito wa Mtume (s.a.w.w.) uliwaogofya mno nao walitambua ya kwamba ameitambua makri yao. Hivyo basi, upesi sana walirudi nyuma na kwenda kujiunga na askari wengine. Hudhayfah anasema: "Mimi niliwatambua kutokana na alama za ngamia wao na nilimwambia Mtume (s.a.w.w.): "Ninaweza

kukuambia ni nani hawa ili uwaadhibu.” Lakini Mtume aliniambia kwa sauti ya upole nisiifunue siri yao, kwa kuwa ulikuwapo uwezekano kwamba wakatubia.

Vilevile aliongeza kusema kwamba: “Kama nikiwaadhibu, wale wasio Waislamu watasema kwamba sasa Muhammad amepata mamlaka na amewafanya masahaba wake mwenyewe kuwa mawindo.”21

Vita Baridi

Hakuna mandhari iliyokuwa kuu zaidi ya mandhari ya kurejea kwa jeshi lililoshinda, linaporejea nchini mwake, na hakuna chenye kumfurahisha askari zaidi ya ushindi dhidi ya adui, ushindi unaoihami heshima yake na kuuthibitisha usalama na uhai wake. Ilitokea kwamba mambo yote mawili yalijidhihirisha na yaliweza kuonekana wakati wa kurejea kwa jeshi lililoshinda la Uislamu, kutoka Tabuk.

Baada ya kumaliza ile safiri baina ya Tabuk na Madina, lile jeshi la Uislamu liliwasili Madina kwa utukufu mkubwa. Wale askari wa Uislamu walifurahi sana na fahari ya ubora ilionekana kwenye mwendo na mazungumzo yao. Vilevile sababu ya fahari hii ilikuwa dhahiri, kwa sababu walililfanya taifa kuu lirudi nyuma katika mapambano ya kivita, ambalo ni ile nguvu ambayo hapo mwanzo ilimshinda adui wake aliyekuwa na nguvu zaidi (Iran). Na pia Waislamu wamewatiisha watu wa mipakani mwa Shamu na Hijaz.

Kwa hakika watu hawa wamejipatia heshima kwa kule kuwazidi nguvu adui na ni dhahiri kwamba walikuwa na haki ya kujivuna dhidi ya wale wengine waliobakia mjini Madina bila ya sababu ya haki. Hata hivyo, ulikuwapo uwezekano kwamba namna hii ya fikira, na huku kurejea kwa ushindi vingeliweza kujenga fahari isiyostahili akilini mwa watu wenye akili finyu, na ikawa ni matusi kwa baadhi ya wale watu waliobakia mjini Madina kwa sababu za haki lakini nyoyo zao zilikuwa pamoja na wale askari kule kwenye uwanja wa vita, nao walishirikiana kwa uaminifu kwenye neema na msiba wao.

Hivyo Mtume (s.a.w.w.) alilihutubia lile jeshi la Uislamu lilipokuwa mahali fulani karibu na Madina lilipotua kwa kitambo hivi, kwa maneno haya: “Huko Madina wako baadhi ya watu wanaokuungeni mkono kwenye safari hii na wakawa pamoja nanyi hatua kwa hatua.”

Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa ni vipi jambo hili lingaliweza kufikiriwa kwamba wale watu waliobakia mjini Madina nao pia walishiriki kwenye safari ile pamoja na lile jeshi. Mtume (s.a.w.w.) alijibu akisema: “Wao, ingawa walikuwa wakipendelea kushiriki kwenye jukumu hili takatifu (Jihadi), hawakuweza kujiunga kutokana na sababu njema.”22

Kwa njia ya hotuba hii fupi Mtume (s.a.w.w.) alidokezea juu ya mmoja wa mipango elekevu wa Uislamu na akawaongoza watu kwenye ukweli wa kwamba nia njema na fikira nyoofu huchukua nafasi ya amali za uchamungu, na wale watu waliokosa kutenda amali njema kutokana na kukosa kwao nguvu au mali, wanaweza kuwa washirika wa wale wengine katika malipo ya kiroho na kufidiwa kwa ajili ya amali njema. Kama Uislamu unataka matengenezo ya nje, una shauku kuu ya matengenezo ya kiroho na usafi

wa fikira, kwa sababu chanzo halisi cha matengenezo ni kuzitengeneza imani na namna ya fikira, na matendo yetu yote hutokana na fikira zetu.

Hivyo Mtume (s.a.w.w.) aliiondoa fahari isiyo ya haki ya wale Mujahidiin na akaihakikisha nafasi ya wale watu wanaosameheka, lakini kuanzia muda uleule alidhamiria kwamba atatoa adhabu ya mfano kwa wale waasi wasiokuwa na sababu ya haki wawezayo kuitoa. Tukio lifuatalo ni mfano wa kitendo cha aina hii.

Siku ambayo jeshi lote lilitangaziwa kuondoka mjini Madina, Waislamu watatu ambao ni Hilal, Ka'ab na Murarah walimjia Mtume (s.a.w.w.) na wakaomba kwamba wasamehewe kushiriki kwenye Jihad ile. Sababu waliyoitaja ilikuwa kwamba mazao yao mashambani na bustani zao yalikuwa bado hayajaiva kabisa. Vilevile walimwahidi Mtume (s.a.w.w.) kwamba watakapomaliza kuvuna baada ya siku chache hivi, watajiunga na jeshi la Waislamu huko Tabuk.

Wale watu wasio tofautisha baina ya faida za kimaada na uhuru wa kisiasa, ni watu wasio na uoni wa mbali wanaozichukulia anasa za huu ulimwengu zenye kupita kuwa sawa na maisha yenye heshima, awezayo kuyaishi mtu chini ya bendera ya uhuru wa kiakili, kisiasa na kiutamaduni, na wakati mwingine mtu huyapenda zaidi maisha tuliyoyataja kwanza kuliko haya ya pili.

Baada ya kurejea Madina kutoka Tabuk Mtume (s.a.w.w.) alilazimika kuwaadhibu watu hao ili kuyazuia maradhi haya yasiingie kwenye akili za watu wengine. Si hivyo tu kwamba watu hawa hawakushiriki kwenye Jihad lakini vile vile hawakuitimiza ile ahadi waliyomwahidi Mtume (s.a.w.w.). Walikuwa bado wangali wakijishughulisha na biashara zao na katika kujilimbikizia utajiri wakati kwa ghafla taarifa za kurejea kwa Mtume (s.a.w.w.) kwa ushindi zilipoenea mjini Madina.

Watu hawa watatu, ili kufanya masahihisho kwa tabia zao mbaya na kuwahadaa Waislamu wengine, walikwenda kumlaki Mtume (s.a.w.w.) kama walivyofanya wengineo wote na wakatoa heshima zao kwake na kumpongeza; lakini yeye hakuwasikiliza. Alipofika Madina aliwahutubia watu miongoni mwa wale wote waliokuwa wakishereheka na hoi hoi, na jambo la kwanza alilolisema lilikuwa hili: "Enyi watu! Watu hawa watatu walizitweza sheria za Kiislamu pia hawakuitimiza ahadi yao waliyoniahidi. Walizipendelea faida za kidunia badala ya yale maisha ya heshima chini ya bendera ya Uislamu. Hivyo basi hamna budi kukata uhusiano nao."

Idadi ya waasi ilifikia tisini lakini kwa vile wengi wao walikuwa wa kundi la wanafiki, na haikuweza kutegemewa kutoka kwao kwamba watajiunga kwenye Jihad dhidi ya adui, shinikizo lilielekezwa kwa hawa Waislamu watatu, ambao Murarah na Hilal, walikuwa wameshiriki kwenye Vita vya Badr na waliheshimiwa miongini mwa Waislamu.

Sera yenye hekima ya Mtume (s.a.w.w.) ambayo ni sehemu muhimu yenye kukamilisha Uislamu ilikuwa na athari za ajabu. Biashara na shughuli za waasi zilisimama kabisa. Biashara zao hazikupata wanunuzi kwenye soko. Ndugu zao wa karibu zaidi wakakata uhusiano nao na wakaacha hata kuzungumza nao au kuwatembelea. Mgomo wa kijamii walioufanya watu dhidi yao ulishusha mno moyo na juhudi za watu

hawa kiasi kwamba ile ardhi ya Madina iliyokuwa pana haikuweza kuwa chochote zaidi ya kuwa kitundu kwao.23

Hivyo ilikuwa ni bahati njema kwamba watu hawa watatu, kwa akili na uoni wao waliweza kutambua kwamba maisha kwenye mazingira ya Kiislamu hayakuwezekana bila ya kushirikiana na Waislamu kwa moyo wote, na maisha ya watu wachache mno wenye kwenda kinyume na walio wengi yasingeliweza kudumu muda mrefu, hasa pale inapokuwa kwamba lile kundi la walio wachache ni la watu waasi, fitna, wagomvi na wenye mfundo.

Kwa upande mmoja wameitwa watoe maelezo yao na kwa upande mwingine ile nguvu ya kimaumbile na silika inawavutia tena kwenye itikadi sahihi, nao wakatubia kwa Allah kwa kile kitendo chao cha woga. Allah Naye aliwasamehe na akamwarifu Mtume Wake (s.a.w.w.) kule kuwasamehe Kwake. Hivyo basi, amri ihusuyo kufutwa kwa mgomo ule ilitangazwa upesi sana.24

Tukio La Masjid Dhiraar

Kwenye Rasi ya Uarabuni Madina na Najraan zilichukuliwa kuwa ni maeneo mapana na vituo vikuu vya Ahlul–Kitaab (Watu wa Kitabu). Hivyo basi, baadhi ya Waarabu wa makabila ya Aws na Khazraji walikuwa na mwelekeo na dini ya Uyahudi na Ukristo, nao walikuwa wafuasi wa dini hizi.

Kwenye Zama za Ujahilia Abu Aamir baba yake Hanzalah, yule shahidi maarufu wa Vita vya Uhud, alikuwa na mwelekeo mkubwa na Ukristo na alikuwa mtawa. Uislamu ulipoanza mjini Madina na kuimeza jamii ndogo ya dini, Abu Aamir alichukizwa sana na akaanza kushirikiana kwa uaminifu na wanafiki wa makabila ya Aws na Khazraji. Mtume (s.a.w.w.) aliyatambua matendo yake yenye uharibifu na akataka kumkamata, lakini alikimbia kutoka Madina akaenda Makka na kisha akaenda Taa'if, na baada ya kutekwa kwa Taa'if alikwenda Shamu. Kutoka pale alianza kuuongoza mtandao wa ujasusi wa wanafiki.

Kwenye moja ya barua zake, Abu Aamir aliwaandikia marafiki zake hivi: "Jengeni msikiti kwenye kijiji cha Quba'a mkabala na msikiti wa Waislamu. Kusanyikeni hapo nyakati za sala, na kwa kujifanya kana kwamba mnasali, jadilianeni na pangeni mipango dhidi ya Uislamu na Waislamu."

Kama walivyo wale maadui wa Uislamu wa siku hizi, Abu Aamri naye alitambua kwamba kwenye nchi ambayo dini ilikuwa imeshamiri, njia iliyo bora zaidi ya kuiangamiza ni kulitumia jina la dini ile, na dini inaweza kudhuriwa zaidi kwa kulitumia jina lake kuliko njia yoyote nyingine. Alijua vizuri sana kwamba Mtume (s.a.w.w.) asingeliwaruhusu wanafiki wajijengee kituo kwa hali yoyote ile, isipokuwa pale walipokipa kituo kile rangi ya kidini na wakajenga sehemu ya kukutania kwa ajili yao kwa jina la msikiti.

Mtume (s.a.w.w.) alipodhamiria kwenda Tabuk wawakilishi wa wanafiki walimjia na kumwomba awaruhusu kujenga msikiti kwenye eneo lao, kwa kusema kwamba katika usiku wa giza au inaponyesha mvua wazee na wagonjwa wao hawakuweza kwenda mwendo mrefu tangu kwenye nyumba zao hadi

kwenye Masjid Qubaa. Mtume (s.a.w.w.) hakuwapa jibu lolote lile la kukubali au la kukataa, na aliahirisha kutoa uamuzi wa mwisho juu ya jambo hili hadi baada ya kurejea kutoka kwenye ile safari iliyokusudiwa.25

Baada ya Mtume (s.a.w.w.) kutoka, wale wanafiki walichagua mahali na wakakijenga hadi wakakimaliza upesi iwezekanavyo kile kituo chao cha kuundia maovu, kwa kukipa jina la msikiti. Katika siku ambayo Mtume (s.a.w.w.) alirejea Madina walimwomba afanye sherehe ya kuifungua sehemu ile ya ibada kwa kusimamisha rakaa chache za sala mahali hapa.

Wakati huo huo Malaika Mkuu Jibril alishuka na kumweleza Mtume (s.a.w.w.) kuhusu hali ya jambo lile la Masjid Dhiraar kwa kuwa ulijengwa ili kujenga mfarakano miongoni mwa Waislamu.26 Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha Masjid Dhiraar ibomolewe kabisa, boriti zake zichomwe na takataka zake zitupwe hapo kwa muda fulani.27

Kubomolewa kwa Masjid Dhiraar kulikuwa ni pigo kali kwa wanafiki na baada ya hapo kikundi chao kilivunjika na Abdullah bin Ubay, mtu pekee aliyekuwa akiwaunga mkono naye alikufa baada ya miezi miwili tangu kupiganwa kwa Vita vya Tabuk.

Tabuk ilikuwa ni vita vya mwisho vya Uislamu ambavyo Mtume alishiriki. Baada ya vita hivi Mtume hakushiriki kwenye vita nyingine yoyote ile.

---

1. Tabaqaatil–Kubra, juz. 2, uk. 165.
2. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk. 166.
3. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 1003.
4. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 517.
5. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk 518. Maghaazil–Waaqidi, juz. 3, uk. 992–993.
6. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 520; Bihaarul An'war, Juz. 21, uk. 207.
7. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 990.
8. Bihaarul–Anwaar, Juz. 21, uk. 244.
9. Siiratu Ibh Hisham, Juz. 2, uk. 520. Lakini Waaqidi amelihusisha tukio hili kwa mabadiliko kidogo, na Abdulah bin Khaythamah.
10. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 3, uk. 152.
11. Allah (s.w.t) amesema: "(Yeye ndiye) Mjuzi wa siri, na wala Hamdhihirishii yeyote yule siri Zake ila kwa Mtume Aliyemchagua; na kisha Humwekea mlinzi mbele yake na nyuma yake." (Sura al Jinn, 72:27)
12. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 523.
13. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 525.
14. Maghaazil–Waaqidi, Juz. 3, uk. 1000.
15. Siiratu Ibn Halabi, Juz. 3, uk. 161.
16. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 526; Siiratu Ibn Halabi, Juz.3, uk. 160; na Bihaarul–An'waar, Juz. 21, uk. 160.
17. Duwmah ilikuwa umbali wa maili 10 (Kilomita 16) kutoka Madina.
18. Tabaqaatil–Kubra, Juz. 2, uk. 146; Bihaarul–An'waar, Juz. 2, uk 246.
19. Mtume (s.a.w.w.) alikaa Tabuk siku ishirini. Siku moja baada ya kusali sala ya asubuhi alitoa hotuba moja iliyokuwa ndefu, yenye ufasaha wa lugha na yenye mafunzo. Baada ya hapo aliyanukuu maneno ya hotuba ile (Maghaazil–Waaqidi, juz. 3, uk. 1014–1015).

20. Muda wa kukaa kwa Mtume (s.a.w.w.) kule Tabuk umeelezwa kwamba ni siku ishirini. (Siiratu Ibn Hisham, Juz.3, uk. 527; Tabaqaati Ibn Sa'ad, Juz. 2, uk. 168).
21. Maghaazil- Waaqidi, Juz. 3, uk. 1042-1043; Bihaarul-An'waar, juz. 21, uk. 247; Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 162.
22. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 163; Bihaarul-An'waar, juz. 20, uk. 219.
23. Maneno ya sentensi hii ni nukuu itokayo kwenye Qur'ani ambako imesemekana kwamba "Kana kwamba haikuwako nafasi kwenye nchi yote (hii) iliyo pana ya kuweza kuwaficha au kwenye nafsi zao kuweza kuwafariji." (Surah, al-Tawbah, 9:118).
24. (Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 165 na Bihaarul-Anwaar, Juz. 10, uk. 119). Hii njia ya Mtume (s.a.w.w.) yenye mafunzo ilikuwa mfano kwetu sisi Waislamu, kuhusiana na kikundi cha watu walio wachache kwenye jamii. Upinzani wa aina hiyo ungeliweza kuondolewa tu kwa uaminifu, dhamira na umoja. Waaqidi ametoa maelezo marefu zaidi ya hawa watu watatu. (Tazama Maghaaz, Juz. 3, uk. 1045-1056).
25. Maghaazil-Waaqidi, Juz. 3, uk. 1046.
26. Aya 107-110 za Surah al-Tawbah zilifunuliwa kuhusiana na Masjid Dhiraar.
27. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 530; Bihaarul-An'waar, juz. 20, uk. 253.

Sura Ya 54: Wajumbe Wa Kabila La Thaqif Waenda Madina

Vita vya Tabuk pamoja na matatizo na taabu zake vilimalizika, na Mujahidiin wote walirejea Madina wakiwa wamechoka kabisa. Askari wa Uislamu hawakupambana na adui yeyote mle njiani na hawakupata ngawira yoyote.

Kwa sababu hii, baadhi ya watu wenye uoni mfinyu waliichukulia safari hii kuwa ni isiyo na faida. Hata hivyo, wao hawakuzifikiria faida zake za ndani. Mara tu baada ya hapo faida hizi zikawa za dhahiri na makabila ya Waarabu wakaidi ambao hapo kwanza hawakuwa tayari kusalimu amri au kusilimu kwa hali yoyote ile, walianza kuwaleta wawakilishi wao kwa Mtume (s.a.w.w.) na wakatangaza kuwa kwao tayari kusilimu, na kuyafungua malango ya ngome zao na kwamba masanamu yaliyowekwa humo yaweze kuvunjwa, na bendera ya Uislamu na Dini ya Allah iweze kudu- mishwa badala ya hii ya masanamu haya.

Kama jambo la kanuni, watu wapumbavu na wasioona mbali daima waliyapa umuhimu matokeo ya dhahiri. Kwa mfano, kama wakati wa safari hii wale askari wangelipambana na adui na baada ya kumshinda wakainyakua mali yake, watu hawa wangelisema kwamba matokeo ya vita vile yalikuwa mazuri sana. Hata hivyo, watu wenye kuona mbali huyatafi- ti matukio na kuuchukulia kuwa ni mzuri na wenye matunda mazuri ule ukweli usadiao katika kuifikia nia na madhumuni.

Kwa bahati njema Vita vya Tabuk vilikuwa na faida katika kulifikia lengo halisi la Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.), yaani kuyavutia makabila ya Kiarabu kwenye dini ya Uislamu. Ilikuwa hivyo kwa sababu taarifa zilizoenea kila mahali nchini Hijaz kwamba Warumi (Wale wale ambao kwenye vita vyao vya

mwisho dhidi ya Wairani ambao kwa muda mrefu sana walikuwa wakitawala nchi ya Yemen na maeneo jirani yake, waliwashinda Wairani na wakaurudisha ule Msalaba kutoka kwao na kuuleta Yerusalem) wametishwa na nguvu ya kijeshi ya Waislamu nao hawakuthubutu kupigana nao.

Kuenea kwa taarifa hii kulitosha kuyafanya makabila ya Kiarabu yaliyokuwa makaidi, ambayo hadi kwenye siku iliyopita walikuwa kwa vyovyote iwavyo bado hawajakubali kukaa kwa amani na Waislamu, kufikia kushirikiana nao na kujiunga nao katika kujisalimisha kutokana na uasi wa Warumi na Wairani, haya mataifa makuu mawili ya ulimwengu wa wakati ule. Ufuatao hapa chini ni mfano wa mabadiliko yaliyotokea miongoni mwa makabila makaidi ya Kiarabu

Mfarakano Miongoni Mwa Watu Wa Kabila La Thaqif

Watu wa kabila la Thaqif walikuwa maarufu miongoni mwa Waarabu kwa ukaidi na ugumu wao. Walilipinga jeshi la Waislamu kwa mwezi mzima chini ya hifadhi ya ngome madhubuti ya Ta'aif nao hawakukubali kusalimu amri mbele yao.1
Urwah bin Mas'ud alikuwa mmoja wa machifu wa kabila la Thaqif. Alipopata kuutambua ushindi mkubwa wa jeshi la Uislamu kule Tabuk alikutana na Mtume (s.a.w.w.) kabla ya kuwasili kwake mjini Madina, akasilimu na akamwomba ruhusa arejee kwenye kabila lake na akaitangaze dini ya Allah miongoni mwao. Mtume (s.a.w.w.) alimwonya kuhusu matokeo ya ujumbe wake ule na akasema: "Mimi ninachelea kwamba unaweza ukaupoteza uhai wako kwenye njia hii." Alijibu, akisema: "Wananipenda zaidi kuliko macho yao."

Kabila lake na machifu wengine walikuwa bado hawajautambua ukuu alioupata Urwah kutokana na Uislamu. Hivyo basi, waliamua kwamba pale mubalighi wa kwanza wa Uislamu atakapojishughulisha katika kuwalingania watu Uislamu, wao wamnyeshee mvua ya mishale mwilini mwake na wamuuwe. Matokeo ni kwmaba, Urwah alishambuliwa na alipokaribia kufa, alisema: "Kifo changu ni baraka ambayo Mtume ameniarifu."

Wajumbe Wa Thaqif Wakutana Na Mtume (S.A.W.W.)

Watu wa kabila la Thaqif walijuta kwa kumuuwa Urwah na wakatambua kwamba ilikuwa ni jambo lisilowezekana kwao kuishi katikati ya nchi ya Hijaz wakati bendera ya Uislamu ilikuwa ikipepea kandokando yao, na malisho na njia za biashara zilitishiwa na Waislamu. Kwenye mkutano waliouitisha ili kulitatua tatizo hili, iliamuliwa kwamba wampeleke mjumbe wao Madina akakutane na Mtume (s.a.w.w.) na amweleze kuhusu kuwa kwao tayari kusilimu chini ya masharti fulani fulani.

Wote kwa pamoja walimteua mmoja wa wazee wao aliyeitwa Abd Yaalayl kwenda Madina na kuufikisha ujumbe wao kwa Mtume (s.a.w.w.), lakini alikataa kulibeba jukumu lile na akasema: "Si jambo lisilowezekana kwamba baada ya kuondoka kwangu mkayabadili mawazo yenu na mimi nami yakanipata yale yaliyompata Urwah." Na akaongeza kusema: "Niko tayari kuwa mwakilishi wenu kwa masharti ya kwamba wazee wengine watano wa kabila la Thaqif niende nao na sisi sote tuwe na

majukumu yaliyo sawa katika jambo hili.”

Ushauri aliotoa Abd Yaalayl ulikubaliwa na watu wale. Hivyo basi, watu wote sita walitoka na kwenda Madina na wakatua kwenye kijimto kilichokuwa kandokando ya chemchemu karibu na Madina.

Mughirah bin Shu’ubah Thaqafi aliyewaleta farasi wa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) malishoni aliwaona wale machifu wa kabila lake pale ukingoni mwa ile chemchemu.

Upesi sana aliwaendea na akapata kuitambua shabaha ya safari yao ile. Kisha aliwaachia wale farasi na akarejea Madina upesi ilivyowezekana kwenda kumjulisha Mtume (s.a.ww) kuhusu ule uamuzi uliochukuliwa na watu wakaidi wa kabila la Thaqif. Alipokuwa njiani alikutana na Abu Bakr na akamweleza jambo lile. Alimwomba Mughirah amruhusu azifikishe zile taarifa za kuwasili kwa wajumbe wa Thaqif kwa Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe.

Hatimaye Abu Bakr alimwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu kuwasili kwa wajumbe wa kabila la Thaqif na akaongeza kusema kwamba walikuwa tayari kusilimu ili mradi tu baadhi ya masharti yao yakikubaliwa na ukafanyika mkataba. Mtume (s.a.w.w.) aliamrisha likitwe hema karibu na msikiti kwa ajili ya hawa wajumbe wa Thaqif na kwamba Mughirah na Khalid bin Sa’id wawapokee.

Hawa wajumbe wa msafara wa Thaqif walimjia Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Mughirah aliwashauri kwamba wajiepushe na aina zote za salam za zama za ujinga na watoe salam kama Waislamu. Hata hivyo, kwa vile fahari na majivuno ilikuwa sifa ya pili ya kabila hili walimsalimu Mtume (s.a.w.w.) kwa desturi ya zama za kabla ya Uislamu. Kisha waliuwakilisha ujumbe wa kabila la Thaqif na kuwa kwao tayari kusilimu na wakaongeza kusema kwamba huko kusilimu kwao kutakuwa chini ya masharti fulani watakayoyaeleza kwenye mkutano utakaofuatia.
Majadiliano ya wale wajumbe wa kabila la Thaqif yaliendelea kwa siku kadhaa na Khalid aliendelea kumwarifu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu taarifa zao.

Masharti Ya Ujumbe Wa Thaqif.

Mtume (s.a.w.w) aliyakubali mengi ya masharti waliyoyatoa kiasi kwam– ba alikubali kufanya nao mkataba wa usalama na akazihakikishia nchi zao. Hata hivyo, baadhi ya masharti yao hayakuwa sahihi hata kidogo, yenye kuchukiza na yasiyo ya adabu njema kiasi kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliudhika. Masharti yao yalikuwa kama ifuatavyo hapa chini:

Kwamba watu wa Taa’if wasilimu kwa sharti la kwamba hekalu kubwa la masanamu la Taa’if libakishwe kwa kipindi cha miaka mitatu, na sanamu kubwa la kabila lao liitwalo Laat liendelee kuabudiwa. Hata hivyo, walipotambua kwamba sharti lao hili limemuudhi Mtume (s.a.w.w.) walil– isahihisha na wakaomba kwamba lile hekalu la masanamu libakie kwa kipindi cha mwezi mmoja. Kumwomba Mtume (s.a.w.w.) jambo hili, ambaye lengo lake kimsingi lilikuwa ni kuidumisha ibada ya Allah Aliye Mmoja tu, na kuyabomoa mahekalu ya masanamu na masanamu yenyewe kulikuwa aibu kubwa, ilionyesha kwamba

waliutaka Uislamu ambao hautayadhuru maslahi na mwelekeo wao, na kama hilo haliwezekani basi dini hii haikubaliki kwao. Walipoutambua ubaya wa ombi lao hili, walianza kuomba msamaha na kusema.

“Tumetoa ombi hili kuwanyamazisha wanawake wetu na watu wetu walio wajinga na kwa njia hii tuweze kuviondoa vizuizi vyote vilivyomo kwenye njia ya kuwasili kwa Uislamu mjini Taa’if. Sasa kwa vile Mtume hakubaliani nalo, basi tafadhalini na awasamehe watu wa kabila letu kutokana na kuyavunja masanamu kwa mikono yao wenyewe na waweze kuwateua watu wengine waifanye kazi hii.” Mtume (s.a.w.w.) alikubaliana na wazo hilo. Kwa kuwa lengo lake lilikuwa kwamba miungu wa uwongo na ujinga vifutiliwe mbali basi hapo suala la nani ayavunje lilikuwa ni jambo lisilo na maana kwake, ni sawa kwake kama kazi hii ikifanywa na watu wale wenyewe au na mtu yeyote mwingine.

Sharti lingine lilikuwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) awasamehe kusali. Walikuwa wakidhania kwamba kama walivyo viongozi wa watu wa Kitabu, Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) anaweza kuziingilia sheria za Allah na hivyo akazitumia kanuni fulani fulani kwa ajili ya kundi moja na kuwaacha wengine wasizitumie kanuni zile. Hawakutambua kwamba ilimbidi kuutii wahyi wa Allah na kwamba asingeliweza kuufanyia mabadiliko. Sharti hilo lilionyesha kwamba moyo wa kujitoa kabisa kabisa katika kuyatimiza mapenzi ya Allah ulikuwa bado haujashamirisha mizizi yake akilini mwao, na kusilimu kwao ni kwa kujionyesha tu. Au la, haikuwepo haki yoyote katika kufanya upendeleo kwao kwenye sheria za Uislamu na kuzikubali baadhi yao na kuzikataa nyingine. Uislamu na kumwamini Allah ni sharti la kujitoa kabisa kabisa ili kuyatimiza mapenzi ya Allah ambayo chini yake amri za Allah zote hutiiwa bila ya kusitasita na hakuna ubaguzi baina yao. Akiwajibu, Mtume (s.a.w.w.) aliwaambia: “Hakuna faida yoyote kwa dini isiyo kuwa na sala.”

Kwa kauli nyingine ni kwamba, mtu asiyemwinamishia Allah kichwa chake wakati wa mchana na vilevile wakati wa usiku, atakuwa hamkumbuki Mola wake na si Mwislamu wa kweli.

Baada ya hapo, hatimaye yale masharti yalitiwa saini na Mtume (s.a.w.w.) na kisha akawaaga wale wajumbe wa msafara ule waliokuwa wakirejea kwenye kabila lao. Miongoni mwa wale watu sita, alimteua kwa ajili ya uongozi kijana mdogo zaidi miongoni mwao ambaye katika kile kipindi cha kukaa kwao mjini Madina alionyesha shauku kubwa ya kujifunza Qur’ani na amri za Allah. Alimteua kuwa mwakilishi wake wa kidini na kisiasa miongoni mwa watu wa Taa’if na akamshauri kwamba atakapokuwa akisalisha sala ya jamaa, awafikirie watu wanyonge hivyo asiirefushe sala. Kisha Mughirah na Abu Sufyani waliteuliwa kufuatana na wale wajumbe hadi Taa’if kwenda kuyavunja yale masanamu yaliyokuwako pale. Abu Sufyani ambaye hadi katika siku iliyopita alikuwa mlinzi wa masanamu na amesabahisha umwagaji wa damu mwingi mno kwa ajili ya kuyahami, sasa aliishika shoka na kishoka kidogo na kuyavun– ja vipande vipande hadi yakalichukua umbile la kichuguu cha kuni. Akayauza mapambo ya yale masanamu, na kama alivyoelekezwa na Mtume (s.a.w.w.) akayalipa madeni ya ‘Urwah na ndugu yake aliyeitwa Aswad kutokana na mauzo ya yale mapambo.2

1. Maelezo ya mazingiwa ya Ngome ya Taa'if yamekwishakutolewa kuhusiana na matukio ya mwaka wa 8 Hijiriya.
2. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 542; Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 243

Sura Ya 55: Mtume (S.A.W.W.) Amuomboleza Mwanawe

"Kipenzi Ibrahim! Hatuwezi kufanya lolote lile juu yako. Mapenzi ya Allah hayawezi kubadilishwa na machozi, na moyo wangu unasikitika na kuhuzunika kwa kifo chako. Hata hivyo, sitasema lolote lile liwezalo kule– ta ghadhabu ya Allah. Kama isingalikuwako ahadi ya kweli na ya uhakika kwamba sisi nasi tutakuja baada yako, ningalilia sana kuhuzunika zaidi kwa kutengana nawe"1

Sentensi hizi zilitamkwa na Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alipokuwa akimuomboleza mwanawe mpenzi, Ibrahim aliyekuwa akikata roho akiwa mapajani mwa baba yake.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ameiweka midomo yake ya huruma kwenye uso wenye rangi ya waridi wa mwanawe na kumpa kwaheri huku akiwa mwenye uso wenye huzuni mno na moyo mzito na wakati huo huo akiwa kwenye kujinyenyekeza kwenye mapenzi ya Allah.

Mapenzi kwa dhuria wake mtu ni moja ya udhihirisho halisi mno na mtukufu zaidi wa moyo wa ubinadamu, na ni dalili ya afya na utakaso halisi wa nafsi yake mtu.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kila mara akisema: "Kuwa mpole kwa watoto wako na uonyeshe hisia za huruma kwao. "2 Zaidi ya hapo, huruma na upendo kwa watoto ilikuwa moja ya sifa zake zenye kupendeza.3

Katika miaka iliyopita, Mtume (s.a.w.w.) alikabiliwa na vifo vya wanawe watatu ambao ni Qaasim, Taahir na Tayyib4 na mabinti watatu ambao ni Zaynab, Ruqayyah na Ummu Kuluthumu, na amekuwa akihuzunika sana kutokana na jambo hili. Baada ya vifo vyao, mwanawe pekee aliyesalia hai, na kumbukumbu ya mkewe kipenzi, Bibi Khadija (a.s.) alikuwa ni Bibi Fatimah (a.s.).

Katika mwaka wa sita Hijiriya aliwapeleka wajumbe wake kwenye nchi za kigeni ikiwa ni pamoja na Misri. Alimpelekea barua mtawala wa Misri akimwita kwenye Uislamu. Ingawa hakuujibu mwito wa Mtume (s.a.w.w.) kwa jibu la dhahiri, lakini alimpelekea jibu la heshima pamoja na zawadi fulani fulani zikiwa ni pamoja na mjakazi aliyeitwa Maarya. Baadae mjakazi huyu alipata heshima ya kuwa mkewe Mtume (s.a.w.w.) na kumzalia mwana aliyeitwa Ibrahim, aliyependwa sana na Mtume (s.a.w.w.).

Kuzaliwa kwa Ibrahim kulimaliza kwa kiasi fulani zile athari mbaya zilizoletwa na vifo vya watoto wake sita, na kulimpa faraja. Hata hivyo, kwa masikitiko yake makubwa Ibrahim naye alifariki dunia baada ya

miezi kumi na minane. Ilikuwa Mtume (s.a.w.w.) ametoka nyumbani mwake kwa kazi fulani alipoitambua hali ngumu ya mtoto wake.

Alirejea nyumbani akamchukua mtoto kutoka mapajani mwa mama yake, na wakati dalili za hali ngumu zilipokuwa zikijidhihirisha usoni mwake, alizitamka zile kauli tulizozitaja hapo juu.

Maombolezo ya Mtume (s.a.w.w.) kwa ajili ya mwanawe ni dalili ya hisia za ubinadamu ulioendelea hata baada ya kifo cha mtoto yule.

Na ule mdhihiriko wa hisia na kuzionyesha huzuni ulikuwa ni dalili ya upole wake uliojidhihirisha bila ya kukusudia maishani mwake mwote. Ama kuhusu kutotamka neno lolote lililo dhidi ya radhi ya Allah, ilikuwa ni dalili ya imani yake na kuyapokea Mapenzi ya Allah, ambayo hakuna yeyote awezaye kuyaepuka.

Kizuizi Kisicho Na Msingi

Abdur-Rahman bin Awf aliyekuwa wa familia ya Ansar, alishangaa alipomwona Mtume (s.a.w.w.) akitokwa na machozi. Alimzuia akisema: “Umekuwa ukituzuia tusililie maiti. Basi inakuwaje kwamba hivi sasa wewe unatokwa na machozi kwa kifo cha mwanao?” Mzuiaji huyu, sio tu kwamba hakutambua misingi mitukufu ya Uislamu lakini vile vile alikuwa mjinga wa moyo na hisia maalum ambazo kwazo Allah Mwenye nguvu zote amemjaalia mwanadamu. Silika zote za kibinadamu zimeumbwa kwa lengo maalum na ni muhimu kwamba kila moja ijidhihirishe kwenye wakati na sehemu yake maalumu. Mtu asiyeshitushwa na kifo cha ndugu yake wa karibu zaidi, ambaye moyo wake haushituki, ambaye macho yake hayatiririkwi na machozi, kwa kifupi mtu asiyezidhihirisha athari zozote kutokana na kutengwa, basi yeye si chochote kile zaidi ya kuwa ni jiwe, na hastahili kuitwa mwanadamu.

Hata hivyo, hapa kuna jambo lililo nyeti na listahililo kuzingatiwa, kwa sababu ingawa kizuizi hiki hakikuwa na msingi lakini kinatufahamisha ya kwamba uhuru kamili na demokrasia halisi ilikuwepo kwenye jamii mpya ya Waislamu wakati ule, ili kwamba mtu angeliweza kuwa na moyo wa kuyafasiri matendo ya mtawala wake pekee kwa uhuru halisi na bila ya kuwapo woga wowote au hofu na vile vile akaweza kupata jibu. Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: “Mimi katu sikusema kwamba msililie vifo vya wapenzi wenu, kwa sababu huko kulia ni dalili ya huruma na masikitiko, na mtu ambaye moyo wake hauhuzunishwi na matatizo yawapatayo wenzie hana haki ya kuipata baraka ya Allah.5 Nimesema kwamba msip- ite kiasi katika maombolezo kwa ajili ya vifo vya ndugu zenu wa karibu zaidi, na katu msitamke neno chafu au lisilofaa wala kupasua mavazi kutokana na huzuni iliyokithiri.”6

Kama alivyoeleza Mtume (s.a.w.w.) Amirul-Mu’minin (a.s.) aliiosha maiti ya Ibrahim na kuikafini. Kisha Mtume (s.a.w.w.) na baadhi ya masahaba wake waliisindikiza maiti na kumzika mtoto yule kwenye mava ya Baqi.7

Mtume (s.a.w.w.) aliangalia kaburi la Ibrahim na akaona shimo kwenye pembe ya kaburi lile. Ili kulifukia

alikaa chini akalisawazisha lile kaburi kwa mikono yake, na akatamka kauli ifuatayo: “Kila mmoja miongoni mwenu anapoifanya kazi fulani hana budi kujitahidi kuifanya kwa ufanisi zaidi.”

Kampeni Dhidi Ya Usihiri

Jua lilipatwa siku ya kufariki dunia kwa Ibrahim. Baadhi ya watu wajinga wasiozijua kanuni za maumbile walifikiria kwamba jua limepatwa kutokana na kifo cha Ibrahim. Ingawa fikira hizi hazikuwa na msingi, kwa dhahiri ingelikuwa na faida kwa Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, kama angelikuwa yu mtu wa kawaida na kiongozi wa kiulimwengu, angeliy- athibitisha maoni haya na hivyo akauthibitisha ukuu na utukufu wake.

Hata hivyo, kinyume na fikira hii, aliipanda mimbari na akawaarifu watu kuhusu hali halisi. Alisema: “Enyi watu! Naifahamike wazi kwenu kwam- ba jua na mwezi ni dalili ya uwezo wa Allah.
Vinasogea kwenye njia zao maalumu alizoziamrisha Allah kwa ajili yao kwa mujibu wa kanuni za maumbile.
Havipatwi kutokana na kifo au kuzaliwa kwa yeyote yule. Ni jukumu lenu wakati wa kupatwa kwa jua kusali.”8
Kinyume na walivyofikiria wengi ambao sio tu kwamba walizitafsiri kweli kutegemeana na wapendavyo, lakini vile vile hujinufaisha na kule kutojua kwa watu na fikira za ngano zao, lakini Mtume (s.a.w.w.) hakuzificha kweli wala hakujaribu kujinufaisha kutokana na ujinga wa watu.

Kama katika siku ile angeliithibitisha dhana hii potovu, basi asingeliweza kujitukuza na kudai kwamba yeye yu kiongozi wa milele wa wanadamu na mwakilishi na mteule wa Allah kwenye zama hizi wakati elimu ya unajimu imeshachukua hatua ndefu na sababu za kupatwa kwa jua na kwa mwezi zimeshafahamika kwa mwanadamu.

Sheria na mwito wake kwa Allah si kwa Waarabu peke yao na havitumiki kwenye wakati au sehemu maalum. Kama yeye Mtume (s.a.w.w.) yu kiongozi wa wale walioishi kwenye zama za awali, vile vile yeye yu Mtume wa hawa waishio kwenye zama za anga na wa zama za ugunduzi wa siri za maumbile. Kila uwanja wa elimu wowote ule aliouzungumzia, maneno yake ni dhahiri kabisa kiasi kwamba mageuzi ya kisayansi ya hivi karibuni yaliyozitangua dhana nyingi za wanachuoni wa kale, hayakuweza kupata japo nukta moja iliyo dhaifu katika kauli zake.

---

1. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 34; Bihaalul-Anwaar, Juz. 22, uk. 157.
2. Biharul-Anwaar, Juz. 23, uk. 114.
3. Muhajjatul Bayzah, Juz. 3, uk. 366.
4. Bihaarul Anwaar, Juz. 22, uk. 166. Hata hivyo, baadhi ya wanachuoni wa Kishiah wamesema kwamba alikuwa na wana wawili tu kutokana na bibi Khadija (a.s.) (Bihaarul Anwaar, Juz. 2, uk. 151-Toleo jipya).
5. Bihaarul-Anwaar, Juz. 22, uk. 151.
6. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 348.
7. (Bihaarul-Anwaar, juz. 22, uk. 156) kufuatana na maelezo ya Halabi, kule kuosha na kukafini kwa mwana wa Mtume

(s.a.w.w.) Ibrahimu, kulifanywa na Fazal mwana wa binamu yake Mtume (s.a.w.w.) Abbas.

8. Al–Muhaasin, uk. 313 na Siiratu Halabi, juz. 3, uk. 348.

Sura Ya 56: Kufutwa Kwa Ibada Ya Masanamu Bara Arabuni

Mwishoni mwa mwaka wa tisa Hijiriya, aya za mwanzoni za Sura al– Tawbah (*Baraa'at*) ziliteremshwa na Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa kumpeleka mtu Makka wakati wa Hijja ili akazisome aya hizo pamoja na tangazo lenye ibara nne.

Kwenye aya hizi, usalama waliothibitishiwa washirikina umefutiliwa mbali na mikataba yote iliyofanywa baina yao na Waislamu (ila ule ambao pande zote mbili hawajauvunja na wameutekeleza kimatendo) imebatilishwa, na machifu wa ushirikina na wafuasi wao wameambiwa kwamba hawana budi kudhihirisha msimamo wao ndani ya kipindi cha miezi minane kuelekea kwenye serikali ya Kiislamu iliyosimamia kwenye msingi wa Upweke wa Allah na kama hawatauacha ushirikina na ibada ya masanamu, basi kule kuachiwa huru walikopewa kutakoma.

Mustashirik wanapoifikia hatua hii ya historia ya Uislamu, huishambulia dini hii vikali mno na kuuchukulia ukali huu kuwa ni kinyume na msingi wa uhuru wa kuabudu. Hata hivyo, kama wangalifanya utafiti wa historia ya Uislamu usio na upendeleo, na wakayaona mambo yaliyowajibisha kuchukuliwa kwa hatua hii iliyotajwa kwenye maelezo ya kihistoria na katika Surah al–Tawbah, bila shaka wangelikutambua kule kutofahamu vipasikavyo na wangelithibitisha kwamba katu kitendo hiki si kinyume na msingi wa 'Uhuru wa Kuabudu' wenye kuheshimiwa na watu wote wenye hekima wa ulimwenguni humu. Zifuatazo hapa chini ndio sababu za kutolewa kwa agizo hili:

Wakati wa Zama za Ujinga ilikuweko desturi moja miongoni mwa Waarabu kwamba mtu yeyote aifanyaye Hija ya Ka'abah alimpa maskini vazi alilofanyia Tawaf (kuizunguka Kaabah). Kama mtu yule alikuwa na nguo moja tu, kwa kawaida aliazima nyingine na akaifanya Tawaaf nayo ili kwamba asiitoe ile nguo yake na kumpa maskini.

Na kama haikuwezekana kuazima nguo, basi ile Tawaaf ilifanywa uchi! Siku moja mwanamke mnene na mwenye sura ya kupendeza aliingia msikitini.

Kwa vile hakuwa na zaidi ya nguo moja, kwa kuitekeleza ile desturi ya imani potofu tu ya zama zile, alilazimika kufanya Tawaafu akiwa yu uchi. Ni dhahiri juu ya ni kiasi gani cha athari mbaya zitakazokuwa zimetolewa na ile Tawaf ya mwanamke aliye uchi katika sehemu ile takatifu mbele ya kundi la watu.

Sura al-Tawbah ilipofunuliwa, zaidi ya miaka ishirini ilikuwa imeshapita tangu Mtume (s.a.w.w.) aianze kazi ya kuulingania Uislamu, na katika kipindi hiki mantiki ya Uislamu yenye nguvu kuhusiana na kuizuia ibada ya masanamu, tayari imeshayafikia masikio ya washirikina wa Rasi ile. Hivyo basi, kama kulikuwako na kikundi kidogo tu kilichoung'ang'ania ushirikina na ibada ya masanamu, sababu yake ilikuwa ni ushupavu wa kidini na ukaidi wao tu.
Hivyo basi sasa wakati umefika kwamba Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) aitumie dawa ya mwisho katika kuitengeneza jamii, kuharibu sura zote za uabudu-masanamu kwa nguvu, kuichukulia (yaani hiyo ibada ya masanamu) kuwa ni uasi dhidi ya ubinadamu na kuangamiza chanzo cha mamia ya tabia nyingine mbaya kwenye jamii.

Hata hivyo, mustashirik ambao huchukulia kitendo hiki kuwa kinyume na kanuni za uhuru wa imani, ambao ni msingi wa Uislamu na msingi wa utamaduni wa siku hizi, wametupilia mbali jambo moja, nalo ni kuwa kanuni ya uhuru wa imani huheshimika tu pale usipoleta madhara katika ustawi wa mtu binafsi na jamii. Vinginevyo kwa mambo yanayopingana na akili na njia wanayoifuata wanafikra wa ulimwengu, haina budi kupingwa kwa nguvu zote.

Kwa mfano, katika Ulaya ya kisasa, kutokana na fikara zisizo sahi- hi baadhi ya watu wenye tamaa za kimwili hukiunga mkono chama cha wenye kukaa uchi kwenye jamii, na hoja iliyo ya kitoto (yaani, kuifunika sehemu ya mwili ni chanzo cha kichocheo na hivyo basi huyafisidi maadili) huunda vilabu vya siri na kuwa uchi humo mbele ya wenzao! Je, akili za mwanadamu zinaruhusu kwamba watu hawa waruhusiwe kuviendeleza vitendo vyao kwa dai la

'Uhuru wa Kuabudu' na iwe kwamba itikadi yao iheshimiwe? Au ni muhimu kwamba, ili kuuhami ustawi wa watu hawa pamoja na ule wa jamii, hatuna budi kupambana dhidi ya fikara hizi zilizo za kijinga kabisa?

Njia hii (yaani, kuuzuia ufisadi kwa nguvu) haitumiwi na Uislamu tu bali wenye hekima wa ulimwengu mzima hupambana mapam- bano makali dhidi ya fikra zenye madhara kwa maslahi ya jamii, na kwa kweli mapigano haya ni vita dhidi ya itikadi za kipumbavu za watu waliovunjika nyoyo. Ibada ya masanamu haikuwa chochote bali ni ukorofi wa ngano na itikadi zenye kuchekesha zilizoleta mamia ya tabia zenye kuchukiza kwenye mafundisho yake.

Na Mtume (s.a.w.w.) ameupa usikivu utoshelezao ule mwongozo wa waabudu masanamu. Hivyo basi, hivi sasa muda umeshawadia wa kuichukua hatua ya mwisho ambayo ni kuitumia nguvu ya kijeshi katika kukiangamiza hiki chanzo cha ufisadi.

Hijja ni moja ya masharti makuu ya imani ya ibada za Kiislamu na kaida za kidini, na hadi kwenye siku za kushushwa kwa Sura hii (*Tawba*), ugomvi na vita vilivyokuwepo baina ya Waislamu na machifu wa ushirik- ina havikuruhusu kwamba Mtume (s.a.w.w.) awafunze Waislamu kiviten- do zile ibada za Hijja kwa njia iliyo sahihi na rahisi. Hivyo, ilikuwa muhimu kwamba Mtume (s.a.w.w.) yeye mwenyewe binafsi ashiriki kwenye huu mkutano mkuu wa Kiislamu na kuwapa Waislamu mafunzo ya kivitendo jinsi ya

kuifanya ibada hii kuu. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) angeliweza kushiriki kwenye ibada hii pale tu Ka'abah tukufu na sehemu zinazoizunguka zitakapoachwa wazi na washirikina, na wakati Nyumba ya Allah itakapokuwa wazi kwa ajili ya wenye kumuabudu Allah na waja wake halisi tu.

Kutokana na sababu tatu tulizozitaja hapo juu, Mtume (s.a.w.w.) alimwita Abu Bakr na kumsomesha baadhi ya aya za mwanzoni za Sura al-Tawbah na kumuamrisha aende Makka pamoja na watu wengine arubaini1 na kuzisoma aya hizo zenye kufarakisha kutokana na ikirahi kwa waabudu masanamu katika siku ya *Idd al-Udh-ha*.

kama ilivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.) Abu Bakr alitoka na akaelekea Makka. Huku nyuma Malaika Mkuu Jibriil (a.s.) alikuja na kuleta ujumbe wa Allah usemao kwamba ile ikirahi kwa wenye kuayaabudu masanamu ni lazima itangazwe na Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe au na mtu atokanae naye.2 Hivyo Mtume (s.a.w.w.) alimwita Sayyidana Ali (a.s.) na kumwarifu jambo lile.

Kisha alimtoa mnyama wake maalum wa kupanda na kumpa Sayyidna Ali (a.s.) na kumwamrisha atoke Madina upesi iwezekanavyo ili amkute Abu Bakr mle njiani na azichukue zile aya kutoka kwake na akazisome yeye pamoja na lile tangazo lihitajikalo katika siku ya Idd Adhha mbele ya mkusanyiko mkuu ambao watu kutoka pande zote za Uarabuni watakuwa wakishiriki humo.

Mambo yaliyokuwamo kwenye tangazo hilo yalikuwa haya: Waabudu masanamu hawana haki ya kuiingia nyumba ya Allah. Kufanya Tawafu katika hali ya kuwa uchi kumepigwa marufuku. Hakuna mwaabudu masanamu atakayeruhusiwa kushiriki kwenye Hijja.

Kama watu fulani walifanya mapatano ya kutoshambuliana na Mtume (s.a.w.w.) nao wameyatekeleza majukumu yao chini ya mapatano hayo kwa ukamilifu basi mapatano hayo yaliyofanywa baina ya Mtume (s.a.w.w.) na watu hao yataendelea kuheshimiwa na uhai wao mali zao vitaheshimiwa hadi uishe muda wa mapatano hayo.

Hata hivyo, wale washirikina wasio na mapatano yoyote na Waislamu, au kivitendo wameyavunja masharti ya mapatano wanapewa muda wa miezi minne kuanzia leo (mwezi kumi Dhil Haj) kuueleza msimamo wao kuhusu serikali ya Kiislamu. Hawana budi kujiunga kwenye itikadi ya Upweke wa Allah (Waislamu) na kuiacha kila aina ya ushirikina au wajitayarishe kwa ajili ya vita.3

Amirul-Mu'minin (a.s.) alitoka na kwenda Makka akiwa amempanda yule mnyama maalum aliyepewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alifuatana na baadhi ya watu akiwemo Jaabir bin Abdullah Ansaari. Alimkuta Abu Bakr mahali paitwapo Juhfah na akampa ule ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.). Abu Bakr akampa Sayyidna Ali (a.s.) zile aya. Wanahadithi wa Kishia pamoja na wa Kisunni wengi wanamnukuu Sayyidna Ali (a.s.) kwamba amemwambia Abu Bakr: "Mtume amekupa uchaguzi wa kufuatana nami hadi Makka au kurudi Madina."

Abu Bakr alichagua kurudi, na baada ya kufika kwa Mtume (s.a.w.w.) alimwuliza akisema: "Ulinifikiria kuwa ninafaa kuitekeleza kazi ambayo watu wengine nao walikuwa na shauku ya kuitenda na kupata

utukufu kutokana nayo, lakini nilipokuwa bado ningali njiani uliniondolea kazi ile. Je, kuna lolote lililofunuliwa juu yangu?" Mtume (s.a.w.w.) alimjibu kwa upole akisema: "Alikuja Jibril na kuleta ujumbe wa Allah kwamba hakuna awezaye kulitekeleza jukumu hili ila mimi mwenyewe au mtu atokanaye na mimi. "4

Hata hivyo, kutokana na masimulizi ya Ahlus–Sunna inaonekana kwamba Abu Bakr aliishika ofisi ya ukaguzi wa ibada za Hijja ambapo Sayyidna Ali (a.s.) aliteuliwa kuzisoma tu zile aya za Allah na lile tangazo la Mtume (s.a.w.w.) mbele ya watu katika siku ya Mina.5

Amirul–Mu'minin aliwasili Makka. Siku ya kumi ya Dhil Haj aliipanda *Jamrah 'Aqibah* (Guzo la mwisho katika yale maguzo matatu ambayo Hujaji huyatupia kokoto saba kila moja), na akazisoma aya kumi na tatu za mwanzoni za *Surat al–Baraa'at*.

Vile vile alilisoma lile tangazo la Mtume (s.a.w.w.) kwa moyo uliojawa na ushujaa na nguvu na kwa sauti kuu iliyoweza kusikiwa na watu wote waliokuwepo pale, na kuwadhihirishia washirikina wasiokuwa na mapatano yoyote na Waislamu kwamba wanao muda wa miezi minne tu mbele yao, ambapo kwenye muda huo hawana budi kuyatoharisha mazingira yao kutokana na kila aina ya ufisadi na fikra zenye kukaidi, na wauache ushirikina na ibada ya masanamu, na wakishindwa kufanya huvyo, basi ule upendeleo wanaopewa utakomeshwa.

Athari za aya na tangazo hili zilikuwa kwamba ule muda uliotolewa wa miezi minne ulikuwa bado haujamalizika pale washirikina waliposilimu kwa makundi, ilipofika katikati ya mwaka wa kumi Hijiriya ibada ya masanamu ilifutiliwa mbali kabisa kwenye Rasi ya Uarabuni yote.

Chuki Mbaya Katika Kulitathmini Tukio Hili

Kumvua Abu Bakr jukumu la kwenda kuzisoma zile aya za Surat al– Baraa'at na kumteua Amirul–Mu'minin (a.s.) badala yake kwa kuafikiana na amri ya Allah, bila shaka hicho ni moja ya sifa bayana zisizokanushika za Sayyidna Ali (as). Hata hivyo, kikundi sha waandishi washupavu katika mambo ya dini wameyashika maoni ya ukaidi katika kulitathmini tukio hili.

Alipokuwa akilitathmini tukio hili, Alusi Baghdadi anasema kwenye *Tafsiri* yake hivi: "Abu Bakr alikuwa maarufu kwa huruma zake ambapo Ali alikuwa kinyume chake kwa sababu ya ushujaa na nguvu zake. Kwa kuwa kule kuzisoma zile aya za Sura al –BarA'at na kuwatisha washirikina kulihitaji ushujaa na nguvu za akili zaidi kuliko jambo lolote lile jingine na Ali alikuwa navyo vitu hivi zaidi kuliko Abu Bakr, hivyo, aliteuliwa badala yake."6

Maelezo haya yaliyosimuliwa katika msingi wa ushupavu wa dini hayalandani na kauli ya Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu alipokuwa akimjibu Abu Bakr alimwambia: "Wahyi wa Allah umeamrisha ya kwamba ni lazima aya hizi zisomwe na mimi mwenyewe binafsi au na mtu atokanaye na mimi." Hivyo basi huruma au ushujaa havina lolote kwenye jambo hili. Aidha, Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alikuwa

mdhihiriko kamili wa huruma.

Hivyo basi, kutokana na maelezo tuliyoyatoa hapo juu, Mtume (s.a.w.w.) naye asingelitakiwa kuwasomea watu aya za *Surat al–Baraa'at* yeye mwenyewe kwa sababu amri ya Allah ilikuwa kwamba yeye mwenyewe au mtu atokanaye na Ahlul Baiti wake alitekeleza jukumu hili. Alipokuwa akiifasiri Sura hii, Ibn Kathir Shaami, akiyafuata maoni ya Maqrizi, amelieleza jambo hili kwa njia nyingine, kwenye kitabu chake *Al– Imta'a* anaandika hivi: "Desturi iliyoko miongoni mwa Waarabu kuhusiana na kuyavunja mapatano ilikuwa kwamba mtu aliyemshirika kwenye mapatano yale, au mmoja wa wale wenye uhusianao naye, hana budi kuanza kuyavunja mapatano yale, na kama akishindwa kufanya hivyo, yale mapatano hubakia kuwa sahihi. Na kwa vile Ali alikuwa mmoja wa ndugu wa karibu wa Mtume (s.a.w.w.) aliwajibishwa kuzisoma aya hizi."

Hata hivyo, maelezo haya nayo si sahihi, kwa sababu miongoni mwa ndugu zake Mtume (s.a.w.w.) vile vile alikuwamo Abbas, ami yake ambaye uhusiano wake naye kwa vyovyote vile si mdogo kuliko ule wa Sayyidna Ali (a.s.). Hivyo basi, swali litabakia palepale kwamba, kwa nini jukumu hili hakupewa yeye Abbas?

Kama tukiombwa kutoa uamuzi usio na upendeleo juu ya tukio hili la kihistoria hatuna budi kusema kwamba huku kutolewa na kuteuliwa hakukutokana na nguvu ya roho ya Sayyidna Ali (a.s.) au uhusiano wake na Mtume (s.a.w.w.), lakini lengo halisi la badiliko hili lilikuwa kwamba kufaa kwa Amirul–Mu'minin (a.s.) kuhusu mambo yahusianayo na serikali ya Kiislamu hakuna budi kudhihirika kivitendo. Na watu hawana budi kutambua kwamba kutokana na fadhila na uwezo wa mtu binafsi, yeye yu mshirika na sahaba wa Mtume (s.a.w.w.).

Na kama baada ya muda utume utakoma, basi mambo ya kisiasa na mambo yenye kuhusiana na mamlaka ya ukhalifa hayana budi kushikwa na yeye, na hakuna mwingine afaaye zaidi kwa mamlaka haya ila yeye binafsi. Na baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) Waislamu wasipate taabu yoyote, kwa sababu wameona kwa macho yao wenyewe kwamba Sayyidna Ali (a.s.) ameteuliwa kwa amri ya Allah kuyatangua mapatano, na utenguzi ule ni haki pekee ya yule mtawala na mrithi wake tu.

---

1. Waaqidi ameitaja idadi yao kuwa ni watu mia tatu (Maghaazi–i Waaqidi, Juz. 3, uk. 1077).
2. Katika maelezo mengine, maneno 'au mtu atokanaye na Ahlul Bayt wako' hutokea (Siiratu Ibn Hisham Juz. 6, uk. 545 na Bihaarul–Anwaar, Juz. 21, uk. 267)
3. 'Furu' Kaafi, Juz. 1, uk. 326.
4. Al–Irshaad Mufid, uk. 33.
5. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 546.
6. Ruhul Ma'aani, katika tafsiri ya Sura al–Tawbah.

Sura Ya 57: Wawakilishi Wa Najraan Mjini Madina

Nchi yenye kupendeza ya Najraan iliyokuwa na vijiji sabini na viwili iko kwenye mpaka wa Hijaz na Yemen.

Katika siku za awali za Uislamu hili lilikuwa eneo pekee nchini Hijaz lililokuwa likikaliwa na Wakristo, ambao kwa sababu fulani fulani waliacha ibada ya masanamu na kuingia dini ya Ukristo.1

Sambamba na barua ambazo Mtume wa Uislamu aliwaandikia wakuu wa nchi mbalimbali za ulimwenguni, vilevile alimwandikia barua Abu Harith, Askofu wa Najraan, na kwa barua ile aliwalingania kwenye Uislamu watu wa eneo lile. Maneno ya barua ile yalikuwa hivi: “Kwa jina la Mola wa Ibrahim, Ishaaq, na Ya’aqub.

Hii ni barua itokayo kwa Muhammad Mtume na Mjumbe wa Allah iendayo kwa Askofu wa Najraan. Ninamsifu na kumtukuza Mola wa Ibrahim, Ishaaq na Ya’qub, na ninakuiteni nyote kumwabudu Allah badala ya kuviabudu viumbe Vyake, ili muweze kutoka chini ya ulinzi wa viumbe wa Allah na kuchukua nafasi chini ya ulinzi wa Allah Mwenyewe.

Na kama hamtaukubali mwito wangu, basi ni lazima (angalau) kulipa *Jizyah* (kodi) kwenye serikali ya Kiislamu (kwa malipo ambayo itachukua jukumu la kuhifadhi uhai na mali zenu), na mkishindwa kufanya hivyo, mnaonywa juu ya matokeo ya hatari.”2

Baadhi ya vitabu vya Kishia vinaongeza kusema kwamba, vilevile Mtume (s.a.w.w.) aliandika kwenye barua hii, aya ya Qur’ani ihusianayo na watu wa Kitabu ambayo ndani yake wote wameitwa kumwabudu Allah Aliye Mmoja tu. Hapa aya ya sitini na nne ya Sura Aali Imran ilizungumziwa:
“Sema: Enyi watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na ninyi: Ya kwamba tusimwabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote, wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa miungu badala ya Allah….”

Mjumbe wa Mtume (s.a.w.w.) aliwasili Najraan na kumpa yule Askofu ile barua. Aliisoma barua ile kwa uangalifu mkubwa, na kisha ili kuweza kutoa uamuzi, aliitisha mkutano wa viongozi wa kidini na wa kilimwengu ili awatake ushauri. Mmoja wa wale watu walioitwa kutoa ushauri alikuwa ni mtu mmoja aliyeitwa Shurahbil aliyekuwa maarufu kwa elimu wake, hekima na ujuzi.

Alipokuwa akimjibu yule Askofu, alisema hivi: “Ujuzi wangu wa mambo ya kidini ni haba mno, na hivyo basi mimi sina haki ya kuzitoa fikiza zangu juu ya mambo hayo, lakini kama ukinitaka ushauri juu ya mambo mengine yasiyokuwa haya ninaweza kutoa maoni yangu juu ya utatuzi wa tatizo hilo. Hata hivyo, ninalazimika kusema jambo moja ambalo ni kwamba kila mara tumekuwa tukisikia kutoka kwa

viongozi wetu kwamba kazi ya Utume itahamishwa kutoka kwenye kizazi cha Ishaaq kwenda kwenye kizazi cha Ismaili na kwamba si jambo lisilowezekana kwamba Muhammad ambaye yu kizazi cha Ismail, kuwa ndiye yule Nabii aliyeahidiwa!"

Ile halmashauri ya ushauri iliamua kwamba kikundi cha watu kiende Madina wakiwa ni wawakilishi wa Najraan ili waweze kuonana na Muhammad na kuzichunguza habari za Utume wake. Waliteuliwa watu sita waliokuwa wataalamu na wenye hekima zaidi kutoka miongoni mwa watu wa Najraan. Kikundi hiki kiliongozwa na viongozi wa kidini watatu ambao majina yao yalikuwa haya:

Abu Harith bin Alqamah, Askofu Mkuu wa Najraan aliyekuwa mwakilishi maalumu wa Kanisa Katoliki nchini Hijaz.

Abdul Masih, Mkuu wa kamati ya wawakilishi, aliyekuwa maarufu kwa hekima zake, busara na uzoefu.

Ayham, mtu mzima aliyekuwa akichukuliwa kuwa yu mtu mwenye kuheshimiwa wa jumuiya ya watu wa Najraan.3

Wajumbe hawa waliwasili msikitini wakati wa alasiri wakiwa wamevaa nguo za hariri, pete za dhahabu na misalaba shingoni mwao, wakamsalimu Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, hali yao yenye kuchukiza na isiyo sahihi, na pia ikiwa ni msikitini, ilimchukiza Mtume (s.a.w.w.). Walitambua kwamba wamemuudhi, lakini hawakuelewa ni kipi kilichomuudhi.

Hivyo basi, upesi sana walionana na Uthman bin Affan na Abdur-Rahman bin Awf, waliokuwa wakiwajua kabla ya hapo na wakawaeleza jambo lile. Uthman na Abdur-Rahman waliwashauri kwamba ufumbuzi wa tatizo lao uko mikononi mwa Sayyidna Ali bin Abu Twalib (as). Hapo wakakutana na Amirul-Mu'minin (a.s.), naye akiwajibu, akiwaambia: "Lazima mbadilishe mavazi yenu na kwenda kwa Mtume mkiwa mmevaa nguo zilizo rahisi na bila ya kuwa na mapambo yoyote yale. Hapo mtapata heshima na taadhima."

Wale wawakilishi wa Najraan wakavaa nguo rahisi na wakavua zile pete na kisha wakamjia Mtume (s.a.w.w.). Mtume (s.a.w.w.) akaijibu salam yao kwa heshima kuu na vilevile alizipokea baadhi ya zawadi walizozileta. Kabla ya kuanza kwa mazungumzo ya pande zote mbili wale wajumbe walisema kwamba muda wao wa sala ulikuwa umewadia, Mtume (s.a.w.w.) aliwaruhusu kusali sala zao msikitini mle wakizielekeza nyuso zao upande wa Mashariki.4

Wajumbe Wa Kutoka Najraan Wajadiliana Na Mtume (S.A.W.W.)

Idadi kubwa ya waandishi wa wasifu, wanahadithi na wanahistoria wa Kiislamu, wameyanukuu maneno ya mazungumzo baina ya wawakilishi wa Najraan na Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo, Marehemu Sayyid bin Taawus ameyanukuu maneno ya majadiliano yale na tukio la Mubahila (Maapizano) katika hali iliyo sahihi zaidi, kwa upana zaidi na kwa namna ya maelezo marefu zaidi, ukilinganisha na waandishi wengine. Ameyanukuu mambo yote na Mubahila tangu mwanzoni hadi mwishoni kutika kitabu kiitwacho

“*Kitabu Mubaahila’* cha Muhammad bin Abdul Muttalib Shabaan na *‘Kitab ‘Amaali Dhil Haj* cha Hasan bin Ismail.5

Hata hivyo, ni nje ya upeo wa kitabu hiki kutoa maelezo marefu ya tukio hili la kihistoria, ambalo kwa bahati mbaya hata halikudokezwa na baadhi ya waandishi wa wasifu. Kwa hiyo, tunataja hapa mambo machache juu ya mazungumzo yale, kama yalivyoelezwa na Halabi katika kitabu chake kiitwacho *Siiratu*.6

Mtume (s.a.w.w.): “Ninakuiteni kwenye dini ya Upweke wa Allah na ibada ya Allah Aliye Mmoja tu na kuzitii amri Zake.” Kisha Mtume (s.a.w.w.) akazisoma baadhi ya aya za Qur’ani mbele yao.

Wajumbe wa Najraan: “Kama Uislamu una maana ya kumwamini Mola wa Ulimwengu, sisi tayari tumeshamwamini na tunazitekeleza amri zake.”

Mtume (s.a.w.w.): “Uislamu una dalili chache na baadhi ya matendo yenu yanaonyesha kwamba hamuuamini Uislamu. Mnawezaje kusema kwamba mnamwanini Allah Aliye Mmoja tu na hali mnauabudu msalaba na hamjiepushi na nyama ya nguruwe na mnaamini kwamba Allah anaye mwana?”

Wajumbe wa Najraan: “Tunamwamini yeye (yaani Isa) kuwa yu mungu kwa sababu aliwafufua wafu, aliwaponya wagonjwa, alimtengeneza ndege kutokana na udongo na kumfanya aruke, na mambo yote haya yaonyesha kwamba yeye ni mungu.”

Mtume (s.a.w.w.): “Hapana! Yeye yu mja wa Allah naye yu kiumbe chake. Allah Alimweka kwenye tumbo la uzazi la Maryamu. Na uwezo na nguvu yote hii alipewa na Allah.”

Mjumbe mmoja: “Ndio! Yeye yu mwana wa Muumba, kwa sababu Maryamu alimzaa bila ya mume yeyote, na hivyo basi, ni muhimu kwamba baba yake ni Yeye yule Mola wa ulimwengu.”

Kufikia hapa, Malaika Mkuu Jibriil (a.s.) alishuka na kumshauri Mtume (s.a.w.w.) awaambie: “Kwa mujibu wa maoni hayo, hali ya Isa ni kama ile ya Adamu aliyeumbwa na Allah kwa nguvu Zake zisizo kifani, kutokana na udongo bila ya yeye kuwa na baba wala mama.7 Kama mtu kutokuwa na baba ni uthibitisho wa kuwa kwake mwana wa Mungu, basi Adamu anastahiki zaidi cheo hiki kwa sababu yeye hana baba wala mama.”

Wajumbe wa Najraan: “Maneno yako hayatutoshelezi. Njia iliyo bora zaidi ya kulitatua swali hili ni ile ya kwamba tufanye Mubahala (Maapizano) baina yetu katika muda utakaowekwa na kumlaani yule aliye mwongo baina yetu na tumwombe Allah kwamba Amwangamize yule aliye mwongo.”8

Wakati huo huo Malaika Mkuu Jibriil (a.s.) alikuja na akaileta ile Aya ihusianayo na Mubaahila na kuiwasilisha kwa Mtume (s.a.w.w.) amri ya Allah kwamba yeye Mtume (s.a.w.w.) afanye hicho kiapo na wale washindanao na kumbishia, na makundi yote mawili yaombe kwa Allah kwamba Amnyime yule mwongo baraka Yake. Qur’ani Tukufu inasema: “Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikia ilimu hii

waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wanawake zetu na wanawake zenu, na nafsi zetu na nyinyi nafsi zenu, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Allah iwashukie waongo." (***Sura Aali Imran 3:61***).

Pande zote mbili zilikubali kulitatua suala hili kwa njia ya kulaaniana, na iliamuliwa kwamba wote wajiweke tayari kwa ajili ya maapizano hayo katika siku inayofuata.

Mtume (S.A.W.W) Aenda Kwenye Maapizano

Tukio la Mubaahilah ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) na wajumbe wa Najraan ni moja ya matukio yenye kuvutia na mazuri sana ya historia ya Uislamu. Ingawa baadhi ya wanahadithi na waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) wameepuka kuzitaja taarifa zake kwa urefu na vilevile katika kulifafanua, lakini idadi yao kubwa kama vile Zamakhshari kwenye *Kashshaf,*9 Imamu Raza kwenye *Tafsiir*10 yake na Ibn Athir kwenye *Kaamil*11 wametamka kwa ufasaha zaidi kuhusu jambo hili. Tunanukuu hapa chini sehemu ya maelezo ya Zamakhshari kuhusu jambo hili.

"Muda wa Mubaahilah ukawadia Mtume (s.a.w.w.) na wajumbe wa ujumbe wa Najraan walikuwa wamekwisha kukubalina kwamba hafla ya Mubaahilah ifanyike mahali fulani nje kidogo ya mji wa Madina, kwenye jangwa. Mtume (s.a.w.w.) aliwachagua watu wanne tu wa kushiriki kwenye tukio hili muhimu mno miongoni mwa Waislamu na ndugu zake wengi. Watu hawa wanne walikuwa ni Ali bin Ali Twalib, Fatimah binti yake Mtume (s.a.w.w.), Hasan na Husein (a.s.), kwa kuwa miongoni mwa Waislamu wote hakuna nafsi zilizo safi zaidi ya hizi. Alitembea kutoka nyumbani kwake hadi kwenye ile sehemu iliyochaguliwa kwa ajili ya Mubaahilah kwa jinsi maalumu. Aliingia kwenye uwanja wa Mubaahilah akiwa amempakata Husain na kumshika Hasan kwa mkono wake, na Fatimah alikuwa akimfuatia, na Ali bin Abi Twalib alikuwa akiwafuatia nyuma yao.12

Kabla ya kuwasili kwenye ile sehemu ya Mubahilah aliwambia masahaba zake: "Dua yoyote nitakayoitamka ninyi hamna budi kuomba kutakabaliwa kwake na kusema: Amin."
Kabla ya kumkabili Mtume (s.a.w.w.) machifu wa wajumbe wa Najraan walikuwa wakiambiana: "Kama mkiona Muhammad amewaleta mashujaa na maafisa wake kwenye uwanja wa Mubahilah na kuuonyesha utukufu wake wa kidunia na nguvu ya nje, basi mfahamu kwamba lengo lake si la kweli na kwamba hauamini utume wake.

Hata hivyo, iwapo atakuja kwenye Mubahila pamoja na watoto wake, na walio wapenzi, na anakuja mbele ya Allah, Mwenye nguvu zote akiwa bila ya nguvu na utukufu wa kidunia, itakuwa na maana ya kwamba yu Mtume wa kweli na anayo imani kubwa sana na kujitegemea, kiasi kwamba sio tu kwamba yuko tayari kuangamia mwenyewe binafsi, bali yuko tayari kwa ujasiri kamili kuwafanya wale walio wapenzi wake nao kukumbwa na maangamizi na kutoweka."

Wakati wale machifu wa wajumbe walipokuwa wakijishughulisha na yale mazungumzo, Mtume (s.a.w.w.) alijitokeza kwa ghafla mbele ya Wakristo wa Najraan pamoja na watu wanne kutoka miongoni

mwa wale walio wapenzi wake zaidi, ambao watatu miongoni mwao walikuwa kizazi chake mwenyewe. Wote walishikwa na mshangao kuona kwamba amewaleta kwenye uwanja wa Mubaahilah hata watoto wasio na hatia wa binti yake mpenzi, na wakasema: “Mtu huyu anayo imani kamili katika mwito na dai lake kwa kuwa mtu mwenye mashaka hawaleti watu walio wapenzi wake zaidi kwenye sehemu ya ghadhabu ya Allah.”

Yule Askofu wa Najraan akasema: “Ninaziona nyuso ambazo kama wakiinua mikono yao na kuomba dua na kumwomba Allah kwamba mlima ulio mkubwa sana usogee kutoka kwenye sehemu yake, utasogea mara moja.

Kwa hali yoyote ile iwavyo tusijitie kwenye Mubahilah na watu hawa watakatifu na wachamungu, kwa sababu si jambo lisilowezekana kwamba tutaangamia, na vilevile ni jambo liwezekanalo kwamba ghadhabu ya Allah inaweza ikatanuka na kuuzingira ulimwengu mzima wa kikristo na asiwepo hata mkristo mmoja atakayebakia hai kwenye uso wa ardhi.”[13]

Wajumbe Wa Najraan Wajitoa Kwenye Mubahilah

Baada ya kuiona hali tuliyoitaja hapo juu, wale wajumbe wa Najraan walishauriana na wote kwa pamoja wakaamua ya kwamba wasishiriki kwenye Mubaahilah kwa vyovyote vile iwavyo. Vilevile walikubali kulipa kiasi kilichowekwa kwa kila mwaka ikiwa ni *Jizyah* na wakaomba kwamba badala ya malipo hayo, serikali ya Kiislamu ihifadhi uhai na mali zao. Mtume (s.a.w.w.) aliyakubali hayo na ikakubaliwa hivyo kuwa kwa malipo ya kiasi kile, wao wawe na haki ya kupata fursa zitolewazo na serikali ya Kiislamu. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Matatizo yameeneza kivuli chake cha ndege mbaya (kisirani) vichwani mwa wale wajumbe wa Najraan na kama wangeliamua kushiriki kwenye Mubaahila na kulaaniana wangelilipoteza umbile lao la kibinadamu na wangelichomwa kwenye moto uliokuwa ukiwashwa kule jangwani na mateso yangalienea hadi kwenye nchi ya Najraan.”

Imenukuliwa na Bibi Aisha kwamba, katika siku ya Mubaahilah Mtume (s.a.w.w.) aliwaweka dhuria wake wapenzi wanne chini ya shuka lake jeusi na akaisoma aya isemayo: **“…Hakika Allah Anataka kukuondoleeni uchafu enyi Ahlil-Bayti na kukutoharisheni kabisa kabisa…”**
(*Surat al- Ahzaab*, 33:33)

Kisha Zamakhshari anayataja mambo yahusianayo na ile aya ya Mubaahilah na mwishoni mwa mazungumzo yake anasema: “Tukio la Mubahilah na kiini cha aya hii ni ushahidi mkuu zaidi wa fadhila (ubora) za wale ‘watu wa shuka’ (*Ahlu'l-Kisaa*) na ni uthibitisho wa dhahiri wa usahihi wa Uislamu!”

Yaliyomo Katika Mkataba Uliofikiwa Kati Ya Pande Mbili Hizo

Wale wajumbe wa Najraan walimwomba Mtume (s.a.w.w.) kwamba, kile kima wapasikacho kulipa kila mwaka na usalama wa jimbo la Najraan viandikwe na yahakikishwe na Mtume (s.a.w.w.) kwenye hati. Amirul-Mu’minin aliwaandikia mkataba ule kama alivyoamrishwa na Mtume (s.a.w.w.), kama ifuatavyo:

“Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Huu ni hati itokayo kwa Muhammad Mjumbe wa Allah, kwa ajili ya watu wa Najraan na vitongoji vyake. Amri na uamuzi wa Muhammad juu ya mali na utajiri wote wa watu wa Najraan ni kwamba kila mwaka wataipa serikali ya Kiislamu nguo elfu mbili ambazo bei ya kila moja haitazidi dirhamu arobaini. Watakuwa huru kutoa nusu ya idadi hiyo kwenye mwezi wa Safar na ile nusu iliyosalia kwenye mwezi wa Rajab.

Na kama itakuwako hatari ya vita kutoka upande wa Yemen, wao (watu wa Najraan) ikiwa ni dalili ya ushirikiano wao na serikali ya Kiislamu, watatoa deraya thelathini, farasi thelathini na ngamia themanini kulipa jeshi la Uislamu kwa njia ya mkopo ulio dhaminiwa. Na vilevile watawajibikiwa kuwafanyia takrima wawakilishi wa Mtume (s.a.w.w.) kwenye jimbo la Najraan kwa kipindi cha mwezi mmoja. Aidha, atakapofika mjumbe wa Mtume (s.a.w.w.) nchini mwao, watampokea. Na uhai, mali, ardhi na sehemu za kuabudia za watu wa Najraan zitakuwa chini ya ulinzi wa Allah na Mtume Wake, ili mradi tu kwamba upesi sana wataacha kula rushwa. Na endapo watashindwa kufanya hivyo, Muhammad hatakuwa na jukumu lolote juu yao na hatawajibika kulitekeleza lolote katika aliyoyaahidi.”14

Mkataba huu uliandikwa kwenye ngozi nyekundu. Masahaba wawili wa Mtume (s.a.w.w.) wakatia saini zao chini yake wakiwa ni mashahidi na baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) akayatia muhuri. Mkataba huu wa amani ambao tafsiri yake imetolewa kwa mukhtasari hapo juu, huidhihirisha haki na usawa wa hali ya juu zaidi kama ulivyotekelezwa na Mtume (s.a.w.w.). Na unaonyesha kwamba Serikali ya Kiislamu haikuwa kama zilivyo nchi zenye nguvu za ulimwenguni zinazojinufaisha visivyostahili kutokana na unyonge wa watu wengine na kuwatoza kodi. Daima Uislamu ulizingatia moyo wa upatanishi na uadilifu na misingi ya ubinadamu; na daima ulikomesha hujuma.

Tukio la Mubaahila na aya iliyoshushwa kuhusiana nayo, vimekuwa ni fadhila kubwa zaidi na utukufu kwa Uislamu na wafuasi wa Ahlil Bayt (a.s.) kwenye kipindi chote cha historia, kwa sababu maneno na maelezo ya aya hii hukionyesha cheo cha juu zaidi walichokuwa nacho wale waliofuatana na Mtume (s.a.w.w.) kwenda kwenye sehemu ile iliyoteuliwa kwa ajili ya Mubaahila, kwa kuwa baada ya kuwaita Hasan na Husain wana wa Mtume (s.a.w.w.) na kumwita Bibi Fatimah (a.s.) kuwa mwanamke pekee wa nyumba yake, inamwita Sayyidna Ali (a.s.) ‘nafsi’ yaani nafsi hasa ya Mtume (s.a.w.w.). Ni heshima gani iwezayo kuwa kubwa zaidi ya hiyo kwa mtu yeyote yule?

Je aya hii si ushahidi wa fadhila za Amirul–Mu’minin (a.s.) juu ya Waislamu wengine wote wa humu ulimwenguni? Fakhri Razi, ambaye msimamo wake juu ya majadiliano ya hali ya theolojia na mambo yahusianayo na Uimamu ni maarufu, amezitaja hoja za Kishia na ameyamalizia majadiliano hayo kwa ukinzani ulio dhaifu na mdogo. Jibu lake ni dhahiri kabisa kwa watu wenye fikira zisizo na upendeleo.

Imefahamika kutokana na maelezo yaliyonukuliwa kutoka kwa viongozi wetu wa kidini kwamba, Mubaahila si hususani kwa Mtume (s.a.w.w.) tu, kila Mwislamu anaweza kupambana na mpinzani wake kwa njia hii.

Dua zinazohusiana nayo zimeandikwa kwenye vitabu vya Hadith, na kitabu kiitwacho *'Nuruth-Thaqalayn'* kinaweza kurejewa katika kupata taarifa zaidi.15 Kwenye kijitabu kilichoandikwa na mwalimu mheshimiwa Allamah Tabatabai tunasoma hivi: "Mubaahilah ni moja ya miujiza ya kudumu ya Uislamu na kila Muumini wa kweli anaweza kupambana na mpinzani wake kwa njia ya Mubaahilah ili kuuthibitisha ukweli wa Uislamu, kwa kumfuata kiongozi wa kwanza wa dini hii, na anaweza kumwomba Allah kumwadhibu mpinzani yule na kumlaani."16

---

1. Yaqut Hamawi ameieleza sababu ya kuingia kwao Ukristo kwenye kitabu chake kiitwacho Majma'ul Buld?n, Juz. 5, uk. 266-267.
2. Al-Bidayah Wan-Nihayah, uk. 54 na Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 285.
3. Tarikhu Yaqubi, Juz. 2, uk. 66.
4. Siiratu Halabi, Juz.3, uk. 239.
5. Maelezo kwa kirefu ya tukio hili la kihistoria yameelezwa kwenye kitabu kiitwacho 'Iqbal' cha marehemu Ibn Taawusi, uk. 496-513.
6. Siiratu Halabi, juz. 3, uk. 239.
7. Hii ndio maana ya Aya: "Hakika mithili ya Isa mbele ya Allah ni kama mithili ya Adamu; Alimuumba kutokana udongo, kisha akamwambia kuwa na akawa." (Surah Aali Imran, 3:59)
8. Bihaarul-Anwaar, Juz. 21, uk. 32 kama ilivyonakiliwa kutoka 'Al-Iqbal' cha Ibn Taawus. Hata hivyo kutoka kwenye 'Siirah Halabi' tunajifunza kwamba Mubaahila ulipendekezwa na Mtume (s.a.w.w.)mwenyewe.
9. Kashaf, Juz. 1, uk. 282-283.
10. Tafsiirul-Mafaatihul Ghayb, Juz. 2, uk. 481-482.
11. Tarikhul-Kamil, juz. 2, uk. 112.
12. Kwenye maelezo mengine imeelezwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa ameishika mikono ya Hasan na Husain na Sayyidna Ali (as) alikuwa mbele ya Mtume (s.a.w.w.) na Fatimah alikuwa akifuatia nyuma ya Mtume (s.a.w.w.). Bihaarul Anwaar, Juz. 21, uk. 338.
13. Ibn Taawus ananakili hivi kutoka kitabu 'Al-Iqbal': Kwenye siku ya Mubaahilah idadi kubwa ya Muhajiriin na Ansar walijikusanya karibu na ile sehemu ambapo Mubaahila ulikuwa ufanyike. Hata hivyo, Mtume alitoka nyumbani kwake na wale watu wanne tuliowataja hapo juu tu na hakuna yeyote miongoni kwa Waislamu aliyekuwako pale kwenye ile sehemu iliyoteuliwa kwa ajili ya kazi ile ila hawa watu watano. Mtume (s.a.w.w.) alilivua joho lake kutoka mabegani mwake na kulitanda kwenye miti miwili iliyokuwa karibu karibu. Kisha akakaa chini ya kivuli cha joho lile pamoja na wale wajumbe wa Najraan kwenye Mubaahilah.
14. Futuhul Buldaan, uk. 76.
15. Nuruth-Thaqalayn, Juz. 1, uk. 291-292.
16. Maudhui hii imefafanuliwa kwenye baadhi ya masimulizi ya Kiislamu. Kuhusiana na jambo hili, rejea kwenye Usulul Kaafi' Kitabu cha Dua, Sura ya Mubaahilah uk. 538.

Sura Ya 58: Matukio Ya Mwaka Wa Kumi Hijiriya

Tangazo kali na chungu lililosomwa na Amirul-Mu'minin kwenye majira ya Hijja kwenye mwaka wa tisa Hijiriya kule Mina kwa niaba ya Mtume (s.a.w.w.), na tangazo rasmi alilotoa yeye kwamba Allah na

Mtume Wake wanachukizwa na waabudu masanamu na wao (waabudu masanamu) waamue mara ya kwanza na ya mwisho katika kipindi cha miezi minne kusilimu na kuiacha ibada ya masanamu au kuwa tayari kwa vita kamili, lilikuwa na athari za kina na za haraka zaidi.

Makabila ya Waarabu wa mikoa mbalimbali ya Uarabuni ambayo hadi hapo walikuwa tayari wameshakataa kuzikubali hoja za Qur'ani na sheria za Allah kutokana na uadui na mfundo, na kung'ang'ania katika kuzishikilia desturi zao zilizo mbaya na chafu, mapokeo ya itikadi za kijinga na ibada za mawe na udongo, sasa wakabaki bila ya msaada wowote na wakaanza kuwapeleka wajumbe wao kwenye makao makuu ya Uislamu (Madina). Kila mmoja wa wajumbe hawa alikuwa na majadiliano na mazungumzo na Mtume (s.a.w.w.).

Ibn Saad kwenye kitabu chake *Tabaqaatul–Kubra*1 amesimulia taarifa za watu sabini na wawili miongoni mwao. Kuwasili kwa wawakilishi hawa kwa wingi na pia kwamba baada ya kutamka ile shahada, huonyesha kwamba mwanzoni mwa mwaka wa kumi wa Hijiriya, haikuweko ngome ya kutegemewa iliyoachwa kwa washirikina wa Uarabuni, vinginevyo wangelikimbilia huko na kupigana vita dhidi ya Waislamu kwa kushirikiana wao kwa wao.

Kile kipindi cha miezi minne kilikuwa bado hakijapita wakati pale Hijaz nzima ilipokuja chini ya bendera ya Uislamu na halikubakia humo hekalu hata moja la masanamu au sanamu au mwaabudu masanamu, kiasi kwamba idadi ya watu wa Yemen, Bahrain na Yamamah nao walisilimu.

Njama Ya Kumuuwa Mtume (S.A.W.W)

Machifu wa makabila ya Bani 'Aamiri walikuwa maarufu mno miongoni mwa makabila ya Kiarabu kwa ukaidi na uasi wao. Watu watatu kutoka miongoni mwa machifu wao walioitwa 'Amir, Arbad na Jabbar waliamua kuja Madina wakiuongoza ujumbe hasa kwa nia ya kutaka kumuuwa Mtume (s.a.w.w.) wakati wakiwa wanafanya majadiliano naye kwenye mkutano. Mpango wao ulikuwa kwamba 'Amir ajishughulishe na majadiliano na Mtume (s.a.w.w.) na wakati yale mazungumzo yao yakiwa yanaendelea, Arbad amshambulie Mtume kwa upanga wake na kumuuwa.

Wale wajumbe wengine ambao hawakuujua mpango ule wa wale watu watatu, waliutangaza uaminifu wao kwa Uislamu na Mtume (s.a.w.w.). Hata hivyo 'Amir alikataa kuonyesha mwelekeo wake kwenye Uislamu na kumwambia Mtume (s.a.w.w.) kwa kurudia rudia kwamba: "Ninataka kuzungumza nawe kwa siri." Kila alipoitamka kauli hii alikuwa akimtazama yule Arbad. Hata hivyo, ingawa aliutazama uso wake kwa makini, alimwona kuwa katulia na shwari. Mtume (s.a.w.w.) alimjibu akisema: "Jambo hili haliwezekani mpaka pale utakaposilimu (yaani kule kuonana nawe ukiwa peke yako)"

Hatimaye Amir aliyapoteza matumaini yote ya kupata msaada wa Arbad katika kufaulu kwa mpango wao. Inaonekana kwamba pale Arbad alipodhamiria kuuweka mkono wake kwenye ule upanga wake alikumbwa na hofu, na ukuu wa Mtume (s.a.w.w.) ulimzuia (yeye Arbad) kuutimiza mpango ule. Ule mkutano ulipomalizika, Amir alisimama pale alipokuwapo akatangaza uadui wake kwa Mtume (s.a.w.w.)

na akasema: “Nitaijaza Madina kwa farasi na askari kukudhuru.”

Hata hivyo Mtume (s.a.w.w.) kutokana na uvumilivu mkubwa aliokuwa nao, hakumjibu bali alimwomba Allah amlinde kutokana na uasi wa wale watu wawili. Dua ya Mtume (s.a.w.w.) ilitakabaliwa upesi sana. ‘Aamir alipata mashambulizi ya tauni alipokuwa njiani na akafa katika hali mbaya mno nyumbani mwa mwanamke mmoja wa kabila la Bani Salul. Ama kuhusu yule Arbad, alipigwa na radi akiwa jangwani na akaugua hadi akafa. Na maamuru waliyoyapata watu hawa waliopanga mpango mbaya dhidi ya Mtume (s.a.w.w.) yaliimarisha zaidi imani ya watu katika Uislamu.2

Amirul-Mu’minin Atumwa Yemen

Kusilimu kwa watu wa Hijaz na usalama aliouhisi Mtume (s.a.w.w.) kutoka kwenye upande wa makabila ya Kiarabu vilimwezesha kuendeleza ushawishi wa Uislamu hadi kwenye maeneo ya jirani na Hijaz. Hivyo basi, kwa mara ya kwanza alimpeleka mmoja wa masahaba zake wenye hekima aliyeitwa Mu’aaz bin Jabal Yemen ili akawaeleze Uislamu watu wa eneo lile.

Alipokuwa akimpa maelekezo kwa kirefu Mtume (s.a.w.w.) vilevile alimwambia Mu’aaz; “Jiepushe na kuwa mkali kwa watu na uwajulishe neema ya Allah iliyoko kwa ajili ya waumini wa kweli. Utakapokutana na watu wa Kitabu huko Yemen na wakakuulizia kuhusu ufunguo wa Peponi basi waambie kwamba ni utambuzi wa Upweke na kutokuwa na kifani kwa Allah.”

Mu’aaz hakuweza kutoa jibu la kutosheleza alipoulizwa kuhusu haki za Mume kwa mkewe.3
Hivyo basi, Mtume (s.a.w.w.) akaamua kumpeleka sahaba wake mwenye fadhila zaidi, Sayyidna Ali (a.s.) kwenda Yemen ili Uislamu uweze kuendelea huko chini ya mafundisho yake, hoja zake za kimantiki, nguvu za mikono yake na ushujaa wake usio kifani na uhodari.

Aidha, Khalid bin Walid naye alipelekwa na Mtume (s.a.w.w.) nchini Yemen wakati fulani kabla ya Sayyidna Ali (a.s.)4 ili akaviondoe vizuizi zilivyokuwako kwenye njia ya uendelezaji wa Uislamu kwenye eneo lile. Hata hivyo, hakuweza kufanya jambo lolote lile kuhusiana na kazi hii katika kipindi kile.

Hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alimwita Sayyidna Ali (as) na akamwambia: “Ewe Ali! Ninakupeleka Yemen ili ukawalinganie wakazi wake kwenye Uislamu na kuwajulisha Amri za Allah pamoja na mambo yaliyo halali na yaliyo haramu.

Wakati wa kurejea kwako Madina, ukusanye Zaka kutoka kwa watu wa Najraan pamoja na kodi wapasikayo kulipa na kuiweka kwenye hazina ya Umma.”

Sayyidna Ali (a.s.) alimjibu Mtume (s.a.w.w.) kwa heshima mno, kwa maneno haya: “Mimi bado ni kijana, maishani mwangu mwote bado sijawahi kupatanisha na katu sikupata kukikalia kiti cha hakimu.” Mtume (s.a.w.w.) aliubandika mkono wake kifuani mwa Sayyidna Ali (a.s.) na kumwombea kwa maneno haya: “Ee Allah! Uongoze moyo wa Ali na uhifadhi ulimi wake kutokana na makosa.” Kisha akasema: “Ewe Ali! Usigombane na yeyote yule na jaribu kuwaongoza watu kwenye njia iliyonyooka kwa hoja na

tabia njema.
Ninaapa kwa jina la Allah! Kama Allah anamwongoza mtu kwenye njia iliyonyooka kupitia kwako, ni bora zaidi kuliko vile viangazwavyo na jua.”

Mwishoni Mtume (s.a.w.w.) alimpa Sayyidna Ali (a.s.) mapendekezo manne: Kuifanya Sala na kumtukuza Allah ni kazi yako kwa sababu Sala ni yenye kutakabaliwa. Kuwa mwenye shukrani kwa Allah kwenye hali zote, kwa sababu shukrani huongeza baraka. Kama ukifanya mapatano na mtu, au kikundi cha watu yaheshimu. Jiepushe na kuwahadaa watu, kwa sababu udanganyifu wa watenda maovu unawarudia wao wenyewe.

Sayyidna Ali (a.s.) kwenye kile kipindi cha kukaa kwake nchini Yemen alikata hukumu zenye kustaajabisha ambazo nyingi kati ya hizo zimerekodiwa kwenye vitabu vya historia. Mtume (s.a.w.w.) hakutosheka na mwongozo ule, bali vile vile aliwaandikia barua watu wa Yemen akiwaita kwenye Uislamu akampa Sayyidna Ali (as) barua ile na akamwelekeza kwenda kuwasomea.

Bara’ bin Azib alikuwa mhudumu wa Sayyidna Ali (a.s.) kule nchini Yaman. Anasema kwamba Sayyidna Ali (a.s.) alipofika kwenye mpaka wa Yemen, alizipanga safu za askari wa Uislamu waliokuwa tayari wameshapelekwa kule chini ya uongozi wa Khalid bin Walid na akasali sala ya jamaa ya alfajiri pamoja nao. Kisha akaliita kabila la Hamdan lililokuwa moja ya makabila makuu zaidi ya Yemen, kuusikia ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.).

Kwanza alimtukuza Allah. Kisha akawasomea ujumbe wa Mtume (s.a.w.w.). Utukufu wa mkutano ule, utamu wa maelezo na ukuu wa maneno ya Mtume (s.a.w.w.) valiwavutia mno watu wa kabila la Hamdan kiasi kwamba walisilimu katika siku moja. Imamu Ali (a.s.) alimwandikia barua Mtume (s.a.w.w.) akimweleza maendeleo yaliyopatikana. Mtume (s.a.w.w.) alifurahi sana kuzisikia habari njema. Alimshukuru Allah akasema: “Na libarikiwe kabila la Hamdan.” Kusilimu kwa kabila la Hamdan ilikuwa chanzo cha watu wengine wa Yemen kusilimu upesi sana.5

---

1. Tabaqaatul-Kubra, Juz. 2, uk. 230-291.
2. Siiratu Ibn Hisham Juz. 2, uk. 568-569.
3. Siiratu Ibn Hisham Juz. 2, uk. 590.
4. Sahih Bukhari, Juz. 5, uk. 163.
5. Tarikhul-Kamil, Juz. 2, uk. 305; Bihaarul-An’waar, Juz. 21, uk. 360-363.

Sura Ya 59: Hijja Ya Mwago

Miongoni mwa kanuni za jamaa za ibada za Uislamu, kaida za Hijja ndizo ibada zilizo kuu na tukufu

zaidi, kwa sababu kuzitekeleza kaida hizi na kwamba pia ni mara moja kwa mwaka ni udhihirisho mtukufu wa umoja na ushirikiano, ishara kamili ya uhuru kuanzia mali na mahali, na ni mfano mashuhuri zaidi wa usawa baina ya matabaka mbalimbali ya watu, na chanzo cha kuimarisha uhusianao baina ya Waislamu n.k. Sasa, kama sisi Waislamu tukiitumia kwa kiasi kidogo tu ile nafasi tuipatayo katika Hijja kwa ajili ya kuitengeneza hali yetu, na hatimaye kuubadili huu mkutano wa Kiislamu wa kila mwaka (ambao bila shaka unaweza kutatua mengi ya matatizo ya kijamii na unaweza kuleta mabadiliko kwenye maisha yetu) bila ya kupata faida zenye kustahili kutokana nao, si kwa sababu ya kwamba sheria ya Hijja ina upungufu bali kosa litakuwa liko kwa viongozi wa Kiislamu ambao hawaitumii vizuri sherehe hii kubwa.

Tangu siku ile Nabii Ibrahim (a.s.) alipoijenga Ka'abah na kuwaalika wenye kumwabudu Mungu Mmoja kuja kufanya Hija yake, daima sehemu hii imekuwa kituo chenye kuvutia, ambapo Tawaaf ilikuwa ikifanywa na watu wachamungu na kila mwaka makundi ya mahujaji yalikuja hapo kutoka sehemu mbalimbali za Uarabuni na kutoka kwenye pembe zote ulimwenguni kuja kufanya Hija ya Nyumba hii, nao walizitekeleza ibada walizofundishwa na Nabii Ibrahimu (a.s.).

Hata hivyo, kama matokeo ya kadiri muda ulivyopita, na vilevile kwa sababu ya watu wa Hijaz kukosa mwongozo wa Mitume, choyo cha Waquraishi, na utawala wa masanamu juu ya ulimwengu wa Kiarabu, ibada za Hijja zilipatwa na mabadiliko kutokana na mtazamo wa nyakati na mahali, na hatimaye kupoteza sura yake halisi.

Kwa sababu hizi Mtume (s.a.w.w.) aliamrishwa na Allah katika mwaka wa kumi hijiriya kushiriki kwenye ibada za Hijja yeye mwenyewe binafsi ili kwamba aweze kuwafunza watu kivitendo majukumu yao na kuweza kuyatupilia mbali desturi za kale na zisizohitajika za ibada hii, na vilevile kuwafunza watu kuhusu mipaka ya Arafat na Mina na kuwaambia kuhusu muda wa kuondoka kwenye sehemu hizo. Hivyo basi, ikilinganishwa na hali yake ya kisiasa na kijamii, safari hii ina hali ya kielimu iliyo kuu sana.

Katika mwezi wa kumi na moja wa Kiislamu (Dhil–Qa'adah) Mtume (s.a.w.w.) alitoa amri itangazwe mle mjini Madina pamoja na miongoni mwa makaliba kwamba, alidhamiria mwaka ule kufanya Hijja ya Ka'abah. Taarifa hii ilizaa shauku kubwa kwenye umma wa Kiislamu. Maelfu ya watu waliyakita mahema nje ya mji wa Madina na kusubiri kuondoka kwa Mtume (s.a.w.w.).1

Mtume (s.a.w.w.) alimteua Abu Dujanah kuwa mwakilishi wake mjini Madina na yeye mwenyewe akaondoka kwenda Makka mnamo tarehe ishirini na nane Dhil–Qa'adah akichukua wanyama sitini wa kutoa kafara. Alipofika Dhil Hulayfah alivaa Ihram kwenye Masjid Shajarah, iliyokuwa ni shuka mbili nyeupe. Na alipokuwa akivaa ile Ihram aliisoma dua maarufu inayoanza na neno *Labbayk* ambalo ni jibu la mwito wa Nabii Ibrahim (a.s.).

Alisema *Labbayk* kila mara alipomwona mtu aliyempanda mnyama au alipofika kwenye sehemu iliyoinuka au iliyo chini. Alipofika karibu na mji wa Makka aliacha kulitamka lile neno *Labayk*. Aliwasili Makka mnamo mwezi nne Dhil Hajj na akaenda moja kwa moja hadi Masjid Haraam, akaingia humo

kupitia kwenye lango la Bani Shaybah. Kisha akaanza kumtukuza Allah na kuomba baraka kwa ajili ya Nabii Ibrahimu (a.s.).

Wakati wa kufanya Tawaaf, alisimama upande wa pili wa Hajarul Aswad (Jiwe Jeusi). Mara ya kwanza aliitekeleza 'Istilaam'2 yake na kisha akaizunguka Ka'abah mara saba. Baada ya hapo alisimama nyuma ya *Maqaamul–Ibrahim* na kusali sala ya Tawaaf yenye rakaa mbili. Baada ya sala ile alianza kufanya Sai baina ya Safa na Marwah.3

Kisha aliwageukia mahujaji na akasema: "Wale wasioleta wanyama wa kutoa kafara wajitoe kwenye hali ya Ihram, na mambo yote yaliyoharimishwa kwao (katika wakati wa Ihram) yatawahalalikia kwa Taqsiir (kupunguza nywele na au kukata kucha). Hata hivyo, mimi na wale wengine tulioleta wanyama wa kutoa kafara tutasalia kwenye hali ya Ihram hadi pale tutakapowachinja wanyama wetu kule Mina."

Jambo hili lilikuwa na uzito mkubwa kwa baadhi ya watu, na udhuru walioutoa ulikuwa kwamba hawakupenda kwamba Mtume (s.a.w.w.) abakie kwenye hali ya Ihram na wao waitoke hali ile, na yale mambo yaliyoharimishwa kwake yawe halali kwao. Wakati fulani walisema: "Si sahihi kwamba sisi tuwe mahujaji wa Nyumba ya Allah na matone ya maji ya udhu yamiminike kutoka vichwani na shingoni mwetu."4
Mtume (s.a.w.w.) alibahatika kumwona Umar aliyekuwa bado yu mwenye hali ya Ihram na akamwuliza kama alileta mnyama wa kutoa kafara. Alijibu "la", hapo Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Basi ni kwa nini hutoki kwenye hali ya Ihram?" Alimjibu: "Sipendelei kwamba mimi nitoke kwenye hali ya Ihramu na wewe uendelee kuwa kwenye hali hiyo hiyo." Mtume (s.a.w.w.) akamwambia: "Utaendelea kuishikilia imani yako hii si hivi sasa tu, bali hadi kwenye siku ya kufa kwako."

Mtume (s.a.w.w.) aliudhishwa na shaka na kutoamua kwa watu na akasema: "Kama hali ya baadae ingalikuwa dhahiri kwangu kama ilivyo kale, na nikawa nimetambua kusita na mashaka yenu yasiyothibitika, Mimi nami ningalikuja kwenye hija ya Nyumba ya Allah bila ya mnyama wa kutoa kafara kama hivyo mlivyo. Hata hivyo, sina la kufanya hivi sasa, kwa sababu nimekuja na wanyama wa kutoa kafara na kwa mujibu wa Amri ya Allah, "Hadi pale kafara itakapofika kwenye sehemu yake" Sina budi kubakia kwenye hali ya Ihram hadi nitakapowachinja wanyama hao kwenye kiwanja cha kutolea kafara cha Mina. Hata hivyo, kila mtu asiyeleta mnyama wa kutoa kafara hana budi kutoka kwenye Ihram na kulichukulia kila jambo alilolitenda kuwa ni Umrah na baada ya hapo hana budi kuvaa Ihram kwa ajili ya Hajj. 5

Saidina Ali (A.S) Arejea Kutoka Yemen Ili Ashiriki Kwenye Ibada Ya Hijja

Amirul–Mu'minin alitambua kuondoka wa Mtume (s.a.w.w.) kwenda kufanya Hijja. Yeye naye aliondoka na kwenda Makka pamoja na askari wake ili kufanya Hijja na akachukuwa wanyama wa kutoa kafara thelathini na wane. Vilevile alileta vile vipande vya nguo alivyovikusanya kutoka kwa watu wa Najran

kutokana na ule ushuru ulioafikiwa kwenye mapatano tuliyoyataja kwenye sura ya hamsini na saba. Alipokuwa njiani alimpa afisa wake mmoja uongozi wa jeshi lake na yeye mwenyewe akaharakisha kwenda Makka. Alionana na Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa na furaha kuu kumwona na akamwuliza: “Ulinuia vipi? “ Sayyidna Ali (a.s.) akamjibu hivi: “Katika wakati uliofaa kwa kuvaa Ihraam nilivaa Ihram kwa nia yako na nikasema: “Ee Allah! mimi nami ninavaa Ihram kwa nia ile ile ambayo Mtume Wako amevalia Ihraam yake. “

Kisha alimfahamisha Mtume (s.a.w.w.) kuhusu wale wanyama wa kutoa kafara aliowaleta. Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Wajibu wetu sote kwenye jambo hili ni moja tu na hatuna budi kubakia kwenye hali ya Ihram hadi pale tutakapowachinja wale wanyama wa Kafara.” Kisha Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Sayyidna Ali (a.s.) kuwarudia wale askari wake na kuwaleta Makka.

Sayyidna Ali (a.s.) alipolifikia jeshi aliona kwamba vile vipande vya nguo vyote alivyovikusanya kutoka kwa watu wa Najraan kufuatana na mapatano yaliyofanywa kwenye ile siku ya Mubaahila, vimeshagawanywa miongoni mwa wale askari, na walikuwa wamevivaa kwa namna ya Ihraam. Ali alikasirishwa sana na kile kitendo cha yule mwakilishi wake pale yeye alipokuwa hayupo, akamwambia: “Kwa nini umevigawa hivi vipande vya nguo miongoni mwa askari kabla sijavifikisha kwa Mtume (s.a.w.w.)? “Alijibu akisema: “Walishikilia kwamba niwaazime hivi vipande vya nguo, na nivichukue baada ya kufanya ibada ya Hajj.” Sayyidna Ali (a.s.) akamwambia: “Wewe hukupewa mamlaka ya kufanya hivyo.” Kisha alivichukua vile vipande vya nguo kutoka kwa askari wale, akavifungasha na kuvipeleka kwa Mtume (s.a.w.w.) kule mjini Makka.

Watu ambao uadilifu na nidhamu ni vitu vinavyouma, na wapendao kwamba daima matukio yatokee kama wapendavyo wao, walimwendea Mtume (s.a.w.w.) na kumwelezea kuudhishwa kwao na kule kuvichukua vile vipande vya nguo alikofanya Sayyidna Ali (as). Mtume (s.a.w.w.) alimtuma mmoja wa masahaba wake kuwaendea wale walalamikaji na kuwafikishia ujumbe wake usemao: “Jiepusheni na kumsema Ali kwa ubaya. Yeye yu hodari katika kuzisikiliza sheria za Allah na wala yeye si mwenye kujipendekeza.”6

Ibada Za Hijja Zaanza

Kaida za Umrah zikamalizika, Mtume (s.a.w.w.) hakuelekea kukubali kukaa nyumbani mwa mtu yeyote baina ya kipindi cha ibada za Umrah na zile za Hajj. Hivyo basi aliamrisha likitwe hema lake nje ya mji wa Makka.

Siku ya nane ya Dhil Hajj ikafika. Katika siku hiyo hiyo, mahujaji wa Nyumba ya Allah walitoka Makka kwenda Arafat ili kwenda kutekeleza kaida za ‘Arafat tangu adhuhuri ya mwezi tisa Dhil Hajj hadi jua kuchwa katika siku ile.

Mnamo mwezo nane Dhil Hajj, ambayo vilevile huitwa siku ta *‘Tarwiyyah,”* Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Arafat kupitia Mina na akakaa Mina hadi jua lilipochomoza mnamo mwezi tisa Dhil Hajj. Kisha

akampanda ngamia wake na akaondoka kwenda Arafat na akashukia mahali paitwapo Numrah lilipokitwa hema lake. Akauhutubia mkusanyiko mtukufu uliokuwapo pale, aliitoa hotuba yake ya kihistoria akiwa amempanda ngamia wake.

Hotuba Ya Kihistoria Ya Mtume (S.A.W.W) Wakati Wa Hijja Yake Ya Kuaga

Siku ile, Arafat ilishuhudia mkusanyiko mkuu na mtukufu, ambao hadi siku ile mfano wake haukupata kuonwa na watu wa Hijaz. Sauti ya Upweke wa Allah na hamasa ya ibada ya Allah Mmoja tu zilikuwa zikilia nchini. Sehemu ambayo hadi muda mfupi tu uliopita ilikuwa makazi ya washirikina na waabudu masanamu ikawa daima kituo kikuu cha wenye kumwabudu Allah Mmoja. Mtume (s.a.w.w.) akasali sala yake ya Adhuhuri na ya al-Asri hapa Arafat pamoja na watu 100,000, na hapo ushindi wa Uislamu juu ya ukafiri ukapatikana.

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) alimpanda ngamia wake na akatoa hotuba yake ya kihistoria iliyorudiwa na mmoja wa masahaba wake aliyekuwa na sauti kubwa, ili kwamba wale waliokuwa mbali nao waweze kukielewa kile alichokuwa akikisema. Katika siku ile alianza hotuba yake kwa kusema: “Enyi watu! Yasikilizeni maneno yangu, kwa vile yawezekana kwamba nisikutane nanyi mahali hapa wakati ujao.

Enyi watu! Damu yenu na mali zenu (heshima na sifa)7 ni vyenye kuheshimiwa miongoni mwenu, kama ilivyo siku hii na mwezi huu, hadi siku ambayo mtakutana na Allah, na kila uasi katika jambo hili ni haramu.”

Ili kuthibitisha kwamba watu wanalipata wazo lihitajikalo kutokana na maneno yake kuhusu kuheshimika kwa uhai na mali za Waislamu, Mtume (s.a.w.w.) alimwomba Rabi’ah bin Umayyah awaulize hivi: “Ni mwezi gani huu?” Wote walijibu wakisema: “Ni mwezi wenye kuheshimiwa na kupigana katika mwezi huu kumekatazwa na ni haramu.” Kisha Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Rabiah: “Waambie: Allah Ametangaza kwamba damu yenu na mali zenu ni haramu na ni vyenye kuheshimika juu ya kila mmoja wenu kama ulivyo mwezi huu hadi pale mtakapoutoka ulimwengu huu.”

Akamwambia tena Rabiah: “Waulize ni ardhi gani hii?” Wote wakajibu “Ni ardhi yenye kuheshimika na umwagaji wa damu na uasi ndani yake vimekatazwa kabisa.” Kisha akamwambai Rabiah: “Waambie: Damu yenu na mali zenu ni vitu viheshimikavyo kama ilivyo ardhi hii na kila aina ya uasi ndani yake ni vitu vilivyokatazwa.”

Baada ya hapo Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Rabia’ah: “Waulize ni siku gani hii?” Wakajibu wakasema: “Ni siku ya *Haj-i Akbar* (Hija kubwa).” Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Waambie: Damu yenu na mali zenu ni vyenye kuheshimika kama ilivyo siku hii.”8
“Ndio, enyi watu! Hamna budi kutambua kwamba damu iliyomwagwa katika Siku za Jahilia haina budi kusahauliwa na isilipiziwe kisasi. Hata damu ya Ibn Rabiah (ndugu wa Mtume s.a.w.w) ni lazima

isahauliwe.

Hivi karibuni mtarejea kwa Allah, na katika ulimwengu huo amali zenu njema na mbaya zitapimwa. Ninakuwambieni: Mtu yule ambaye kitu fulani kiliwekwa amana kwake, hana budi kukirejesha kwa mwenyewe.

Ndio, enyi watu! Hamna budi kutambua kwamba riba imeharimishwa kabisa kwenye dini ya Uislamu. Wale waliowekeza mitaji yao katika kuchuma riba wanaweza kuichukua mitaji yao tu. Wasiwaonee watu wala wao wasionewe. Ama kuhusu riba ambayo wadeni wa Abbas walipaswa kulipa kabla ya Uislamu, riba hiyo imekwisha kupita, naye hana haki ya kuidai.

Enyi watu! Shetani kaishapoteza matuamini ya kuabudiwa humu nchini mwenu. Hata hivyo, iwapo mtamfuata kwenye mambo madogo madogo atakuwa kwenye furaha na kupendezwa. Hivyo basi, msimfuate shetani.

Kufanya mabadiliko9 kwenye miezi mitakatifu (yaani kwenye ile miezi ambayo kupigana n.k ni haramu) huonyesha kukithiri katika kufuru, na wale makafiri wasioifahamu miezi mitakatifu wamepotoka kutokana na mabadiliko haya, na matokeo yake ni kwamba mwezi mtakatifu huwa halali kwenye mwaka mmoja na huwa ulioharimishwa vita kwenye mwaka mwingine. Wanadhania kwamba kwa kufanya hivyo, wanayabadili mambo yaliyohalalishwa na Allah na kuwa haramu na kinyume cha hivyo.

Ni muhimu kwamba mpango wa miezi iliyo halali na iliyo mitakatifu iwe ni kwa mujibu wa siku ambazo Allah aliziumba mbingu na nchi, mwezi na jua. Mbele ya Allah idadi ya miezi ni kumi na miwili na miongoni mwao Ameamua ya kwamba miezi minne iwe mitakatifu. Miezi hiyo ni Dhil Qa'adah, Dhil Hajj na Muharram, miezi ambayo inafuatana, na kisha ni mwezi wa Rajab.

Ndio, enyi watu! Wanawake wenu wanayo haki juu yenu na ninyi nanyi nnayo haki juu yao. Haki yenu ni kwamba wasimkaribishe mtu yeyote nyumbani bila ya idhini yenu, na wasiwe wakosefu wa jambo lolote lisilo la haki, ambalo kutokana na kushindwa kwao kulitoka na kushindwa kwao kutekeleza, Allah amekupeni mamlaka ya kuvitoka vitanda vyao na vile vile kuwaadhibu. Hata hivyo, kama wakirejea njia ya ukweli, hamna budi kuwatendea upole na huba na kuwapa njia ya maisha ya raha.

Ninakuusieni katika ardhi hii kwamba muwe wapole kwa wanawake wenu, kwa sababu ninyi mnawachukua kwenye dhamana itokayo kwa Allah, nao wamekuwa halali kwenu kwa mujibu wa sheria Zake. Ndio, enyi watu! Yasikilizeni maneno yangu kwa makini na yafikirieni. Ninakuachieni vitu viwili vya kumbukumbu: Kimoja kati yao ni Kitabu cha Allah na kingine ni Kauli yangu na Sunna,10 na kama mkijiambatisha navyo, katu hamtapotea.

Ndio, enyi watu! Yasikilizeni maneno yangu na yafikirini. Kila Mwislamu yu ndugu wa Mwislamu mwingine na Waislamu wote ulimwenguni ni ndugu wao kwa wao. Na chochote kile kinachotokana na mali ya Waislamu si halali kwa Mwislamu ila pale akipatapo kwa dhamiri ya uadilifu.11

Ndio, enyi watu! Wale walioko hapa wawafikishie maelezo haya wale wasiokuwepo. Baada yangu hatakuwepo Mtume, na baada yenu ninyi Waislamu hautakuwepo umma[12] mwingine.

Enyi watu! hamna budi kutambua kwamba leo ninatangaza kwamba nimezipiga marufuku ibada na itikadi zote za Zama za Ujahilia na ninakuarifuni juu ya uwongo wao. "[13]

Alipofika hapa, Mtume (s.a.w.w.) aliisimamisha hotuba yake na akafanya ishara kuelekea mbinguni kwa kidole chake cha shahada, na akasema: "Ee Allah! Nimeufikisha ujumbe Wako." Kisha baada ya kusema mara tatu: "Ee Allah! Shuhudia." Alimalizia hotuba yake.

Mtume (s.a.w.w.) alikaa Arafat siku ya mwezi tisa Dhil Hajj hadi lilipozama jua, na kabla ya jua kuzama kabisa kwenye upeo wa macho wa Magharibi na hali ya hewa kuwa na giza kidogo alimpanda ngamia wake na akaitumia sehemu ya usiku ule mahali paitwapo Muzdalifah, na muda wa baina ya alfajiri na kuchomoza kwa jua mahali paitwapo Mash'ar.

Katika siku ya kumi alikwenda Mina na kufanya ibada ya *'Rami-i' Jamrah,* akatoa kafara kwa kuwachinja wale wanyama na *taqsiir* (kupunguza nywele na kucha). Kisha alirudi Makka kwenda kuzifanya ibada nyinginezo za Hijja na hivyo akawafunza watu ibada hizo kivitendo.

Katika istilahi ya hadith na historia safari hii ya kihistoria inaitwa '*Hijjatul Widaa'* (Hija ya mwago), na wakati mwingine vilevile huitwa '*Hajul Balaagh'* (Hija ya Ufikishaji ujumbe) na *Hajul Islam* (Hija ya Uislamu). Kila moja ya majina haya lina uhusiano na ibada hii, tena ulio dhahiri kabisa.

Mwishoni tunaweza kutaja kwamba, inafahamika mno miongoni mwa wanahadithi kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliitoa hotuba hii kwenye siku ya Arafah, lakini baadhi yao wanaamini kwamba hotuba hii ilitolewa kwenye siku ya kumi ya Dhil Hajj.[14]

---

1. Siiratu Halabi, Juz. 3, uk. 289.
2. Maana ya 'Istilaam' ni kupangusa mikono kwenye Hajar'ul Aswad kabla ya kufanya Tawaaf; lengo la kitendo hiki ni kwamba, pale Nabii Ibrahim (a.s.) alipokuwa akiijenga Ka'abah, alisimama juu yake. Hivyo basi, Jiwe hili lilipata heshima isiyo na kifani. Kwenye kipindi chake cha miaka kumi ya kuishi kwake mjini Madina Mtume (s.a.w.w.) alifanya 'Umrah mara mbili, mara ya kwanza kwenye mwaka wa saba na mara ya pili kwenye mwaka wa nane wa hijiriya, ilikuwa ni baada ya kutekwa kwa mji wa Makka. Umrah ya mara hii ilikuwa ni ya tatu ambayo aliifanya pamoja na ibada za Hijja. (Tabaqaatul-Kubra, juz. 2, uk. 174).
3. Safa na Marwah ni majina ya vilima viwili vilivyoko karibu na Masjidul Haraam. Na Sai maana yake ni kutembea baina ya hivyo vilima viwili. Sai huanzia kwenye kilima cha Safa na kumalizikia kwenye kilima cha Marwah.
4. Ni kidokezo cha kujamiiana na kuoga kunakowajibishwa nako, kwa kuwa moja ya mambo yaliyoharimishwa wakati mtu awapo kwenye hali ya Ihraam, ni tendo la ngono na mwanamke na uharamu wake unaishia kwa Taqsiir.
5. Bihaarul-Anwaar, Juz. 21, uk. 319.
6. Bihaarul-Anwaar, Juz. 21, uk. 185.
7. Khisaal cha Shaukh Saduq, Juz. 2, uk. 84.
8. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 605.
9. Wadhamini wa Ka'abah walikuwa wakiibadilisha miezi mitakatifu baada ya kutwaa fedha kutoka kwa watu waliokuwa na

shauku ya kupigana vita kwenye miezi hiyo.

10. Kwenye hotuba hii ya kihistoria Mtume (s.a.w.w.) aliwausia watu kuhusu Qur'ani Tukufu na Sunnah; na kwenye ile hotuba aliyoitoa pale Ghadiir na wakati wa kufariki dunia kwake aliwausia Kitabu cha Allah na Dhuria wake. Hakuna upinzani wowote ule baina ya haya maelezo mawili yaliyotolewa kwenye matukio mawili tofauti, kwa sababu, hakuna yeyote awezaye kumkanusha Mtume (s.a.w.w.) kule kuifanya kwake Sunna kuwa sawa na Qur'ani na kuvitaja vyote viwili (Sunna na Qur'ani) kuwa kumbukumbu kwenye tukio moja, na kuusia dhuria na warithi wake kwenye tukio jingine na kusisitiza juu ya kuwafuata, jambo ambalo kwa kweli ndio huko kumfuata Mtume (s.a.w.w.) na Sunna yake. Baadhi ya wanachuoni wa Ahlil Suna kwenye tafsiri zao wamedhania kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliyasema maneno haya kwenye tukio moja tu, na wamewataja dhuria wake kwenye tanbihi (maelezo ya chini ya kurasa) kama kauli mbadala, ambapo sisi hatuhitaji masahihisho yoyote ya aina hiyo. Kwa sababu kimsingi, hakuna kutoafikiana kokote baina ya haya maelezo mawili.

11. Siiratu Ibn Hisham, juz. 2, uk. 605.

12. Khisaal' cha Shaykh Saduq, uk. 84.

13. Bihaaru–Anwaar, Juz. 21, uk. 405.

14. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz, 2, uk. 184–186.

Sura Ya 60: Uislamu Wakamilishwa Kwa Uteuzi Wa Mrithi

Kutokana na maoni ya wanachuoni wa Kishia, Ukhalifa ni kazi ya Allah apewayo mtu aliye bora zaidi, afaaye zaidi na aliye na hekima zaidi miongoni mwa watu wa umma (taifa) wote. Mpaka ulio wazi zaidi baina ya Mtume na Imamu (Mrithi wa Mtume) ni kwamba Mtume huweka msingi wa dini, anapata wahyi na anacho Kitabu.

Hata hivyo kuhusu Imamu, ingawa hana chochote kati ya vyeo hivi, vivyo ukiachilia mbali kule kuwa na cheo cha mtawala, yeye yu mtu yule azifafanuaye na kuifikisha sehemu ya dini ya Allah ambayo haingeweza kufafanuliwa hadharani na Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kukosa fursa au kutokana na hali ya mambo kuwa isiyofaa, na hivyo basi alimwachia mrithi wake awaambie watu.

Hivyo basi, kutokana na maoni ya Mashia, Khalifa si mtawala wa wakati ule tu, kiongozi wa Uislamu, mwenye mamlaka ya kiutawala, mlinzi wa haki na mwenye kuzihami ngome na mipaka ya nchi, bali vile vile yu mwenye kuyafafanua masuala yenye utata ya dini na kuikamilisha ile sehemu ya amri na sheria ambayo kutokana na sababu fulani fulani haikuweza kuelezwa na yule mwanzilishi wa dini hii.

Hata hivyo, kufuatana na maoni ya Ahlul Sunna, Ukhalifa ni cheo cha kawida na cha kidunia na lengo la kuasisiwa kwake ni kwa ajili ya kuyahami mambo ya kidunia tu na maslahi ya kilimwengu ya Waislamu. Kufuatana na imani yao, Khalifa huchaguliwa kwa kurejea kwenye maoni ya watu kwa ajili ya kuyatawala mambo ya kisiasa, kisheria na kiuchumi.

Ama kuhusu ufafanuzi wa mambo ya kidini ikiwa ni pamoja na ufafanuzi wa sheria uliosimamishwa wakati wa Mtume (s.a.w.w.) lakini haukuenezwa kutokana na sababu mbalimbali, hiyo ni kazi ya wanachuoni wa Uislamu na ni juu yao kuyatatua magumu hayo na masuala yenye utata kwa njia ya Ijtihad.

Kutokana na tofauti hii ya maoni, ya Waislamu kuhusu ukweli wa ukhalifa mabawa mawili tofauti yalijitokeza miongoni mwao na kuwafanya makundi mawili. Tofauti hii inaendelea hadi leo hii.

Kwa mujibu wa maoni ya kwanza, Imamu anashirikiana na Mtume (s.a.w.w.) kwenye baadhi ya sifa, na zile sifa ambazo kuzitimiza kunafikiriwa kuwa ni muhimu kwa Mtume (s.a.w.w.) vile vile huwa muhimu kwa Imamu. Yafuatayo ndiyo yale masharti yapasikayo kutimizwa na Mtume na hata Imamu naye:

Ni lazima Mtume awe mtakatifu. Yaani ni lazima asitende dhambi yoyote ile kwenye kipindi chote cha uhai wake na asitende kosa lolote wakati wa kuzieleza amri na habari za dini au anapoyajibu maswali ya watu. Imamu naye hana budi kuwa vivyo hivyo, na hoja iliyoko kuhusiana na wote wawili ni sawa.

Mtume hana budi kuwa mtu mwenye busara zaidi kuhusiana na mambo ya sheria za kidini na lisiwepo jambo lihusianalo na dini lijifichalo kwake. Na kwa vile Imamu yu mtu aitimizaye au aifafanuaye ile sehemu ya sheria za kidini isiyofafanuliwa kwenye wakati wa Mtume wa Allah, yeye (yaani Imamu) naye hana budi kuwa mwenye kukubalika zaidi kuhusiana na maamrisho, kisheria na kanuni za dini.

Utume ni cheo akipatacho mtu kwa njia ya kuteuliwa na Allah na wala si kwa njia ya uchaguzi wa watu. Mtume hutangazwa na Allah na anateuliwa na kuishika kazi ya utume na Yeye Allah, kwa sababu ni Yeye tu awezaye kuainisha baina ya mtu aliye maasum na asiye maasum, na ni Yeye tu awezaye kuelewa kwamba ni nani aliyeifikia daraja hiyo.

Hata hivyo, kutokana na maoni ya aina ya pili, (yaani yale ya Masunni), si lazima kwamba lolote katika masharti hayo yaliyopo katika Utume liwepo kwa Imamu. Si muhimu kwamba awe mtakatifu, mnyoofu, mwenye elimu au mjuzi wa sheria za dini au ateuliwe au kuwa na uhusiano wowote na ulimwengu wa ghaibu.

Inatosha tu kwamba auhami utukufu na maslahi ya kidunia ya Uislamu kwa kuzitumia busara na hekima zake pamoja na kupata ushauri wa Waislamu na athibitishe upatikanaji wa usalama wa eneo lile kwa kutekeleza sheria ya adhabu na ajitahidi katika kuitanua nchi ya Uislamu kwa mwito wa Jihad.

Utume Na Uimamu Vilihusiana

Ukiziachilia mbali zile hoja za kimantiki na kifalsafa ambazo hatimaye huudhihirisha usahihi wa ule mtazamo wa awali, hadithi na masimulizi tuliyoyapokea kutoka kwa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) pia yanathibitisha maoni ya wanachuoni wa Kishia. Katika kipindi cha Utume wake, Mtume (s.a.w.w.) mara kwa mara alimuainisha mrithi wake na kulitoa suala la Uimamu kutoka kwenye eneo la uchaguzi au utegemezi wa kura za umma.

Sio tu kwamba alimuainisha mrithi wake kwenye Siku za mwishoni za uhai wake, bali hata pale mwanzoni kabisa mwa utume wake, wakati ambapo sio zaidi ya watu wawili ambao wamesilimu, alimtangaza mrithi wake.

Siku moja aliamrishwa na Allah kuwaonya ndugu zake wa karibu zaidi kuhusu adhabu ya Allah na kuwaita kwenye mwito wake hadi kuwafikia watu wote. Kwenye mkutano uliohudhuriwa na wazee arobaini na watano wa familia ya Bani Hashim, alisema: "Mtu wa kwanza atakayenisaidia atakuwa ndugu yangu na mrithi wangu." Sayyidna Ali (as) aliposimama na kukiri utume wake, Mtume (s.a.w.w.) aliwageukia wale waliokuwapo pale na kusema: "Kijana huyu yu ndugu yangu na mrithi wangu."1Hadith hii ni maarufu miongoni mwa wafasiri wa Qur'ani na wanahadithi kwa jina la *'Hadith Yaumud-Dar'* na *'Hadith Bid'ul Da'wah.'*

Si katika kuanza kwa utume wake tu, bali katika matukio mbalimbali mengine pia Mtume (s.a.w.w.) alitangaza utawala na urithi wa Sayyidna Ali (as). Hata hivyo, hakuna hata moja ya matangazo haya lililopata kuwa sawa na 'Hadith ya Ghadiir' katika ukuu wake, udhahiri wake na ueneaji wake.

Kaida za Hijja zilimalizika na Waislamu walijifunza moja kwa moja kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) matendo ya kidini yaliyohusu Hijja. Mtume (s.a.w.w.) aliamua kuondoka mjini Makka. Ilitolewa amri ya kuondoka, ule msafara ulipofika kwenye ukanda wa Raabigh2 ulioko umbali wa maili tatu (kilometa tano) kutoka Juhfah,3 Malaika Mkuu Jibriil alishuka mahali paitwapo ***Ghadiir-Khum*** na kumfikishia Mtume (s.a.w.w.) Aya ifuatayo: **"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Allah Atakulinda na watu. Hakika Allah Hawaongoi watu makafiri." (*Surat al-Maidah*, 5:67).**

Mahadhi ya aya hii yaonyesha kwamba Allah Alimpa Mtume (s.a.w.w.) kazi iliyokuwa muhimu mno. Na ni kazi ipi iwezayo kuwa muhimu mno kuliko kwamba amteuwe Sayyidna Ali (a.s.) kuwa Khalifa na mrithi wake mbele ya macho ya mamia ya maelfu ya watu.

Hivyo watu wote waliamrishwa kutua. Wale watu waliotangulia walikoma kuendelea mbele na wale walioachwa nyuma walijiunga na wale waliotangulia pale. Huo ulikuwa ni wakati wa adhuhuri na hali ya hewa ilikuwa ya joto sana. Watu walivifunika vichwa vyao kwa sehemu za majoho yao na kuweka ile sehemu nyingine chini ya miguu yao. Kilitengenezwa kivuli kwa ajili ya Mtume (s.a.w.w.) kwa kutumia joho lililotandazwa kwenye mti. Alisali sala ya adhuhuri kwa jamaa. Baada ya hapo, watu walipokuwa wamemzunguka, alisimama kwenye mimbari iliyotengenezwa kwa matandiko ya ngamia na akatoa hotuba ifuatayo kwa sauti kuu:

Hotuba Ya Mtume (S.A.W.W) Pale Ghadiir Khum

"Utukufu wote wamstahiki Allah. Tunauomba msaada wake na tunamwamini na kumtegemea. Tunakimbilia Kwake kutokana na matendo maovu na machafu. Yeye ndiye Mola ambaye hakuna kiongozi ghairi Yake. Hatakuwepo mtu wa kupotosha ya kwamba hakuna mungu ila Allah na

Muhammad ni mja wake na Mtume Wake. Ndio, enyi watu! Hivi kari– buni ninaweza kuukubali mwito wa Allah, na ninaweza kutoka miongoni mwenu. Mimi nina jukumu na ninyi pia mnalo jukumu. Mna maoni gani kuhusiana nami?"

Katika hatua hii wale wote waliokuwepo pale walisema kwa sauti kuu: "Tunashuhudia ya kwamba umeitekeleza kazi yako na umefanya juhudi kuhusiana na jambo hili. Allah akujazi kwa hili." Mtume (s.a.w.w.) akase– ma: "Je, mnashuhudia ya kwamba Mola wa Ulimwengu Yu Mmoja na Muhammad yu mja na Mjumbe Wake na kwamba hakuna shaka juu ya ulimwengu wa Akhera?"

Wote wakajibu wakasema: "Ni sahihi na tunalishuhudia hilo."
Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Enyi wafuasi wangu! Ninakuachieni rasilimali mbili (vitu viwili) zenye thamani kama urithi kwenu na itaangaliwa ni jinsi gani mlivyojihusisha na hizi rasilimali zangu mbili"

Kufikia hapa, mtu mmoja alisimama na kusema kwa sauti kuu: "Una maana gani unaposema vitu viwili vilivyo bora sana?" Akilijibu swali hili, Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Kimoja kati yao ni Kitabu cha Allah, ambacho upande wake mmoja unahusiana na Allah na upande mwingine umo mikononi mwenu. Na kitu kingine ni dhuria wangu na Ahlu Baiti wangu.

Allah ameniarifu ya kwamba vitu hivi viwili vya kumbukumbu havitatengana. Ndio, enyi watu! Msitake kuitangulia Qur'ani na dhuria wangu, na msizembee katika tabia zenu kuhusiana navyo, ili msije mkaangamia."

Alipofika hapo aliushika mkono wa Sayyidna Ali (a.s.) na kuuinua hadi weupe wa makwapa yao wote wawili ukaonekana kwa watu. Alimtambulisha Sayyidna Ali (a.s.) kwa watu wote na kisha akasema: "Ni nani aliye na haki zaidi juu ya waumini kuliko wao wenyewe?" Wote wakajibu wakasema: "Allah na Mtume Wake wanajua zaidi." Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Allah Yu Mwenye kutawalia mambo yangu na mimi ni mwenye kutawalia mambo ya waumini, nami nina haki zaidi juu yao kuliko wao wenyewe.

Ndio, Enyi watu! Yeyote yule ambaye mimi ni mwenye kutawalia mambo yake, huyu Ali naye yu mwenye kutawalia mambo yake.4 Ee Allah! Wapende wale wampendao Ali na uwe adui kwa wale walio maadui wa Ali. Ee Allah! Wasaidie marafiki wa Ali; wafedheheshe maadui wake na umfanye kuwa kitovu cha ukweli."

Wakati huo huo Malaika Mkuu Jibriil alishuka na kuileta aya hii: "**…Leo mimekukamilishieni Dini yenu, na kukutimiziezi neema Zangu, na Nimekuridhieni Uislamu uwe Dini yenu; …" (Surat al–Ma'idah, 5:3).**

Hadi hapo Mtume (s.a.w.w.) aliitamka '*Takbir*' kwa sauti kuu na kisha akaongeza kusema: "Ninamshukuru Allah kwa kuikamilisha Dini Yake na kuzitimiza fadhila zake na kuuridhia utawala na urithi wa Ali baada yangu." Kisha Mtume (s.a.w.w.) alishuka pale mimbarini na akamwambia Sayyidna Ali (a.s.): "Kaa hemani ili kwamba machifu na watu wakuu wa Uislamu waweze kukupa mkono wa

hongera.”

Wale masheikh wawili, Abu Bakr na Umar walimpongeza Sayyidna Ali mbele ya wengineo wote nao walimwita mtawalia wa mambo yao.

Hassan bin Thabit mshairi maarufu, baada ya kupata idhini ya Mtume (s.a.w.w.) alizisoma beti zifuatazo: “Alimwambia Ali: Simama kwa kuwa nimekuchagua unirithi kuwaongoza watu baada yangu. Yeyote yule ambaye mimi ni mtawalia wa mambo yake, Ali yu mtawalia wa mambo yake naye. Mpendeni kwa ukweli na mfuateni.”

Vyanzo Sahihi Vya Hadith Ghadiir

Miongioni mwa Hadith na masimulizi yote ya Kiislamu hakuna Hadith yoyote nyingine iliyoenezwa na kunukuliwa kama ilivyo Hadith Ghadir. Kutoka miongoni mwa Ulama wa Ahlul Sunna pekee, ulamaa 353 wameinukuu kwenye vitabu vyao na idadi ya wasimuliaji wao wategemewao inafikia masahaba 110. Wanachuoni 26 wa Uislamu wameandika vitabu vinavyotegemewa kuhusu wasimuliaji na njia (*asnad*) za Hadith hii.
Mwanahistoria maarufu wa Uislamu Abu Ja’afar Tabari amekusanya orodha ya watu wenye maarifa juu ya Hadith hii na njia zake kwenye vitabu viwili vikubwa.

Katika maadiko yote ya historia hadithi hii imekuwa simulizi kubwa ya maarifa kuhusu Imamu Ali (a.s.) kupewa umuhimu wa kwanza juu ya masahaba wote wengine wa Mtume (s.a.w.w.). Na Imamu Ali Amirul- Mu’minin (as), yeye mwenyewe alithibitisha juu ya msingi huu kwenye kamati ya ushauri (*shuura*) iliyofanyika baada ya kifo cha Khalifa wa pili, na halikadhalika katika kipindi cha Ukhalifa wa Uthuman na wakati wa ukhalifa wake yeye mwenyewe.

Ukimwachilia mbali Amirul-Mu’minin (a.s.) watu wakuu wengine wengi daima wamekuwa wakiitegemea Hadithi hii katika kuwajibu wapinzani na wenye kuikanusha haki ya Sayyidna Ali (a.s.).

Tukio la Ghadir[5] lina umuhimu mkuu mno kiasi kwamba, kama ilivyonukuliwa na wafasiri wengi wa Qur’ani Tukufu na wanahadithi, aya za Qur’ani Tukufu zimefunuliwa kuhusina na tukio la siku ile.

---

1. Tarikhut-Tabari, Juz. 2, uk. 216 na Tarikh Kamil, Juz. 2, uk. 410.
2. Raabigh ni mahali palipo baina ya Makka na Madina.
3. Ni moja ya Miqaat (Yaani sehemu ya kuvulia Ihraam). Kutoka hapa njia za watu wa Madina, Misri, na Iraq ziligawanyika.
4. Ili kuthibitisha kwamba hakuna kueleweka vibaya kutokeako baada ya hapo, Mtume (s.a.w.w.) aliirudia sentensi hii mara tatu.
5. Kwa maelezo zaidi soma kitabu ‘al-Ghadiir’ cha Allamah Amini, Juz. 1.

Sura Ya 61: Walaghai Na Kukamatwa Kwa Urumi

Baada ya taratibu zihusianazo na uteuzi wa mrithi kumalizika pale Ghadiir Khum, watu wote waliokuja kutoka Shamu na Misri kuja kushiriki kwenye ibada ya Hijja waliachana na Mtume (s.a.w.w.) pale Juhfah na kuelekea makwao.

Na watu waliokuja kutoka Hadhramaut na Yemen, nao walijitenga na ule msafara wa Hijja mahali hapa au mahali walipopafikia mapema kabla ya hapa na wakaelekea makwao. Hata hivyo, wale watu elfu kumi waliokuja na Mtume (s.a.w.w.) kutoka Madina walifuatana naye na kurejea Madina na wakafika huko kabla ya kumalizika kwa mwaka wa kumi wa hijiriya.

Mtume (s.a.w.w.) na Waislamu walikuwa na furaha kwamba Uislamu umeenea kila mahali Bara Arabuni, utawala wa washirikina na ibada ya masanamu imekoma nchini kote Hijaz, na vizuizi vyote vilivyokuwemo kwenye njia ya uhubiri wa Uislamu vimeondolewa.

Mwezi wa Muharramu wa mwaka wa kumi na moja hijiriya ulikuwa karibu uandame mjini Madina wakati watu wawili walipowasili kutoka Yamamah kumletea Mtume (s.a.w.w.) barua kutoka kwa Musaylimah ambaye hapo baadae alifahamika kwa jina la Musaylimah Kadh-dhab (yaani Musaylimah muongo).

Mmoja wa makatibu wa Mtume (s.a.w.w.) aliifungua ile barua na kumsomea Mtume (s.a.w.w.). Ile barua ilionyesha kwamba mtu aitwaye Musaylimah alidai kwamba yu Mtume huko Yamamah. Alidai kuwa mshirika wa Mtume (s.a.w.w.) katika utume na kwa njia ya barua ile alitaka kumjulisha Mtume (s.a.w.w.) jambo lile.

Maneno ya ile barua ya Musaylimah yamehifadhiwa kwenye vitabu vya maisha ya Mtume (s.a.w.w.) na vya historia ya Uislamu. Jinsi ya utumiaji wa maneno kwenye barua ile huonyesha kwamba mwandishi alitaka kuiga jinsi ilivyo Qur'ani Tukufu.

Hata hivyo, uigaji huu umeifanya barua yake ile kuwa dhaifu, yenye kufedhehesha na isiyo na faida hata kidogo kiasi kwamba sentensi zake nyingine za kawaida ni bora zaidi kuliko hiyo.

Kwenye barua yake hiyo alimwandikia Mtume (s.a.w.w.) hivi: "Nimefanywa kuwa mshirika wako katika utume. Nusu ya nchi ni yetu na ile nusu nyingine ni ya Waquraishi. Hata hivyo, Waquraishi hawatendi haki."

Mtume (s.a.w.w.) alipoyatambua yale yaliyomo kwenye barua ile aliwageukia wale walioileta na kuwaambia: "Kama msingelikuwa wawakilisha na wajumbe ningeliamrisha muuwawe. Mkiwa mwishasilimu tayari, na kuushuhudia utume wangu, ni kwa nini mnamfuata mtu huyu mpumbavu na kuiacha dini takatifu ya Uislamu?" Mtume (s.a.w.w.) alimwita katibu wake na kumsomea kwa njia ya imla jibu la barua ile lililo fupi lakini lililo laini lakini zito. Yafuatayo hapa chini ndio maneno ya Mtume

(s.a.w.w.): “Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Rahimu.

Ni barua itokayo kwa Muhammad Mjumbe wa Allah, kwenda kwa Musaylimah laghai; Amani iwe juu ya wafuasi wa mwongozo. Nchi ni mali ya Allah, Naye huwapa nchi hiyo wale waja Wake walio wachamungu, Awapendao. Na watu wachamungu huupata mwishilizio mwema.”1

Wasifu Mfupi Wa Maisha Ya Musaylimah

Musaylimah alikuwa mmoja wa wale watu waliokuja Madina kwenye mwaka wa kumi wa hijiriya na kusilimu. Hata hivyo, baada ya kurejea kwenye sehemu aliyozaliwa, yeye naye alidai ya kwamba yu mtume na baadhi ya watu wajinga na vilevile baadhi ya watu washupavu wa dini walimwitikia mwito wake. Umaarufu wake huko Yamamah haukuwa udhihirisho wa sifa zake halisi. Baadhi ya watu walimkusanyikia wakijua ya kwamba yu laghai lakini mantiki yao ilikuwa hivi.
“Laghai wa Yamamah ni bora kuliko mtu mkweli wa Hijaz.” Kauli hii ilitamkwa na mmoja wa marafiki wa Musaylimah alipomwuliza: “Je, anakushukia malaika?” Alijibu: “Ndio, Jina lake ni Rahmaan.” Yule mtu aliuliza tena: “Je, malaika huyo yu katika nuru au katika giza?” Musaylimah alijibu akisema: “Yu katika giza”. Yule mtu akasema: “Ninashuhudia ya kwamba wewe u mlaghai. Hata hivyo, laghai wa kabila la Rabi’ah la Yamamah ni bora kuliko mtu mkweli wa kabila la Mazar la Hijaz.” (kwa kusema mtu mkweli wa kabila la Mazar alikuwa na maana ya Mtume wa Uislamu s.a.w.w).

Haiwezekani tena kusemwa kwamba mtu huyu alidai kuwa yu mtume na akajikusanyia watu. Hata hivyo, haikuweza kuthibitishwa kwamba alipanga kuipinga Qur’ani Tukufu. Na sentensi na aya zilizonukuliwa kwenye vitabu vya historia kama mifano yake ya upinzani dhidi ya Qur’ani Tukufu haziwezi kuwa ni mantiki na msemo wa mtu aliye fasaha kama Musaylimah, kwa sababu maneno yake ya kawaida na kauli zake zinabeba uthabiti mkubwa na kujiamini. Kwa mtazamo huu tunaweza kusema kwamba kila kilichohusishwa naye ni kama kauli zilizohusishwa na mtu wa zama zake aliyeitwa Aswad bin Ka’ab ‘Unsi aliyedai kuwa mtume nchini Yemen sambamba na Musaylimah,2na si yamkini kwamba yote hayo yawe ni madoido tu, katika hali zote, yaliyoishia kwenye sababu maalum.

Sababu ya kuyashikilia maoni haya ni kwamba, Qur’ani Tukufu ina ukuu usio kifani na ufasaha kiasi kwamba hakuna awezaye kuthubutu kufikiria kupingana nayo, na kila mwarabu alitambua wazi kwamba kibinadamu haikuwezakana hata kidogo kuiiga.

Baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) kampeni dhidi ya murtadi ilikuwa kitendo cha kwanza cha Ukhalifa wa Kiislamu. Hivyo basi, ukanda wa ushupavu wa Musaylimah ulizingirwa na majeshi ya Uislamu.

Mzingiro ule ulipokuwa imara na hatimaye kushindwa kwa laghai huyu kulipo dhihirika, baadhi ya marafiki zake wajinga walimwambia: “Je, imetokea nini kwa ule msaada wa ghaibu uliotuahidi?” Musaylimah alijibu akisema: “Hakuna taarifa yoyote juu ya sheria na msaada wa ghaib.

Hiyo niliyokupeni ilikuwa ni ahadi ya uwongo. Hata hivyo, ni wajibu juu yenu kuihami heshima na ukuu wenu.”

Hata hivyo, ulinzi wa heshima na ukuu ulikuwa na msaada mdogo mno! Musaylimah na kikundi cha marafiki zake waliuwawa ndani ya eneo la bustani na ule utume wa uwongo ulifikia mwisho ulioustahili.

Hiyo sentensi iliyotafsiriwa hapo juu yaonyesha kwamba Musaylimah alikuwa mzungumzaji fasaha na vile vile yaonyesha kwamba kamwe yeye hakuwa mzungumzaji wa zile kauli dufu ambazo historia imezihusisha naye, kuwa mfano wa upinzani wake dhidi ya Qur’ani Tukufu.

Kukamatwa Kwa Urumi

Ingawa kutokea kwa walaghai hawa wa utume kwenye sehemu mbalimbali za Uarabuni kulileta hatari kwa umoja wa Kiislamu, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na wasiwasi zaidi juu ya Warumi waliokuwa wakiishikilia Shamu na Palestina zikiwa ni sehemu ya makoloni yao, kwa sababu alijua ya kwamba Magavana wenye uwezo na ustadi wa Yamamah na Yemen watakuwa na uwezo wa kuwashughulikia wale walaghai wa utume. Hivyo basi, Aswad Unsi, yule laghai wa pili kwenye kipindi cha uhai wa Mtume (s.a.w.w.) aliuawa, ikiwa ni matokeo ya hatua alizozichukua Gavana wa Yemen, siku moja tu kabla ya Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na uhakika kwamba watawala wenye nguvu wa Urumi, waliokuwa wakiuangalia vema upanukaji wa daima wa serikali ya Kiislamu wataingiwa na wasiwasi kwa vile Ukristo ulikuwa ukipoteza mvuto wake Uarabuni na Uislamu umewawajibisha baadhi ya Wakristo kulipa kodi kwenye serikali ya Kislamu.

Alikuwa akizingatia kwa makini kila hatari kutoka upande wa Urumi kwa muda mrefu. Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba kwenye mwaka wa nane hijiriya alipeleka jeshi kwenye nchi ya Kirumi chini ya uamiri jeshi wa Ja’far bin Abi Talib, Zayd bin Harith na Abdillah Rawaha, na kwenye mapambano haya hawa makamanda wote watatu waliuawa na jeshi la Uislamu lilirejea Madina, ikiwa ni matokeo ya utawala wa Khalid, bila ya kupata ushindi.

Taarifa za Warumi kuishambulia Hijaz zilipoenea mjini Madina kwenye mwaka wa 9 hijiriya Mtume (s.a.w.w.) alikwenda Tabuk, yeye mwenyewe akiliongoza jeshi madhubuti lenye askari 30,000 na akarejea Madina bila mapigano na bila ya kupambana na adui.

Akiyazingatia yote hayo Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akitambua vizuri hatari iliyokuwepo na kwa sababu hii, baada ya kurejea Madina alitayarisha jeshi walimokuwemo Muhajiriin na Ansar; walimokuwemo watu wakuu kama vile Abu Bakr, Umar, Abi Ubaydah, Sa’ad Waqqas n.k. Kusema kweli alitoa amri kwamba wale Muhajirin wote ambao walihajiri Madina mapema kuliko wenzao lazima washiriki katika vita hivi.3

Ili kuweza kuamsha hisia za kidini za mashujaa wa Kiislamu, Mtume (s.a.w.w.) alifunga bendera na kumpa Usamah kwa mkono wake mwenyewe4 na kumpa maelezo yafuatayo: “Pigana kwa jina la Allah

na katika njia Yake. Pigana dhidi ya maadui wa Allah.

Washambulie watu wa Unba5 mapema asubuhi na tembea umbali huu upesi sana kiasi kwamba wewe na askari wako mfike mahali pale kabla ya taarifa za kwenda kwenu huko hazijafika pale."

Usamah alimpa Buraydah bendera ile na akaiweka Jurf 6 kuwa sehemu yake ya kupigia kambi ili wale askari wa Kiislamu waweze kufika pale kwa makundi na kisha wote waweze kuondoka katika muda uliowekwa.

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiyafikiria mambo mawili pale alipomchagua kijana kuwa kiongozi wa jeshi lake na kuwaweka wazee kutoka miongoni mwa Muhajiriin na Ansar chini ya uongozi wake. Kwanza kabisa alitaka kumpa fidia Usamah kwa msiba uliompata kutokana na kumpoteza baba yake katika Vita vya Mutaah na kuliinua daraja lake.

Pili, alitaka kuihuisha sheria ya ugawaji wa kazi na vyeo kwa msingi wa sifa na uwezo wa mtu, na alitaka kudhihirisha kwamba ofisi za Umma na hali ya mazingira havihitaji chochote ila uwezo na ustadi, na mambo haya hayana lolote lihusianalo na umri, ili kwamba vijana wenye uwezo waweze kujitayarisha kuyashika majukumu ya umma yaliyo muhimu, na hawana budi kutambua kwamba katika Uislamu cheo na ofisi vinauhusiano wa moja kwa moja na uwezo na ustadi na wala si miaka na umri.

Uislamu ni nidhamu halisi kwa mujibu wa mafundisho ya Allah; na Mwislamu halisi ni yule ambaye mbele ya maamrisho ya Allah yu kama alivyo askari katika uwanja wa mapambano, na anayakubali maamrisho hayo kwa uaminifu, yawe matokeo yake ni faida kwa mtu yule au ni hasara, na iwe ni kwa mujibu wa mapenzi yake au dhidi yake. Sayyidna Ali Amirul–Mu'minin (as) anaufafanua ukweli wa Uislamu kwa sentensi fupi mno na yenye maana. Anasema: "Uislamu si chochote kingine ila kujitoa barabara ili kuzitekeleza amri zake."7

Baadhi ya watu hufanya ubaguzi kuhusiana na maamrisho na kanuni za Uislamu, na kila wazionapo kuwa zinapingana na matakwa yao ya binafsi, mara moja hukataa na hutafuta sababu za kujitoa kwenye uwajibikaji wa maamrisho hayo. Watu hawa wanaikosa nidhamu ya Kiislamu, nao hawana shauku halisi ya kujitoa barabara kwa ajili ya sheria hizo.

Ukamanda wa kijana Usamah bin Zayd, ambaye wakati ule umri wake haukuzidi miaka ishirini,8 ni uthibitisho wa dhahiri wa yale tuliyoyasema hapo juu, kwa sababu cheo chake kiliwaudhi baadhi ya masahaba waliokuwa na umri mkubwa kuliko wake.

Walianza kumdhihaki na kukana na kutamka maneno yaliyoonyesha utovu wa nidhamu ya kijeshi na ukosefu wa moyo wa utii wa amri za Amiri jeshi Mkuu wa Uislamu (yaani, Mtume). Sababu yao kubwa waliyotoa ilikuwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) amemteua kijana kuwa kamanda wa masahaba wazee.9

Hata hivyo, wao hawakuyatambua yale maslahi makubwa yaliyokuwemo kwenye jambo lile kama tulivyoyaeleza kwenye mistari iliyotangulia, walilikasimia jambo hili kutegemeana na hekima zao chache

na maslahi yao ya kibinafsi.

Licha ya ukweli kwamba walijihisi kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akijitahidi kuliandaa jeshi hili, watu wenye njama za siri walikuwa wakichelewesha kuondoka kwake kutoka pale penye kambi yake pale Jurf, na lilikuwa likipanga mipango miovu.
Siku iliyofuatia baada ya Mtume (s.a.w.w.) kuifunga ile bendera ya vita kwa ajili ya Usamah, alipatwa na homa kali sana na kuumwa na kichwa. Ugonjwa huu uliendelea kwa siku kadhaa na hatimaye kutokea kifo chake cha kimasaibu.

Wakati wa kipindi cha kuumwa kwake, Mtume (s.a.w.w.) alitambua kwamba kuondoka kwa jeshi lile kutoka kwenye ile kambi yake kulikuwa kukizuiwa, na baadhi ya watu walikuwa wakiudhihaki ukamanda wa Usamah.

Jambo hili lilimuudhi mno Mtume (s.a.w.w.), na huku akiwa kaweka taulo begani mwake na kitambaa kilichofungwa kichwani mwake, alikwenda msikitini ili akazungumze na Waislamu kwa karibu zaidi na kuwaonya juu ya kuzivunja amri za Allah.

Alikuwa ana joto kali sana mwilini, alipanda mimbari na baada ya kumtukuza Allah alisema hivi: “Ndio, enyi watu! Ninasikitika sana kutokana na kuchelewa kuondoka kwa jeshi. Inaonyesha kwamba ukamanda wa Usamah umekataliwa na baadhi yenu, nanyi mmeanza kutoa udhuru. Hata hivyo, udhuru na uasi wenu si kitu kigeni, hapo awali mliulaumu ukamanda wa baba yake Usamah, Zayd. Ninaapa kwa jina la Allah kwamba yeye alistahiki kukishika cheo kile na mwanawe naye anastahiki kukishika pia. Yeye ni mpendwa kwangu mimi. Enyi watu! Kuweni wema kwake na vilevile mpendekezeni kwa wenzenu kwamba wawe wema kwake. Yeye yu mmoja wa wale walio wema wenu.”

Mtume (s.a.w.w.) aliimalizia hotuba yake hapa, akashuka kwenye mimbari na akaenda kulala akiwa yu mwenye homa kali na mwili mzito. Kwa kurudiarudia alikuwa akiwaambia wale masahaba wakubwa wakubwa waliokuja kumtazama: “Lifanyeni jeshi la Usamah liondoke.”10 Na wakati mwingine alisema: “Lipatieni silaha jeshi la Usamah” au “Lipelekeni jeshi la Usamah.”

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na shauku mno juu ya kuondoka kwa jeshi la Usamah kiasi kwamba alipokuwa yu mgonjwa wa kitandani aliwataka masahaba wake walipatie silaha jeshi la Usamah ili liweze kuondoka. Vilevile aliwalaani wale waliotaka kujitenga na jeshi lile na kubakia pale Madina.11

Maagizo haya ya Mtume yaliwafanya wazee wale kutoka miongioni mwa Muhajiriin na Ansar waliokuja kumtazama Mtume (s.a.w.w.) kumuaga na kisha kuondoka Madina kwa shingo upande na kwenda kujiunga na lile jeshi la Usamah kule kwenye kambi ya Jurf.

Katika kile kipindi cha siku mbili au tatu Usamah alipokuwa akijishughulisha kufanya matayarisho ya kuondoka, taarifa juu ya hali mbaya zaidi ya Mtume (s.a.w.w.) ilifika kule kambini kutoka Madina na kuzidhoofisha nyoyo za watu kuhusiana na kuondoka hadi ikafika siku ya Jumatatu, yule kamanda wa jeshi lile alikuja kumuaga Mtume (s.a.w.w.) na akaiona hali ya Mtume (s.a.w.w.) ikiwa na afadhali

kidogo.

Mtume (s.a.w.w.) akamtaka aendelee na safari yake upesi iwezekanavyo. Alirejea kule kambini na kutoa amri ya kuondoka kwa jeshi lile. Ilikuwa bado jeshi halijaondoka pale Jurf (penye kambi) ilipofika taarifa kutoka Madina kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mahututi.

Baadhi ya watu waliochelewesha kule kuondoka kwa jeshi kwa kipindi cha siku kumi na sita kwa kutoa udhuru wa aina mbalimbali, waliifanya ile hali mbaya ya Mtume (s.a.w.w.) kuwa sababu na wakarejea Madina na wengine wakafanya vivyo hivyo. Hivyo moja ya shauku kuu ya Mtume (s.a.w.w.) haikuweza kutimizwa kwenye kipindi cha uhai wake kutokana na utovu wa nidhamu wa baadhi ya maafisa wa jeshi lile.[12]

Udhuru Usiofaa

Haiwezekani kulielezea hasa kosa hili kwa upande wa baadhi wa masahaba wale ambao baadae walizishika hatamu za Ukhalifa wa Mtume (s.a.w.w.)! Baadhi ya wanachuoni wa Ahlus-Sunna wamejitahidi kuelezea na kutetea utovu wao wa nidhamu kwa njia mbalimbali. Ili kudurusu nyudhuru zao zisizo na msingi soma vitabu: *'Al-Muraji'at* [13] na *Al-Nass Wal-ijtihad.*[14]

Kuwaombea Msamaha Wale Waliozikwa Baqii

Baadhi ya waandishi wa wasifu wameeleza kwamba: "Siku ambayo joto la mwili wa Mtume (s.a.w.w.) liliongezeka sana, na akawa amelala kitandani, alikwenda kwenye mava ya Baqii wakati wa usiku wa manane akifuatana na mtumwa wake aliyeitwa Abi Muwayhabah[15] kwenda kuwaombea msamaha wale waliozikwa pale.

Baadhi ya wanahistoria wanaamini ya kwamba siku ambayo Mtume (s.a.w.w.) aliugua, aliushika mkono wa Sayyidna Ali (a.s.) na kwenda kwenye mava ya Baqii pamoja na kundi la watu waliokuwa wakiwafuata, na akawaambia wale waliokuwa wakifuatana naye: "Nimeamrishwa na Allah kuwaombea msamaha watu wa Baqii."

Alipoubandika mguu wake kwenye mava yale, aliwasalimu wale waliozikwa pale, na akasema hivi: "Ninakutoleeni salaam, ninyi mliozikwa chini ya ardhi. Hali mliyonayo hivi sasa na iwe ya furaha na nzuri kwenu. Misukosuko imetokea kama sehemu za usiku wa giza na imeungana pamoja." Kisha aliwaombea msamaha watu wa Baqii.

Baada ya hapo alimgeukia Sayyidna Ali na kusema: "Nimekabidhiwa funguo za hazina ya ulimwengu na maisha yaliyorefushwa ndani yake na nimepewa nichague baina ya hizo na kukutana na Allah na kuingia Peponi, lakini nimependelea kukutana na Mola wangu na kuingia Peponi. (Kama ilivyonukuliwa na wasimuliaji wa *Tabaqaat* n.k aliugeuzia uso wake kwa Abi Muwayhabah) "Malaika Mkuu Jibriil alikuwa akinileta Qur'ani mara moja kwa mwaka, lakini mwaka huu amenileta mara mbili. Hapawezi

kuwa na sababu yoyote ile kwa jambo hili ila tu kwamba muda wa kuondoka kwangu umekaribia."[16]

Watu wauonao ulimwengu huu kwa macho ya kimaada tu, nao hawalifikirii lengo la uumbaji kuwa ni chochote kile nje ya maada na midhihiriko yake, pengine wanaweza kuwa na shaka juu ya jambo hili na wanaweza kusema nafsini mwao: "Basi ni vipi mtu aweza kuwasiliana na roho na kuzungumza nazo na ni vipi mtu aweza kutambua muda wa kufa kwake?"

Hata hivyo, wale watu walioyakana mambo ya kidunia nao wanaamini kuwako kwa roho iliyo huru kutokana na mwili wa kimaada, katu hawakani kuwasiliana na roho na hulichukulia jambo hili kuwa ni lenye kuwezekana na la ukweli.[17]

Mtume ambaye ameungana na ulimwengu wa wahyi na dunia zingine zilizo huru kutokana na maada, na aliye huru kutokana na kukosea, bila shaka anaweza kutoa taarifa kuhusiana na matakwa ya Allah kuhusu kifo chake.

---

1. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 600–601.
2. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 599.
3. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 6452; 'Al–Nass wal Ijtihad', cha Sharafuddin Aamili, uk. 12.
4. Kufuatana na vitabu vya kihistoria vya Ahlil Sunna ile bendera ilifungwa mnamo mwezi 26 Safar na kwa mujibu wao, kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) kulitokea mnamo, mwezi 12 Rabi'ul Awwal; hivyo basi matukio yote atakayoyasoma msomaji yaelekea kutokea kwenye kipindi cha siku kumi na sita. Hata hivyo, kwa vile wanachuoni wa Kishia wanawafuata dhuria wa Mtume (s.a.w.w.) huichukulia tarehe ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni 28 Safar, hivyo itakuwa muhimu kwamba matukio haya yalitokea siku kadhaa kabla ya 28 Safar.
5. Ni ukanda wa nchi kwenye jimbo la Balqa nchini Shamu nao uko baina ya 'Asqalaan na Ramlah karibu na Mutaah.
6. Ni sehemu iliyoko maili tatu kutoka Madina kuelekea upande wa Shamu.
7. Nahjul Bahagha, Kalimaatul–Qisaar (Hadith namba, 125).
8. Baadhi ya waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) kama vile Halabi wameutaja umri wake kuwa ulikuwa miaka 17 na kwa mujibu wa wengine alikuwa na umri wa miaka 18. Hata hivyo wote wanakubaliana kwamba umri wake wakati ule haukuzidi miaka 20.
9. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, juz. 2, uk. 120.
10. Tabaqaatu Ibn Sa'ad Juz. 2, uk. 190.
11. Al–Milal Wan–Nahl' cha Shahristani utangulizi wa nne, uk. 29; na Sharhu Nahjul Balaghah, cha Ibn Abil Hadid Mutazili, Juz. 2, uk. 20.
12. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, juz. 2, uk. 190.
13. Al–Muraji'at, uk. 310–311.
14. An–Nass Wal–ijtihad, uk. 15–19.
15. Baadhi ya wanachuoni wanasema kwamba alifuatana na Abu Raafi' au na Burayrah, mtumishi wa Aisha (Tabaqaatu Ibn Sa'ad, juz. 2, uk. 204).
16. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2, uk. 204; Bihaarul An'waar, Juz. 21, uk. 366.
17. Hata hivyo, kama tulivyoelezea kwenye majadiliano yahusianayo na mawasil– iano na roho, si sahihi kumsikiliza kila mwenye kudai hivyo.

Sura Ya 62: Usia Ambao Haukuandikwa

Enzi za mwisho wa maisha ya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.) alipokuwa yu mgonjwa wa kitandani, ni moja ya nyakati zilizo nyeti zaidi na zenye kutatiza mno katika historia ya Uislamu. Katika siku hizo Waislamu walikuwa wakipita kwenye wakati mgumu sana. Utovu wa adabu wa dhahiri kabisa kwa upande wa baadhi ya masahaba na kukataa kwao kujiunga na jeshi la Usamah ni ushahidi wa mfululizo wa matendo ya chini chini na dhamira ya awali kabisa ya watu waliohusika ya kwamba, baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) wataichukua serikali na mambo ya kisiasa ya Uislamu na watamsukumizia nyuma yule mtu ambaye hapo awali aliteuliwa kwenye siku ile ya Ghadiir kuwa mrithi wa Mtume (s.a.w.w.).

Kwa kiasi fulani Mtume (s.a.w.w.) naye aliitambua dhamiri yao, na ili kuyabatilisha matendo yao, alisisitiza kwamba wale masahaba watu wazima wote wajiunge na jeshi la Usamah na watoke mle mjini Madina upesi kwa kadiri ilivyowezekana na waende wakapigane na Warumi. Hata hivyo, ili kuitekeleza kivitendo mipango yao, hawa walaghai wa kisiasa walijitolea nyudhuru wenyewe za kutojiunga na jeshi la Usamah kwa visingizio mbalimbali na hata kuthubutu kulizuia lile jeshi lisiondoke, kiasi kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliiaga dunia lakini lile jeshi la Uislamu halikuondoka pale Jurf (sehehu kambi ya kijeshi mjini Madina) na lilirejea Madina baada ya kukaa pale kwa kipindi cha siku kumi na sita.

Kule kuzuilika kwao kulitokana na kifo cha Mtume (s.a.w.w.). Hivyo basi, ile hamu ya Mtume (s.a.w.w.) kwamba siku ya kifo chake mji wa Madina utakuwa huru kutokana na waasi wa kisiasa ambao wangeliweza kujitumbukiza kwenye matendo yaliyo dhidi ya yule mrithi wake haikutimizwa. Hawakushindwa kuondoka Madina tu bali vilevile walijitahidi kukipinga kila kitendo ambacho kingeliweza kukithibitisha cheo cha Sayyidna Ali (a.s.) kuwa yu mrithi wa papo kwa papo wa Mtume (s.a.w.w.) na kumzuia Mtume (s.a.w.w.) kulizungumzia jambo hili kwa njia yoyote ile.

Mtume (s.a.w.w.) alipata kuyatambua yale matendo ya kushitusha na shughuli za siri ya baadhi ya mabinti zao, ambao walipata kuwa wakeze. Ingawa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na homa kali, aliingia msikitini, akasimama kandokando mwa mimbari, akawageuzia watu uso wake akasema kwa sauti kuu iliyoweza kusikika hata kwa nje ya msikiti ule. “Enyi watu! Uasi umelipuka na uasi umejitokeza kama vipande vya usiku wa giza. Hamna kisingizio dhidi yangu. Sikutangaza kitu chochote kuwa ni halali isipokuwa kile ambacho Qur’ani imekitangaza kuwa ni halali na sikutangaza kitu chochote kuwa ni haramu isipokuwa kile ambacho Qur’ani imekitangaza kuwa ni haramu.”1

Kauli hii yaionyesha ile shauku kuu ya Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na hali ya baadae na kuhusu hatima ya Uislamu baada ya kifo chake. Alikuwa na maana gani pale aliposema uasi umelipuka? Je, maana yake yaweza kuwa yoyote nyingine zaidi ya – uasi na mfarakano ulioundwa baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) na miali yake bado haijazimika, bali unaendelea bado kuwaka?

Nileteeni Kalamu Na Kidau Cha Wino Ili Niweze Kuwaandikieni Usia

Mtume (s.a.w.w.) aliyatambua matendo yaliyokuwa yakitendeka mbali na nyumba yake ili kunyakua Ukhalifa. Ili kuweza kuzuia kukengeushwa kwa ukhalifa kutoka kwenye mhimili wake halisi na kutokea kwa mifarakano na ugomvi, aliamua kuuthibitisha ukhalifa wa Sayyidna Ali Amirul– Mu'minin, na cheo cha Ahlul–Bayt (a.s.) kwa maandishi ili kwamba maandishi hayo yaweze kuwa ushahidi wa dhahiri juu ya jambo la Ukhalifa.

Siku moja wale masahaba wakuu walipokuja kumtazama Mtume (s.a.w.w.) aliinamisha kichwa chake kidogo na akafikiria kwa kitambo fulani hivi.
Kisha akawaambia: "Nileteeni karatasi na kidau cha wino ili kwamba nikuandikieni jambo fulani kwa ajili yenu, ambalo baada yake hamtapotea."2

Mambo yalipofikia hapo, khalifa wa pili alikivunja kimya kilichotawala pale na kusema: "Mtume kazidiwa nguvu na ugonjwa. Mnayo Qur'ani. Kitabu Kitukufu cha Allah kinatutosha."

Maelezo aliyoyatoa khalifa yule yakawa mada ya majadiliano. Baadhi ya watu walimpinga wakisema: "Ni lazima amri ya Mtume itiiwe. Nenda ukamletee kalamu na karatasi ili kwamba chochote kile alichonacho akilini mwake kiweze kuandikwa." Wengine waliuchukua upande wa yule khalifa na kuzuia kule kumletea Mtume (s.a.w.w.) kalamu na wino. Mtume (s.a.w.w.) aliudhishwa mno na kule kugombana kwao na kule kutoa maneno ya ufidhuli, hivyo akasema: "Amkeni na ondokeni katika nyumba hii (tokeni hapa). "

Baada ya kulisimulia tukio hili, Ibn Abbas anasema: "Msiba mkuu kwa Uislamu ulikuwa ni kule kutoafikiana, na ule ugomvi wa baadhi ya masahaba uliomzuia Mtume kuandika usia aliokusudia kuandika."3

Tukio hili la kihistoria limenukuliwa na baadhi ya wanahadithi na wanahistoria wa Kisunni na Kishia. Na kutokana na maoni ya wachanganuzi wa hadithi, wanaichukulia hadithi hii kuwa inaangukia kwenye mkumbo wa hadithi zilizo sahihi.

Nukta yenye kuhitaji mazingatio hapa ni kwamba, wanahadithi wa Kisunni wamenukuu maana ya jumla tu ya yale maneno ya Umar, lakini hawakuinukuu ile kauli yake ya kifidhuli. Ni dhahiri kwamba wameepuka kuinukuu kauli ile ya asili, sio kwa sababu kwamba kuinukuu kauli ile ya kiburi ni sawa na kumzoea Mtume (s.a.w.w.) kupita kiasi (cha nidhamu), bali vilevile wao wameyabadili maneno ya khalifa kwa lengo la kukihami cheo chake ili kwamba kizazi kijacho nyuma kisiwe na fikira mbaya juu yake watakapoona maneno yake ya matusi.

Hivyo basi, Abu Bakr Jauhari, mwandishi wa kitabu kitwacho *'Al–Saqifa'* alipofika kwenye nukta hii ndani ya kitabu chake alisema, wakati akiyanukuu maneno ya Umar: "Umar alisema maneno fulani ambayo

maana yake ni kwamba maradhi yamemzidi nguvu Mtume."4

Hata hivyo, baadhi yao wanapotaka kuyanukuu yale maneno ya yule khalifa, wanaepuka kulitaja jina lake waziwazi kwa lengo la kukihami cheo chake na wanaandika tu hivi: "Na wakasema: Mtume wa Allah kazungumza akiwa kwenye hali ya kupayuka."5

Ni ukweli ukubalikao kwamba mwenye kuyatamka maneno haya machafu na yenye kuchukiza hawezi kusamehewa, kwa sababu kama ielezwavyo dhahiri kwenye Qur'ani, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa safi kutokana na kila aina ya makosa na kila alichokisema kilikuwa ni ufunuo uliofunuliwa kwake.

Kubishana kwa masahaba mbele ya Mtume (s.a.w.w.) aliye mtakatifu kulikuwa kunakokirihisha na kuudhisha kiasi kwamba baadhi ya wakeze Mtume (s.a.w.w.) waliokuwa wamekaa nyuma ya pazia, waliuliza kwa jinsi ya kuchukizwa, ni kwa nini amri yake Mtume (s.a.w.w.) isitiiwe. Ili kuwanyamazisha, khalifa yule alijibu akisema: "Ninyi wanawake mko kama masahaba wa Nabii Yusufu: Mtume anapougua ninyi mnalia na anapopona mnamtawala."6

Ingawa baadhi ya washupavu wa kidini wamejaribu kuunda udhuru kwa ajili ya khalifa yule kuipinga haja ya Mtume7 lakini wamemlaumu katika msimamo wa mantiki, na wameyachukulia maneno yake (kitabu cha Allah kinatutosha) kuwa yasio na msingi. Wote wamekubali waziwazi kwamba Sunna za Mtume (s.a.w.w.) ndio msingi wa pili wa Uislamu na Kitabu cha Allah hakiwezi hata kidogo kuuondolea umma wa Kislamu haja ya Sunna ya Mtume (s.a.w.w.).

Hata hivyo, inashangaza kwamba Dakta Haykal, mwandishi wa kitabu kiitwacho *'Hayat–i Muhammad'* ameamua kuwa pamoja na yule khalifa kwa njia ya kidokezo na anaandika hivi: "Baada ya tukio hili Ibn Abbas aliamini kwamba kwa kutokuandikwa kwa kile Mtume (s.a.w.w.) alichotaka kiandikwe, Waislamu wamekipoteza kitu kilicho muhimu sana, lakini Umar aliyashikilia maoni yake, kwa sababu Allah anasema mwenye Qur'ani: **"Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote"**8

Hata hivyo, kama mwandishi huyu angeyachunguza maneno yaliyotangulia na yanayofuatia ya aya hii (yaani, muktadha) asingelieleza kwa namna isiyothibitika kama hiyo na asingesimama na kumuunga mkono yule khalifa dhidi ya maneno ya dhahiri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu maana ya neno Kitabu kwenye aya iliyotajwa ni uumbaji na kurasa za uhai na jamii ya viumbe mbalimbali katika ulimwengu wa uhai ni kurasa mbalimbali za kitabu cha maumbile. Na hizi kurasa zisizo na idadi hukipa umbo kile kitabu cha maumbile. Haya yafuatayo hapa ndio maneno ya aya ile:

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ ۚ مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ ۚ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ {38}

"Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anayeruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma

kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa." (***Sura al- An'am, 6:38***).

Kwa vile maneno yanayoitangulia sentensi inayojadiliwa yanazungumzia wanyama na ndege, na maneno yanayoifuatia yanazungumzia juu ya Siku ya Ufufuo, basi tunaweza kusema waziwazi kwamba kwenye aya hii maana ya neno Kitabu, ambacho ndani yake hakuna kilichoachwa ni kitabu cha maumbile.

Mbali na hili, hata kama tukikubali kwamba maana ya neno Kitabu kwenye Aya hii ya Qur'ani ni Qur'ani yenyewe, hata hivyo, kufuatana na ilivyoelezwa na Qur'ani yenyewe, ni ukweli ukubalikao kwamba yenyewe Qur'ani inaweza kueleweka tu katika mwanga wa hadithi na mwongozo wa Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Qur'ani inasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِي إِلَيْهِمْ ۚ فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ {43}

بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ ۚ وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ {44}

"Nasi hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume tuliowapa Wahyi. Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui. Kwa ishara wazi na vitabu. Nasi tumekuteremshia wewe ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, wapate kufikiri."
(***Sura al- Nahl, 16:43-44***).

Katika aya hii, haikusemwa: "Ili uweze kuwasomea wanadamu." Maneno yaliyotumika ni: "ili uwabainishie watu." Kwa hiyo, hata kama Kitabu cha Allah Kitosheleze kwa wanadamu, bado kinayo haja kubwa ya maelezo ya Mtume (s.a.w.w.).

Kama umma wa Kiislamu kwa uhakika wangeweza kuachana na hati ya maandishi kama ile, yaani yale aliyotaka kuyaandika Mtume (s.a.w.w.), ni kwa nini basi Ibn Abbas aliyatamka maneno yafuatayo, wakati machozi yakimtiririka mashavuni mwake: "Msiba ulioje wa siku ya Alhamisi; Mtume aliposema: 'Nileteeni mfupa wa bega la mnyama na kidau cha wino au karatasi na kidau cha wino ili nikuandikieni jambo fulani na baadae msije mkapotoka.' Baadhi ya watu wakasema: 'Mtume ana....."[9]

Itawezekanaje kusemwa kwamba pamoja na hisia hizi zilizoelezwa na Ibn Abbas, na ule msisitizo alioufanya Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe, Qur'ani imeuwezesha umma wa Kiislamu kuachana na usia huu? Na kwa vile Mtume (s.a.w.w.) hakufaulu kuutamka usia ule ili uandikwe, je inaweza kukisiwa kwa

njia zozote za dalili zilizowazi kile alichokusudia kukiandika kwenye usia wake huo?

Usia Ulilenga Juu Ya Nini?

Moja ya njia zilizo bora zaidi za kuzielezea aya za Qur'ani, ambazo hata hivi sasa bado zinaamrisha mazingatio na upendeleo wa utafiti wa wanachuoni na ulamaa wa wakati huu, ni kwamba ufupi na utata wa aya iliyoshushwa juu ya jambo fulani unaweza kuondolewa kwa njia ya aya nyingine juu ya jambo hilo hilo, ambayo kutegemeana na aina ya maelezo yake inakuwa yenye kueleweka vizuri zaidi kuliko ile ya awali. Kwa mujibu wa tafsiri ya Qur'ani, njia hii inaitwa kuitafsiri aya moja kwa msaada wa aya nyingine.

Njia hii si njia pekee ya kuzifasiri aya za Qur'ani Tukufu tu ambayo hutumika kwenye mafundisho ya Kiislamu, kwani halikadhalika utata wa hadithi moja unaweza kuondolewa kwa msaada wa hadithi nyingine, kwa sababu viongozi wetu wakuu wametilia mkazo na maelekezo ya mara kwa mara juu ya masuala nyeti na yenye kuonekana, ambayo maelezo yao kuhusiana na lengo lao si yenye kutambulika dhahiri na kwa kiwango kilekile. Wakati mwingine lengo lao limeelezwa waziwazi na kwa wakati mwingine limechukuliwa kiushauri tu.

Kama ilivyoelezwa hapo juu, Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa yu mgonjwa kitandani, aliwataka masahaba wake wamletee kalamu na karatasi ili aweze kutamka usia na usia huo uandikwe.

Vilevile aliwaambia ya kwamba usia huo utawathibitishia kutopotea kwao wakati wowote ule. Baadae, kutokana na tofauti baina ya wale waliokuwapo, Mtume (s.a.w.w.) alilitupilia mbali wazo lile la kuuandika ule usia.

Bila shaka mtu anaweza kuuliza: "Ni juu ya jambo gani ambalo Mtume (s.a.w.w.) alitaka kuliandikia usia?" Jibu la swali hili ni dhahiri kabisa, kwa sababu tukiuchukulia ukweli wa kimsingi uliotajwa hapo mwanzoni mwa majadiliano haya, hatuna budi kusema kwamba lengo la Mtume (s.a.w.w.) katika kuuandika usia ule, halikuwa lolote jingine ila kuuthibitisha Ukhalifa na urithi wa Sayyidna Ali Amirul–Mu'minin (as), na kuwawajibisha watu kuwafuata watu wa nyumba yake.

Tunaweza kuamua hivi kwa kuchunguza *Hadith Thaqalayn* ambayo imekubaliwa kwa pamoja na wanahadithi wa Kisunni na Kishia kwa pamoja, kwa sababu alisema hivyo kuhusiana na usia aliotaka kuuandika: "Ninaiandika hati hii ili kuthibitisha kwamba hampotei baada yangu."

Na kwenye *Hadith Thaqalayn,* vilevile alitumia maneno yenye kuanisha na akasisitiza kwamba watu lazima wafuate zile *'Thiql'* mbili (Vitu viwili vizito au vyenye thamani, yaani Qur'ani Tukufu na dhuria wake) ili kwamba wasipotee baada yake. Yafuatayo hapa ndio maneno ya *Hadith Thaqalayn:* "Ninakuachieni vitu viwili vizito (vyenye thamani) miongoni mwenu. Kwa kadiri mvifuatavyo vyote viwili hamtapotea. Vitu hivi viwili vyenye thamani ni Kitabu cha Allah (Qur'ani Tukufu) na dhuria wangu Ahlul–Bayt."

Je, haiwezi kuamuliwa kutokana na maneno ya hizi hadith mbili, na kule kufanana kuliko ndani yao, kwamba lengo la Mtume (s.a.w.w.) katika kule kutaka aletewe kalamu na karatasi lilikuwa ni kuyaandika maneno ya *Hadith Thaqalayn* katika hali iliyo waziwazi zaidi na kuuthibitisha utawala na ukhalifa wa papo kwa papo wa mrithi wake, ambao ulitangazwa kwa maneno tu mnamo mwezi kumi na nane Dhil Hajj wakati mahujaji wa Iraq, Misri na Hijaz walikuwa wakiagana pale Ghadir Khum?

Aidha, upinzani wenye nguvu wa mtu mmoja, ambaye mara tu baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) aliasisi halmashauri ya ushauriano kwenye Saqifah Bani Saidah kwa ajili ya uchaguzi wa khalifa na akamfanya rafiki yake wa tangu kale na kale kuwa mgombea uchaguzi wake kwa namna maalumu na baadae yule rafiki akamteua yeye awe khalifa kwa kubatilisha kanuni zote, labda kwa ajili ya kumlipa fadhila kwa msaada wake, huonyesha kwamba kulikuwa na dalili katika mkusanyiko ule na katika khutba ya Mtume kwamba, alitaka kuandika jambo fulani kuhusu ukhalifa na utawala wa Waislamu. Hivyo yeye alipinga vikali kule kuleta kalamu na karatasi, kwa kuwa kama si hivyo haikuwapo sababu ya yeye kushikilia mno kiasi hicho kwamba isiletwe kalamu na karatasi.

Kwa Nini Mtume (S.A.W.W) Hakushikilia Kuandika Ule Usia?

Kwa nini Mtume (s.a.w.w.) hakutumia nguvu yake katika kuuandika ule usia wakati ambapo licha ya kuwepo upinzani wa baadhi ya watu lakini angeliweza kabisa kumwita katibu wake na kumtolea imla ya kuuandika usia ule?

Vilevile jibu la swali hili liko wazi. Kama Mtume (s.a.w.w.) angelishikilia kuuandika ule usia, wao, wale ambao walikuwa wakisema kwamba maradhi yamemzidi nguvu, wangelishikilia zaidi ukosa adabu wao na mafuasi wao wangeyaeneza maoni haya na wakajitahidi kuyathibitisha maoni yao.

Katika hali hiyo, mbali na ukweli kwamba ukosa adabu kwa Mtume (s.a.w.w.) ungeenea na kuendelea, ule usia nao ungepoteza thamani yake. Hivyo basi, wakati baadhi ya watu walipotaka kujisahihisha kutokana na matendo yao mabaya, walipomuuliza Mtume (s.a.w.w.) kama walete kalamu na karatasi, aliingiwa mno na wasiwasi na akasema: “Baada ya yote hayo mliyoyasema, mnataka kuleta kalamu na karatasi? Mimi ninakuusieni tu kwamba muwe wema kwa dhuria wangu.”

Baada ya kusema hivyo aligeuzia mbali uso wake kutoka kwa wale waliokuwepo pale, nao waliamka na kutawanyika. Pale wakabakia Sayyidna Ali (as), Abbas na Fazdhl tu! 10

Kufanya Masahihisho Ya Jambo Hili

Ingawa ule upinzani wa dhahiri uliofanywa na baadhi ya masahaba ulimfanya Mtume (s.a.w.w.) aache kuandika ule usia, alilitambulisha lengo lake kwa njia nyingine. Historia inashuhudia ya kwamba alipokuwa yu mgonjwa sana aliuweka mkono wake mmoja begani mwa Sayyidna Ali (a.s.) na ule mwingine begani mwa Maiymunah mjakazi wake, na akaenda msikitini. Ingawa alikuwa na maumivu makali na hali isiyokuwa nzuri lakini alijikusuru hadi akaifikia mimbari na akaipanda.

Machozi yalitiririka machoni mwa watu na kimya halisi kikatanda msikitini mle. Watu walikuwa wakisubiri kuyasikia maneno yake ya mwisho na mapendekezo yake.

Mtume (s.a.w.w.) alikivunja kimya cha mkusanyiko ule na akasema: “Ninaacha miongoni mwenu vitu viwili vyenye thamani” Hapo akasimama mtu mmmoja na kuuliza: “Ni nini maana ya vitu viwili vyenye thamani?” Kisha akaongeza kusema: “Kimojawapo ni Qur’ani na kingine ni dhuria wangu.”11
Ibn Hajar Askalaani ametoa tafsiri nyingine ya kufanya masahihisho ya jambo hili na inalingana na ile ya awali. Anasema: “Siku moja, wakati Mtume alipokuwa mgonjwa, na kitanda chake kilikuwa kimezungukwa na masahaba wake, aliugeuzia uso wake kwao na kuwaambia:

“Enyi watu! Muda wa kifo changu umewadia na hivi karibuni nitakuacheni. Tambueni ya kwamba ninakuachieni miongoni mwenu Kitabu cha Allah na dhuria wangu, Ahlul Bayt wangu miongoni mwenu.” Kisha aliushika mkono wa Ali na kuuinua juu, akasema: “Ali yu pamoja na Qur’ani na Qur’ani iko pamoja na Ali na havitatengana hadi Siku ya Kiyama.”12

Mtume (s.a.w.w.) ameisimulia Hadith *Thaqalaini* kwenye matukio mbalimbali na kwa njia mbalimbali kabla ya kuugua kwake, na amekuwa akiwatahadharisha watu kuhusu vitu hivi viwili vizito, lakini pale alipokuwa yu mgonjwa kitandani alikuwa akiwatahadharisha tena watu juu ya uwiano baina ya Kitabu na dhuria wake na akasisitiza kuhusu umuhimu wao mbele ya watu walewale waliopinga kule kuandika kwake usia. Hii humfanya mtu aamini kwamba lengo la kurudiarudia huku lilikuwa ni kufanya masahihisho kwa kule kutokuwapo kwa maandishi ya usia ule.13

Ugawaji Wa Dinari

Sera ya Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na hazina ya umma (*Baytul Mal*) ilikuwa kwamba katika fursa ya awali kabisa aligawa mali ya hazina ile miongoni mwa maskini na alijiepusha na kuiweka mali ya hazina ya umma kwa muda mrefu. Hivyo basi, alipokuwa mgonjwa wa kitandani na dinari fulani alikuwa nazo mmoja wa wakeze, alimwamrisha azilete kwake.

Zile dinari zilipoletwa mbele yake alizishika mkononi mwake na akasema: “Vipi Muhammad atategemea kitu chochote kile kutoka kwa Allah kama atakutana Naye huku akiwanazo hizi?” Kisha alimwamrisha Amirul– Mu’minin kuigawa fedha ile miongoni mwa maskini.14

Mtume (S.A.W.W.) Akasirika Kutokana Na Dawa Aliyopewa

Wakati wa kuishi kwake nchini Ethiopia, Asmaa’ binti wa ‘Umays aliyekuwa ndugu wa karibu wa mkewe Mtume (s.a.w.w.) Maymunah alijifunza mchanganyiko wa dawa iliyokuwa majimaji ya mimea fulani. Alifikiria kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiugua ugonjwa wa ngozi ya nje ya mapafu (*Pleurisy*) na huko Ethiopia ugonjwa huu ulikuwa ukitibiwa kwa mchanganyiko huo.

Hali ya Mtume (s.a.w.w.) ilipozidi kuwa mbaya zaidi na akawa na maumivu makali mno alimnywesha

dawa ile. Hali ya Mtume ilipoanza kuwa nzuri kwa kiasi fulani, na akapata kulitambua tukio lile alichukia mno na akasema: “Katu Allah hamfanyi Mtume wake kuugua ugonjwa wa aina hii.”15

Buriani Kwa Marafiki

Katika kipindi cha maradhi yake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na kawaida ya kuja msikitini katika baadhi ya nyakati na kusali na masahaba wake, na pia aliweza kuzungumzia juu ya mambo fulani fulani. Katika moja ya siku hizi aliingia msikitini, akiwa amefunga kitambaa kichwani mwake na Sayyidna Ali (as) na Fadhl bin Abbas wakimshika makwapani mwake, na alikuwa akitembea kwa kuburuza miguu. Alipanda mimbari na akaanza kuzungumza, akisema: “Enyi watu! Umefika wakati wa kukuacheni, kama nimefanya ahadi na mtu yeyote yule niko tayari kuitimiza, na kama nimekopa chocote kile kutoka kwa mtu aseme, ili niweze kumlipa.”

Hadi hapo, mtu mmoja alisimama na kusema: “Katika kipindi fulani kilichopita uliniahidi kwamba kama nikioa, utanisaidia kwa kunipa pesa.” Mtume (s.a.w.w.) alimwamrisha Fadhl kumpa mtu yule kiasi kinachohitajika mara moja. Kisha alishuka kutoka mimbarini na akaenda nyumbani. Baada ya hapo alikuja tena msikitini siku ya Ijumaa (yaani siku tatu kabla ya kifo chake) na akaanza kuzungumza, na akazungumza mambo mengi ikiwa ni pamoja na haya: “Mwenye haki yoyote ile juu yangu naasimame na aitaje, kwa kuwa adhabu kwenye ulimwengu huu ni nyepesi kuliko adhabu kwenye Siku ya Hukumu.”

Hapo Sawadah bin Qays alisimama na kusema: “Wakati wa kurejea kutoka kwenye Vita ya Taa’if, ulipokuwa umempanda ngamia, uliinua fimbo yako ili umpige mnyama wako, lakini kwa bahati mbaya fimbo ile ilinipiga tumboni. Sasa ninataka kulipiza kisasi.”

Fursa iliyotolewa na Mtume (s.a.w.w.) haikuwa ya urasimu wa kinidharia tu, kwa kuwa yeye alidhamiria kweli kuelekea kwenye kuwafidia watu hata kwa ajili ya zile haki ambazo kwa kawaida si zenye kuwekwa maanani na watu.16 Hivyo basi, aliamrisha iletwe fimbo ileile kutoka nyumbani kwake. Baada ya hapo alivua shati lake ili kwamba Sawadah alipize kisasi. Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) walikuwa wakiitazama mandhari ile kwa nyoyo zilizojawa na huzuni, na machozi yakiwatiririka machoni mwao, nao walikuwa wakisubiri waone jambo lile litaishia wapi, na iwapo kama Sawadah atalipiza kisasi kweli. Hata hivyo kwa ghafla walimwona Sawadah akilibusu tumbo na kifua cha Mtume (s.a.w.w.). Hapo, Mtume (s.a.w.w.) alimwombea du’a Sawadah na akasema: “Ee Allah! Msamehe Sawadah kama vile alivyomsamehe Mtume wa Uislamu!”17

---

1. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 654; Tabaqaatu Ibn Saad, Juz. 2, uk. 216.
2. Kwa dhahiri alichomaanisha ilikuwa kwamba Mtume (s.a.w.w.) atamke usia na mmoja wa makatibu wake auandike, kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) katu haku– pata kushika kalamu mkononi mwake au kuandika jambo lolote lile.
3. Sahih Bukhari, Kitabul’ilmi’, Juz. 1, uk. 22, na Juz. 2, uk. 14; Sahihi Muslim, Juz. 14; Musnad Ahmad, Juz. 1, uk. 325; na Tabaqaatul Kubra, Juz. 2, uk. 244.
4. Sharhu Nahjul–Balagha, Ibn Abil Hadid, Juz. 2, uk. 20.
5. Sahih Muslim, Juz. 1, uk. 14, na Musnad Ahmad, Juz. 1, uk. 155.

6. Kanzul'Ammal, Juz. 3, uk. 138 na Tabaqaatul Kubraa, Juz. 2, uk. 244.
7. Marehemu Allamah Mujaahid Sharfuddin amekusanya nyudhuru zote kwenye kitabu chake kitwacho Al-Muraaji'aat na akazikanusha katika njia iliyo bora zaidi.
8. Hayaatu Muhammad, uk. 475.
9. Musnad Ahmad bin Hanbal, Juz. 1, uk. 355.
10. Bihaarul Anwaar, Juz. 22, uk. 469, kama ilivyonukuliwa kutoka Al-Irshaad ya Shaykh Mufid na Aa'lamul Wara' cha Tabrsi.
11. Biharul Anwaar, Juz. 22, uk. 476; kama ilivyonukuliwa kutoka Majaalis, cha Shaykh Mufid.
12. As-Sawa'iq, Sura ya 9, ya Juz. 2, uk. 57 na Kashful Ghummah, uk. 43
13. Hadith Thaqalayn ni moja ya zile hadith zikubaliwazo na wanahadithi wa Kisunni na Kishia kwa pamoja, na imesimuliwa na masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) katika njia sitini tofauti tofauti. Ibn Hajar Askalaani anaandika hivi: "Mtume (s.a.w) aliutaka uangalifu wa watu juu ya uwiano baina ya Kitabu na dhuria wake kwenye matukio mbalimbali kama vile kwenye Siku ya Arafa, Siku ya Ghadir Khum, alioporejea kutoka Taa'if, na hata pale alipokuwa yu mgonjwa wa kitandani." (Soma kitabu Al-Sawaaiq al-Muhriqah, uk. 136).
Marehemu Mir Ahmad Husayn wa India ameweka sehemu ya kitabu chake kwa ajili ya masimulizi ya asili za Hadith Thaqalayn. Kimetolewa hivi karibuni mjini Isfahan (Iran) katika juzuu sita. Katika mwaka 1374 Hijiriya, kitabu kidogo juu ya Hadith hii kilichapishwa na Darut Taqrib Foundation (Misri). Muhimu wake kuhu- siana na asili ya Hadith hii na heshima iliyopata kutoka kwa wanahadithi kwenye zama mbalimbali za historia ya Kiislamu vimenukuliwa kwa ufupi ndani ya kitabu hiki
14. Tabaqaatul-Kubra, Jz. 2, uk. 238
15. Tabaqaatul-Kubra, Jz. 2, uk. 236
16. Manaaqib Ali ibn Abi Talib, Jz. 1, uk. 164
17. Zaidi ya hapo, kwa vile Mtume hakulipiga tumbo la Sawadah kwa kukusudia, Sawadi hakuwa na haki ya kulipiza kisasi, lakini kitendo kile kingeliweza kufidiwa kwa kulipa fedha ya dia (fidia iliyoamrishwa). Ingawa ilikuwa hivyo, Mtume (s.a.w.w.) aliamua kuitekeleza haja yake.

Sura Ya 63: Masaa Ya Mwisho Ya Mtume (S.A.W.W.)

Mji wa Madina ulimezwa na wasiwasi na mashaka. Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) walikusanyika karibu na nyumbani kwake wakiwa wamejawa na machozi machoni mwao na nyoyo zenye huzuni. Taarifa zilizokuwa zikimiminika nje kutoka nyumbani mle zilionyesha ya kwamba hali yake ilikuwa mbaya zaidi, na yalikuwepo mategemeo madogo mno kuhusu kupona kwake. Hii ilionyesha kwamba ni kitambo kidogo tu cha uhai wake wenye thamani kilichosalia.

Idadi fulani ya masahaba wa Mtume walikuwa na hamu kubwa ya kuonana naye kwa karibu, lakini ile hali yake mbaya haikuruhusu hivyo kwa yeyote yule ila ni watu wa familia yake tu ndio waliweza kuingia chumba alicholala.

Binti yake mwenye kuheshimiwa na kumbukumbu la pekee la Mtume (s.a.w.w.), yaani Bibi Fatimah

(a.s.) alikuwa amekaa kandoni mwa kitanda cha baba yake. Alikuwa akiutazma ule uso wake mtakatifu na aliweza kuona kwamba jasho la kifo lilikuwa likimiminika kutoka usoni mwake. Akiwa na moyo mzito, macho yaliyojawa na machozi, na koo lililokabwa, alikuwa akiusoma ubeti ufuatao ambao ulisomwa na Abu Twalib katika kumsifu Mtume (s.a.w.w.):
“Uso wenye nuru ambao kutokana na heshima yake mvua ziliombwa kutoka mawinguni. Mtu aliyekimbilio la mayatima na mlezi wa wajane.”

Wakati huohuo Mtume (s.a.w.w.) aliyafungua macho yake na akamwambia yule binti yake kwa sauti ya chini: “Huu ni utungo aliousoma Abu Twalib kuhusiana nami. hata hivyo, ni bora kama badala ya utungo huo, ungeliisoma aya hii ya Qur’ani Tukufu:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۚ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ۚ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ {144}

“Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru Allah kitu. Na Allah atawalipa wanaomshukuru.” (***Surat Aali Imran, 3:144***). 1

Mtume (S.A.W.W) Azungumza Na Binti Yake

Uzoefu waonyesha kwamba kutokana na wingi wa shughuli, hisia za watu wakubwa juu ya watoto wao hufifia, kwa sababu kujishughulisha mno na mambo ya kidunia na hatimaye huzififiza hisia zihusuzo watoto wao. Hata hivyo, wakuu wa kiroho hawakumbwi na tatizo hili. Ingawa walikuwa na malengo makuu na fikira za ulimwengu mzima na shughuli zilizokuwa zikiongezeka damia, wao walikuwa na roho kuu zaidi kiasi kwamba mwelekeo wa upande mmoja hauwazuii kuzielekea zile pande nyingine.

Huba ya Mtume (s.a.w.w.) kwa mtoto wake wa pekee ilikuwa moja ya udhihirisho mtukufu wa hisia za ubinadamu, kiasi kwamba katu hakwenda safari yoyote ile bila ya kumwaga binti yake, na aliporejea kutoka safarini kwanza kabisa alikwenda kuonana naye. Alimheshimu mno kuliko wakeze na alikuwa akiwaambia masahaba zake: “Fatimah yu sehemu ya mwili wangu. Furaha yake ni furaha yangu na ghadhabu yake ni ghadhabu yangu.”2

Kila mara Mtume (s.a.w.w.) alipomwona Fatimah alikuwa akimkumbuka Khadija, yule mwanamke aliyekuwa mchamungu zaidi na mwenye huruma zaidi ulimwenguni kote, aliyezikabili shida zisizo kifani na kuutumia utajiri wake mkubwa katika njia ya ujumbe mtakatifu wa mumewe.

Katika kipindi chote cha ugonjwa wa Mtume (s.a.w.w.) Bibi Fatimah (a.s.) alibakia kandoni mwa kitanda

cha Mtume (s.a.w.w.) na hakupata kuwa mbali naye japo kwa kitambo tu. Ghafla Mtume (s.a.w.w.) akamwashiria akimtaka azungumze naye. Binti wa Mtume (s.a.w.w.) aliinama na akazungumza naye kwa kumnong'oneza.

Wale watu waliokuwa wamekizunguka kitanda cha Mtume (s.a.w.w.) hawakujua ni kitu gani walichokuwa wakikizungumza. Mtume (s.a.w.w.) alipoacha kuzungumza, Bibi Fatimah alilia sana. Hata hivyo, mara tu baada ya hayo, Mtume (s.a.w.w.) alimwashiria tena na akamnong'oneza tena. Wakati huu alikiinua kichwa chake katika hali ya furaha na midomo yenye kutabasamu. Wale waliokuwapo walishangaa sana kuziona hizi hali mbili zilizotofautiana katika wakati mmoja, na wakamwomba Bibi Fatimah (a.s.) awaeleze kile alichoambiwa na Mtume (s.a.w.w.). Aliwajibu hivi: "Mimi sitaifichua siri ya Mtume wa Allah."

Baada ya kufariki dunia kwa Mtume (s.a.w.w.) Bibi Fatimah (a.s.) aliwaeleza hali halisi ya yale aliyokuwa akiyazungumza na Mtume (s.a.w.w.), baada ya kusisitizwa na bibi Aisha akasema:

"Mara ya kwanza baba aliniarifu kuhusu kifo chake na akaeleza ya kwamba hakuna tegemeo katika kupona kwake kutokana na maradhi yake.
Hivyo basi, nilianza kulia. Hata hivyo, alipozungumza nami kwa mara ya pili aliniambia nitakuwa mtu wa kwanza kutoka miongoni mwa Ahlul–Bayt wake atakayejiunga naye. Jambo hili lilinifurahisha na nilifahamu kwamba nitakuwa pamoja na baba yangu mpenzi hivi karibuni."3

Kupiga Mswaki

Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na kawaida ya kupiga mswaki kabla ya kwenda kulala wakati wa usiku na baada ya kuamka asubuhi. Mswaki wa Mtume (s.a.w.w.) ulikuwa ni kipande cha mti wa '*Araak*' wenye faida sana katika kuziimarisha fizi, kusafisha meno na kuondoa chembechembe za chakula kutoka kwenye meno. Siku moja Abdur Rahman, umbu lake Bibi Aisha, alikuja kumtazama Mtume (s.a.w.w.). Wakati ule alikuwa kashika kipande cha mti mbichi mkononi mwake. Bibi Aisha alielewa kutokana na mtazamo wa Mtume (s.a.w.w.) kwamba alitaka apige mswaki na kile kipande cha mti. Hivyo basi, upesi akakichukua kile kipande cha mti kutoka kwa umbu lake na kumpa Mtume (s.a.w.w.) naye akapiga mswaki kwa kijiti kile.4

Mapendekezo Ya Mtume (S.A.W.W.)

Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa yu mgonjwa wa kitandani aliweka umuhimu zaidi katika kuwakumbusha watu juu ya mambo yaliyo wajibu, na katika siku zake za mwisho za ugonjwa wake aliwausia watu kwa nguvu zaidi juu ya kusali na kuwatendea wema watumwa. Alisema: "Watendeeni wema watumwa wenu, muwe waangalifu juu ya chakula na mavazi yao, zungumzeni nao kwa upole na zigaweni nao kazi zenu za maisha."

Siku moja Ka'ab Akhbaar alimwuliza Khalifa wa pili: "Mtume (s.a.w.w.) alisema nini muda mfupi tu kabla

ya kifo chake?" Yule Khalifa alimuashiria Amirul-Mu'minin (a.s.) aliyekuwamo kwenye mkutano ule, akasema: "Muulize yeye huyo." Sayyidna Ali (a.s.) akasema: "Wakati kichwa cha Mtume (s.a.w.w.) kilipokuwa kimeegemea begani mwangu, alisema: "Sala, Sala". Kisha Ka'ab Akhbaar akasema: "Hii ndio njia ya Mitume waliotangulia pia."5

Katika dakika za mwisho za uhai wake Mtume (s.a.w.w.) aliyafungua macho yake na akasema: "Mwiteni ndugu yangu, aje na akae karibu nami." Wale wote waliokuwapo pale walielewa ya kwamba hakuwa na maana ya yeyote yule ila Sayyidna Ali (as). Ali (a.s.) alikaa karibu na kitanda chake lakini alihisi kwamba alitaka kuamka kutoka kitandani mwake. Hivyo alimwamsha Mtume (s.a.w.w.) kutoka pale kitandani pake na akamwegemeza kifuani mwake.6

Mara tu baada ya hapo, dalili za kifo zilianza kujitokeza kwenye mwili wake mtakatifu. Mtu mmoja alimuuliza Ibn Abbas: "Ni mapajani mwa nani alimofia Mtume (s.a.w.w.)?" Ibn Abbas alijibu akisema: "Mtume alitawafu wakati kichwa chake kikiwa mapajani mwa Ali." Yule mtu aliongeza kusema: "Aisha anadai kwamba alipofariki dunia Mtume (s.a.w.w.) kichwa chake kiliegemea mapajani mwake."

Ibn Abbas alilipinga dai lake hilo na akasema: "Mtume alifariki dunia mapajani mwa Ali, na Ali na kaka yangu Fadhl walimwosha." 7 Katika moja ya hotuba zake, Imam Ali (a.s.) amelitaja jambo hili kwa maneno haya: "Mtume alifariki dunia kichwa chake kikiwa kifuani mwangu. Niliosha maiti yake huku malaika wakiwa wananisaidia."8
Idadi fulani ya wanahadithi wamenukuu kwamba kauli ya mwisho aliyoitamka Mtume (s.a.w.w.) kabla ya kufariki kwake dunia ilikuwa ni: "Kuwa pamoja na Allah."

Inaonyesha kwamba wakati wa kufariki dunia kwake Malaika Mkuu Jibriil alimpa uhuru wa kuchagua, apone kutokana na maradhi yake na kurejea kwenye ulimwengu huu au Malaika wa mauti aichukue roho yake na auendee ulimwengu wa Akhera na kwenda kuishi huko pamoja na watu waliotajwa kwenye aya hii:

وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۚ وَحَسُنَ أُولَٰئِكَ رَفِيقًا {69}

"Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao watakuwa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii na Wakweli na Mashahidi na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!" **(*Surat al-Nisa, 4:69*).**

Mtume (s.a.w.w.) aliitamka kauli hiyo hapo juu na akafariki dunia.9

Siku Ya Mwisho

Roho takatifu na tukufu ya Mtume wa Allah (s.a.w.w.) ilipaa Peponi katika Siku ya Jumatatu mwezi ishirini na nane Safar (Mfungo Tano).10 Maiti yake ilifunikwa shuka la Yemen na kwa kipindi kifupi hivi iliwekwa pembeni mwa chumba. Kutokana na vilio vya wanawake na vya ndugu wa karibu wa Mtume (s.a.w.w.), watu waliokuwako nje ya kile chumba walijua kwamba Mtume (s.a.w.w.) kaishaitoka dunia. Mara tu baada ya hapo taarifa za kifo chake zilienea mjini mwote.

Kwa sababu zisizoeleweka hadi hivi sasa, Khalifa wa pili alipiga kelele huko nje ya nyumba kwamba Mtume hajafa bali amekwenda mbele ya Allah kama alivyofanya Nabii Musa (a.s.). Alilishikilia jambo hili sana, na ulikuweko uwezekano kwamba angeliweza kuwafanya watu wengine kumuunga mkono katika maoni haya, lakini wakati ule mmoja wa masahaba 11wa Mtume (s.a.w.w.) alimsomea aya ifuatayo:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۚ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ۚ وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ {144}

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru Allah kitu. Na Allah Atawalipa wanaomshukuru." **(*Surat Aali Imran, 3:144*)**12

Aliposikia aya hii aliliacha dai lake hilo na akatulia.13

Imamu Ali (a.s.) aliiosha maiti takatifu ya Mtume (s.a.w.w.) na kumkafini kama alivyoelekeza yeye mwenyewe Mtume (s.a.w.w.) kwamba maiti yake ioshwe na mtu aliyekuwa karibu zaidi naye,14 na mtu huyo hawezi kuwa yeyote mwingine ila Sayyidna Ali (a.s.). Kisha aliufunua uso wa Mtume (s.a.w.w.) huku akiwa analia sana, na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Nilikupenda mno kuliko vile nilivyowapenda wazazi wangu. Kifo chako kimeishilizia Utume, Wahyi, na Mitume watokao kwa Mola. Wakati kifo cha Mitume wengine hakikufanya hivyo.
Kifo chako kimeleta huzuni ambayo huzuni yoyote nyingine imesahaulika. Huzuni ya kutengana nawe imekuwa huzuni kubwa na kila mtu ameihisi. Kama usingetuamrisha kuwa na subira, na kutoomboleza na kulia kwa sauti kuu, tungeliendelea kulia na kuomboleza bila ya kukoma, ingawa maombolezo yote haya yasingelikuwa chochote kile yanapolinganishwa na hasara halisi ya kutengwa kwetu na wewe. Lakini kifo ni tukio lisiloepukika, hakuna awezaye kukipa kisogo kifo na hakuna awezaye kukizuia kisije. Tafadhali utukumbuke uwapo mbele ya Allah."15

Mtu wa kwanza kumsalia Mtume (Sala ya maiti) alikuwa ni Imam Ali (a.s.). Baada ya hapo waliingia masahaba wengine kwa vikundi na kumsalia Mtume (s.a.w.w.) na ibada hizi ziliendela hadi adhuhuri ya

Jumanne. Baada ya hapo iliamuliwa ya kwamba maiti takatifu ya Mtume (s.a.w.w.) izikwe kwenye nyumba ileile alimofia. Kaburi lilitayarishwa na Abu Ubaydah bin Jaraah na Zayd bin Sahl na mazishi yalifanywa na Imam Ali (a.s.) akisaidiwa na Abbas na Fadhl.

Tukio hili lilikuwa ni tukio la masaibu makubwa mno. Huyu mtu mashuhuri aliyeibadili hali ya wanadamu kwa juhudi zake na kujitoa mhanga na akazifungua kurasa mpya katika ustaarabu wa binadamu amefariki dunia.16

Bila shaka mtu aliye na fikira zisizo na upendeleo anapochunguza mambo mbalimbali ya sifa za mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama mwanadamu, mkuu wa familia, mwanajamii, hakimu, mtawala, mwalimu, kamanda wa jeshi na kiongozi, huufikiria uamuzi wa kwamba ukamilifu wake katika kila jambo ni ushuhuda wa dhahiri wa kuwa yeye yu Mtume wa Allah. Historia ya mwanadamu haijawahi kuona mtu yeyote mwingine aliyelifikia daraja la ukamilifu kama huyu.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amechagua mambo mengi katika ustawi wa mwanadamu kwa ujumla. Kwanza, yeye mwenyewe alifanya kazi ya kuufikisha Ujumbe, aliutekeleza Ujumbe wa Allah na kisha akawaita watu wamfuate.

Alizidumisha haki za watu katika zama ambazo haki za watu zilikuwa zikinyakuliwa; alidumisha uadilifu wakati dhuluma ilikuwa ikienea kila mahali; aliasisi usawa wakati ubaguzi usiofaa ulikuwa jambo la kawaida; na aliwapa watu uhuru walipokuwa wakiugua kwenye uonevu, ukatili na dhuluma.

Aliuleta ujumbe uliomfunza mwanadamu kumtii na kumcha Allah tu, na kuomba msaada kutoka kwake tu. Ujumbe wake ulioletwa kwa ajili ya wanadamu unayahusu mambo yote ya maisha ya mwanadamu ikiwa ni pamoja na haki, uadilifu, usawa na uhuru. Huu ni ujumbe ambao kutokana nao, mwanadamu anakipata tena kile ambacho ni kinyimwa. Basi kwa nini tusiingie tena kwenye ulezi wake, ili mwanadamu aweze kuokolewa kutokana na maangamizi, na kuweza kuipata amani, maendeleo na furaha.

---

1. Soma Al-Irshaad, cha Shaykh Mufid, uk. 98.
2. Sahih Bukhari, Juz. 5, uk. 21
3. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2, uk. 247; Tarikhul Kamil, Juz. 2, uk. 219.
4. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2 uk. 23; Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 654.
5. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2, uk. 254.
6. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2, uk. 263
7. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 2 uk. 263
8. Nahjul-Balaghah
9. Aa'lamul Waraa', uk. 83.
10. Wanahadithi na waandishi wa wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) wa Kishia wote wanaikubali tarehe hii, na kwenye Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 658, imenukuli- wa katika hali ya masimulizi.
11. Kwa mujibu wa Sahih Bukhari (uk. 7) alikuwa ni Abu Bakr (r.a).
12. Soma Al-Irshaad, cha Shaykh Mufid, uk. 98

13. Siiratu Ibn Hisham, Juz. 2, uk. 656.

14. Tabaqaatu Ibn Sa'ad, Juz. 1, uk. 57.

15. Nahjul Balagha, Hutuba na. 23

16. Baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kufariki matatizo mengi sana yalijitokeza katika kazi yake na utekelezaji wa kazi yake. Lililokuwa chanzo kikuu miongoni mwao lilikuwa ni swala la Ukhalifa na uongozi wa Umma wa Kiislamu. Hata kati-ka siku za kabla ya kifo chake dalili za tofauti na mfarakano ziliweza kuonekana waziwazi miongoni mwa Waislamu. Licha ya ukweli kwamba suala hili lilikuwa moja ya masuala yaliyokuwa nyeti na sura muhimu za historia ya Uislamu, ni nje ya upeo wa mazungumzo yetu ya hivi sasa. Hivyo basi, tunaweza kuyaishilizia masimulizi yetu hapa, na tunamshukuru Allah, kwa baraka Yake. (Kwa maelezo zaidi, tafadhali soma vitabu vitolewavyo na: "Islamic Seminary, P.O. Box 5425, Karachi, Pakistani au vya Al-Itrah Foundation)"

Majina Ya Vitabu Vilivyorejewa

'Abaqaatul Anwaar - cha Sayyid Hamid Husayn Musawi.

Al-Amaali – cha Shaykh Saduq.

Al-Asarul Arba'ah-Sadruddin Shiraazi (maarufu kwa jina la Mulla Sadraa).

Al-Amwaal - cha Abil 'Ubayd.

Abu Twalib - Mu'umin Quraysh – cha Abdullah al-Khunayzi.

Biblia.

Bihaarul Anwaar - cha Allamah Muhammad Baaqir Majlis.

Al-Bidaayah wan Nihaayah - cha Ibn Kathir Qarayshi.

Diwaan Abu Twaalib - cha Abu Twalib.

Daa'iratul Ma'aarif –cha Farid Wajdi.

Durrul Manthur – cha Jalaluddin Abdur Rahmaan Suyuti.

Darajaatur Rafiy'ah – cha Sadruddin Ali Khan.

Futuhul Buldaan – cha Abu Ja'afr; Yahya bin Jaafar Balaazari.

Futuhusha Shams.

Al-Fadhaa'il Shaazaan.

Furu' al-Kaafi – cha Muhammad bin Ya'aqub Kulayni.

Fahrist Nahjaashi – cha Najashi.

Hayaat Muhammad - cha Hasnayn Haykal.

Al-Isaabah fi Tamizis Swahaabah – cha Ibn Hajar al-Asqalaani.

Al-Imtaa Asmaa' – cha Taqi'uddin Ahmad Shaafi'I Miqrizi.

Al-Isti'aab fi Tamizis Sahaabah – cha Ibn Abdul Barr makki

Al-Irshaad – cha Shaykh Mufid.

Al-Iqbaal – cha Sayyid bin Taa'us.

Iqdul Farid – cha Ibn Abd Rabbihi.

Jawaami'ul Kalim - cha Shaykh Ahmad.

Kashaful Ghummah – cha Abul Fath Ali Bin 'Isa Arbali.
Kanzul 'Ummaal – cha Alaa'ulddin Ali al–Muttaqi.
Al–Kashshqaaf – cha Mahmud bin Umar Zamakhshari.
Limaadhaa Khasiral Aalam bi Inhitaalil Muslimin – cha Abul Hassan Nadawi.
Murujudh Dhahab – cha Ali bin Husayn Mas'ud.
Manlaa yahzaruhul Faqih – cha Shaykh Tusi.
Majma'ul Bayaan – cha Shaykh Abu Ali Tabarsi.
Manaaqib – cha Allamah Ibn Shahr Ashob. *Musnad* – cha Ahmad bin Hanbal.
Mughaazi – cha Waqidi.
Al–Mustadrak'alas Swahihiyn – cha Hakim Nishaapuri.
Mafaatihul Ghayb – cha Fakhruddin Raazi.
Majaalis – cha Ibnush Shaykh.
Al–Mahaasin – cha Abi Ja'afar Ahmad al–Barqi.
Al–Muraaji'aat – cha Allamah Sharafuddin al–Aamili.
Al–Mizaan – cha Allamah Tabaatabaa'i
Al–Nass wal Ijtihaad – cha Allamah Sharafuddin al–Aamini.
Naasikhut Tawaarikh – cha Muhammad Taqi Sipher
Qurbul Asnaad – cha Abdullah bin Ja'afar al–Himyara.
Qaamus Kitaab Muqqadas
Ruhul Ma'ani – cha Mahmud Aalusi.
Rawzah al–Kaafi – cha Muhammad bin Yaa'qubi Kulayn.
Safinatul Bihaar – cha Allamah Muhammad Baqir Majlisi.
Siirah–i – cha Ibn Hishamu.
Siirah Halabiyah – cha Ali bin Burhaamuddin halabi Shaafi'i
Tarikh al–Kaamil – cha Ibn Athir.
Tarikhut– Tabari –cha Muhammad bin Jurayr Tabari.
Tarikh Ya'qubi – cha Ahmad bin Ali Ya'qubi.
Tibyaan – cha Shaykh Tusi.
Tadhkiratul Khawaas – cha Abu Muzaffar Yusuf Bin Jawzi,.
Al–Taaj – cha Jaahiz.
Tafsir – cha Ali Ibrahim.
Tuhaful 'Uquul – cha Abu Muhammad bin Shaybah Karraani
Usudul Ghaabah fi Ma'arifatis Sahaabah – cha Ibn Athir Jazari.
Usudul Kaafi – cha Muhammad bin Ya'aqub Kulayni.
'*Uyunul Akhbaar*, cha ibn Qutaybah.
Wasaa'ilush Shi'ah – cha Shaykh Hurr al–Aamili.
Yanabi'ul Mawaddah – cha Shaykh Sulaymaan Hanafi al–Qanduzi.

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu

35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as–Salaatu Khayrun Mina –'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume – Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume – Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume – Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu

74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
75. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali
87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Idil Ghadiri
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

113. Shiya N’abasahaba
114. Iduwa ya Kumayili
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Historia na sera ya vijana wema
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaa ya kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Mas–ala ya Kifiqhi
139. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili

Back Cover

Historia inatuambia kuhusu ustaarabu mkubwa uliopita hapo kale na mwishowe ukapotea. Hivi sasa tumebakiwa na masalio na magofu bubu yanayotukumbusha zama za kale za wanaadamu zilizochakaa.

Imam Ali (a.s.) alimpa dokezo la fikra zake mwanawe ambalo ni lenye kuhusika na jambo hili. Alisema: “Mwanangu mpenzi! Ingawa muda wa maisha yangu si mkubwa kama ule wa watu wengine waliofariki dunia kabla yangu, lakini nilijichukulia hadhari kubwa kujifunza maisha yao.

Kwa juhudi nyingi niliyapitia matendo yao na nilizifikiria fikra na maten– do yao. Niliyachunguza masalio ya vitu vyao visivyo na uhai na magofu, na nikayafikiria maisha yao kwa makini mno kiasi kwamba

nilijihisi kana kwamba niliishi na kufanya kazi pamoja nao tangu kwenye zama za awali za historia hadi kwenye hizi nyakati zetu, na ninayajua yaliyowatendea mema na yaliyowadhuru.”

Hakika sifa moja ya historia iangazayo mno ni kwamba, inazichukua taarifa za maisha ya watu wakuu wa kale. Hakika watu hawa waliiunda historia kwa kuwa walileta mapinduzi na mabadiliko kwenye mtindo wa maisha ya wanaadamu.

Miongoni mwa hawa watu wakuu, hakuna hata mmoja aliyeishi maisha yenye mambo mengi, ya kimapinduzi na yenye maana kama aliyoishi Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Hakuna yeyote miongoni mwao aliyeziacha athari za kudumu kwenye jamii aliyojitokeza kama alivyofanya Mtume wa Uislamu (s.a.w.w.). Huu ni ukweli uliokubaliwa na karibuni wanahistoria wote wawe ni wa Mashariki au wa Magharibi.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [13]
Katika mtandao: www.ibn-tv.com [14]

Source URL: https://www.al-islam.org/node/25197

Links
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/25197%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/25197%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/sheikh-jafar-subhani
[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/person/maalim-dhikiri-um-kiondo
[6] https://www.al-islam.org/library/general-history-politics
[7] https://www.al-islam.org/tags/historia
[8] https://www.al-islam.org/tags/vita
[9] https://www.al-islam.org/tags/jeshi
[10] https://www.al-islam.org/tags/hadith
[11] https://www.al-islam.org/person/mtume-muhammad-saw
[12] https://www.al-islam.org/person/imam-ali-1
[13] mailto:alitrah@raha.com
[14] http://www.ibn-tv.com